Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NNE

**Kikao cha Saba – Tarehe 4 Februari, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 83

**Umiliki na Uendeshaji wa Shirika la Ndege ATCL**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imerejesha umiliki w Shirika la Ndege *(ATCL)* ili kuliongezea ufanisi na masafa ya ndani na ya kimataifa:-

(a) Je, kuna hatua gani za makusudi za kuipa *ATCL* mtaji wa kutosha?

(b) Je, ni sababu zipi zimeifanya *ATCL* kupata hasara na kuwa na madeni?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na )b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuliwezesha Shirika la Ndege la Tanzania *(ATCL)* kupata mtaji wa kuendesha shughuli zake kwa ufanisi, Serikali imemtafuta na kumpata mwekezaji binafsi ambaye yuko tayari kuingia ubia na Kampuni ya Ndege ya Tanzania *(ATCL)* kwa kununua hisa zipatazo asilimia 49 za Serikali ndani ya *ATCL*. *(Makofi)*

Mwekezaji huyo ni kampuni ya *China SONANGOL International Limited (CSIL)* kutoka Jamhuri ya Watu wa China ambayo imekubali kushirikiana na Serikali kutafuta fedha za kutekeleza mpango mkakati wa *ATCL* ambapo unahusu kununua ndege tisa za aina mbalimbali kwa matumizi ya safari za ndani na nje ya nchi, mafunzo kwa Marubani

na Wahandisi na kubadili mifumo mbalimbali ya uendeshaji ili kuwezesha Kampuni kutoa huduma zake kwa ufanisi na kuweza kuhimili ushindani.

Kwa sasa Serikali imekamilisha nyaraka muhimu zitakazowezesha uuzaji wa hisa hizo kufanywa kabla ya kusaini mkataba na mwekezaji huyo. Serikali pia inakamilisha zoezi la kuhakiki mahesabu ya *ATCL* yanayoishia Juni 2008, kwa kutumia kampuni ya *PriceWaterHouse Coopers* pamoja na kukamilisha zoezi la kutathmini mali na madeni ya *ATCL*, kwa kutumia Kampuni ya *Ernest and Young.* Mwekezaji aliyepatikana na upande wake pia ametaka kufanya tathmini ya menejimenti ya *ATCL* (*Management Valuation*). Kazi inayotarajiwa kufanywa na Kampuni ya *Aerogestion* ya Ufaransa kwa gharama za mwekezaji. Mkataba wa kazi hiyo tayari umesainiwa na kazi itaanza muda wowote kuanzia sasa. Baada ya mazoezi haya kukamilika, Mkataba kati ya Serikali na Kampuni ya China *SANANGOL International (CSIL)* utatiwa saini na hivyo *ATCL* kupata mtaji unaohitajika.

(b)Mheshimiwa Spika, sababu ambazo zimeifanya Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)* kupata hasara na kuwa na madeni makubwa zinatokana na ubia uliokuwepo kati ya *ATCL* na Shirika la Ndege la Afrika Kusini *(South Africa Airways (SAA)* ambao ulianza Novemba 2002. Ubia huo haukuendeshwa vizuri kama ilivyotarajiwa na hivyo kusababisha Kampuni ya Ndege ya *(ATCL)* kuwa na hali mbaya kiutendaji na kuathirika kimapato. Hali ya kuzorota kwa Kampuni iliendelea hadi Agosti 2006, wakati Serikali ilipositisha ubia ule. Wakati wa kusitisha Mkataba kati ya ATCL na SAA, Kampuni ya Ndege ya Tanzania ilikuwa na madeni yanayofikia shilingi bilioni 13.2.

Pamoja na athari zitokanazo na ubia huo, sababu nyingine inatokana na mtaji mdogo pamoja na kuendelea na idadi kubwa ya wafanyakazi ambayo haioani na idadi ya ndege za *ATCL*. Vile vile kuendelea kutumia ndege za zamani kama aina ya *Boeing 737-200;* ndege hizi zinatumia mafuta mengi na matengenezo ya mara kwa mara hali inayoongeza gharama za uendeshaji wa Kampuni. Aidha kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia kumechangia kwa *ATCL* kupata hasara na pia kulimbikiza madeni.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri anajua kabisa kwamba Shirika la Ndege ni kiungo muhimu sana kwa usafirishaji na kwa uchumi hapa nchini na anasema kwamba mchakato wa kufanya unaendelea wa kusaini mkataba mpya na mwekezaji.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba ni lini Shirika hili la Ndege la Tanzania linalobeba hadhi ya Tanzania litaanza kufanya kazi kwa ufanisi kama ambavyo inategemewa?

Swali la pili, miongoni mwa aibu mbaya kubwa ambayo imewahi kutokea katika Shirika la Ndege ni pamoja na kufungiwa mwishoni mwa mwaka jana kwa kukosa mafuta, kwa kukosa pesa za kulipa wafanyakazi na hata kufungiwa na *Civil Aviation* na kwa sasa hivi limefungiwa na Shirika la Ndege la Kimataifa *IATA*. Je, anachukua hatua gani kama itabainika Menejimenti au Bodi imesababisha aibu kama hii ikatokea kwa nchi

ya Tanzania. Kama ni kuwafungulia kesi za uhujumu au kuwachukulia hatua kali ili wasije wakarudia tena.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi ni kwamba sasa hivi yapo mazoezi yanayoendelea ya kutuwezesha kufika katika mchakato wa kusaini mkataba. Mawili yanasimamiwa na Serikali ya Tanzania ambayo ni yale ya tathmini ya mali pamoja na uhakiki wa mahesabu ambayo tunatazamia kwamba kufikia mwisho wa mwezi hu wa Februari yatakuwa yamekamilika; na kwa upande wa mwekezaji tuna uhakika kwamba naye ataharakisha lile zoezi analoendelea nalo la kutathimini ya Menejimenti. Mazoezi yakishakamilika mchakato wa kusaini mkataba utaendelea na hatimaye kuliwezesha Shirika liweze kupata mtaji wa kuweza kujiendesha kwa matarajio tunayoyakusudia.

Mheshimiwa Spika, la pili nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba matatizo mengi yamelikumba Shirika hili baadhi ya matatizo yanatokana na haya niliyoyaeleza. Baada ya Serikali kugundua yote haya kwa upande wetu Waziri aliunda *task force* ya kuweza kufuatilia matatizo yaliyosababisha kusuasua huko pamoja na mambo mengine ya uendeshaji mbovu wa Shirika la *ATCL*. Kamati hiyo imeshawasilisha taarifa kwa Waziri inafanyiwa kazi kutokana na mapendekezo tutachukua hatua muafaka. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inavunja mkataba wake na Shirika la Ndege la Afrika Kusini, ilitaka Serikali iendeshe Shirika hili lenyewe na ikaenda kutafuta ndege za kukodi nje. Kampuni ya *ATCL* ilikodi ndege ambayo ilikuwa inafanyiwa *C-check* na ndege ambayo ilikuwa ni kongwe sana kiasi cha kwamba ikashindwa kuruka lakini mbaya zaidi katika mkataba ule ndege hayajakamilika matengenezo *ATCL* ilikuwa inalipa dola zisizopungua 370,000. Je, haya yote Serikali haikuona mpaka tukafika hali hii leo ndege za *ATCL* zimeshindwa kuruka na kwa hasara hii iliyopatikana na hata kuchukua hatua za Menejimenti iliyofanya makosa haya? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyoikumba *ATCL* nimeyaeleza katika jibu la msingi. Moja ya matatizo nilisema kwamba ilikuwa inatumia ndege mbovu ambayo tayari Mheshimiwa Mbunge amebainisha katika swali lake. Sasa juu ya Serikali kuchukua hatua, nasema kwamba katika mchakato wa kutathimini uendeshwaji wa Shirika hili tulidhani kwamba njia sahihi za kuunda kile kikosi kazi ambacho nimekieleza hapa. Kwa kweli tuwe na subira tuone matokeo ya mapendekezo hayo Serikali itakavyoyatumia.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anakiri kwamba Shirika lilithubutu kurusha ndege mbovu, anaweza akauthibitishia umma wa Tanzania kwamba hiyo ilikuwa ni kuhatarisha maisha ya raia na abiria?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nimesema hapa baadhi ya sababu zilizosababisha kususua kwa uendeshaji wa shirika hili. Kulikuwepo na ndege mbovu zimetajwa hata katika swali ambalo limeulizwa hivi karibuni. Sasa suala la matumizi ya ndege mbovu siwezi nikasema ilikuwa inahatarisha maisha ya wananchi kwa sababu hata katika ndege nzima inawezekana kabisa hatari ikatokea. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba ilikuwa inatumia ndege hizo kuweza kujinusuru ili iweze ikaendelea kufanya kazi. Lakini niseme tu kwamba uendeshaji wa ndege mbovu ni hatari.

**SPIKA:** Natumaini hizo zinazoruka sasa sio mbovu. Waheshimiwa bado tupo kwenye Wizara hiyo hiyo swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama wa Peramiho.

Na. 84.

**Barabara ya Muhukuru –Mitomoni – Mkenda.**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa anakagua ujenzi wa daraja la Muungano kati ya Msumbuji na Tanzania eneo la Muhukuru –Mitomoni – Mkenda aliagiza barabara hiyo sasa iwe ya taifa na ijengwe kwa kiwango cha lami:-

Je, Serikali imezingatia kwa kiasi gani utekelezaji wa agizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mheshimiwa Rais alipofanya ziara katika Mkoa wa Ruvuma, alikagua ujenzi wa daraja linalounganisha Tanzania na Msumbiji eneo la Mitomoni, tarehe 25 Julai, 2008. Mheshimiwa Rais aliagiza barabara ya Songea hadi Mitomoni yenye urefu wa kilometa 125 ipandishwe hadhi kutoka barabara ya Mkoa na kuwa barabara Kuu na ijengwe kwa kiwango cha lami.

Kwa sasa barabara hii ni ya Kitaifa na inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS).* Barabara hii pia ni miongoni mwa barabara zilizokuwa zimependekezwa na Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Ruvuma kupandishwa hadhi kuwa Barabara Kuu. Katika zoezi la kitaalam la kuhakiki barabara zote zilizopendekezwa kupandishwa hadhi, barabara hii nayo inahakikiwa ili ipandishwe hadhi kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais. Kuhusu kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami, Wizara yangu imezingatia agizo la Mheshimiwa Rais na hivi sasa mipango na taratibu za kuwezesha barabara hiyo kujengwa kwa kiwango cha lami inaandaliwa

ambapo kwa maoteo ya Bajeti ya mwaka 2009/2010 Serikali imepangwa kufanya upembuzi yakinifu ili barabara hiyo iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa maendeleo ya Jimbo la Nyasa kule Msumbiji yanaenda kwa kasi kubwa sana ukilinganisha na maendeleo ya Jimbo la Peramiho katika nchi hii ya Tanzania; na kwa kuwa wenzetu wa Jimbo lile la Nyasa wameshaweka barabara yao lami na inakaribia sasa kufika katika eneo la mpaka wa Tanzania na Msumbiji na sisi huku bado hatujafikia kiwango hicho Je, Mheshimiwa Waziri na Wizara yake ipo tayari sasa kutupatia mpango mkakati utakaoonyesha ni lini upembuzi yakinifu utaishia na utekelezaji wa uwekaji wa lami utaanza na kukamilika katika barabara hiyo ili kweli tuone nia njema ya kutekeleza agizo la Serikali ipo kama Mheshimiwa Rais alivyokusudia?

La pili, kwa kuwa wananchi wa Kata ya Muhukuru na Kata ya Mpitimbi maeneo ambayo barabara hiyo ya kitaifa inapita kuelekea huko mpakani wamefurahishwa sana sana na kitendo cha Mheshimiwa Rais kwenda kule na kukagua barabara hiyo na kutoa maagizo hayo makubwa je, Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu yupo tayari sasa kuja kutembelea maeneo hayo na kutoa majibu haya kwa wananchi ili wapate moyo kwamba maagizo ya Mheshimiwa Rais yanatekelezwa kama yalivyopangwa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mhagama na wananchi wa Jimbo la Peramiho na Mkoa wa Ruvuma ya kwamba maagizo ya Mheshimiwa Rais kwetu sisi ni Sheria na ni utekelezaji na ndiyo maana sasa hivi tumeanza mara moja kuandaa mipango na mikakati ambayo itawezesha kutekeleza.

Hili agizo na kwa hiyo kwa kuanzia mwaka unaokuja wa kuweka fedha katika Bajeti ya Serikali ni moja ya mambo ambayo tunatazamia kuwa ni sehemu ya mpango ambao tupo tayari kumkabidhi Mheshimiwa Mbunge ili wananchi wa Peramiho waweze kuona.

Lakini eneo la pili nataka niwahakikishie wananchi wa maeneo ya Mpitimbi na kwingineko ambao Mheshimiwa Rais alipita ya kwamba Serikali iko makini na iko thabiti katika kutekeleza maagizo ya Rais mimi mwenyewe au Waziri wangu tupo tayari kutembelea eneo hilo kutoa majibu haya kwa wananchi. (*Makofi*)

Na. 85

**Kituo cha Ajira –Mwanza**

**MHE. MKIWA ADAM. KIMWANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imefungua Kituo cha Ajira Kanda ya Ziwa pale Mwanza mwezi Mei, 2007 na mpaka kufikia mwezi Juni 2008 kituo kimeandikisha watafuta kazi 405 na kuunganisha vijana 243 kwa waajiri, kati ya hao wanaume 169 na wanawake 74.

(a) Je, Serikali inaweza kutueleza viwango vya elimu vya vijana hao?

(b) Je, ni katika fani gani za uajiri ambazo vijana hao wameunganishwa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa Serikali imefungua Kituo cha Ajira Kanda ya Ziwa pale Mwanza ambacho toka Julai, 2008 kimebadilishwa na kuwa Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (*Tanzania Employment Service Agency*) kwa lengo la kuwaunganisha vijana watafuta kazi wenye sifa za fani husika kwa waajiri wenye mahitaji ya kuwaajiri. Viwango vya elimu ya vijana hao inaanzia kiwango cha chini kabisa cha shule ya msingi hadi Chuo Kikuu. Hata hivyo tukichambua zaidi kwa vijana walioandikishwa, idadi kubwa ni wale waliomaliza zaidi kwa vijana walioandikishwa idadi kubwa ni wale waliomaliza kidato cha nne na cha sita bia luwa na kozi yoyote ambao ni asilimia 38 ya wote waliojiandikisha.

Kundi jingine ni wale wenye Stashahada ya Juu (*Advanced Diploma*) na Shahada ya Chuo Kikuu (*University Degree*) ambapo ni asilimia 13 na kufuatiwa na kundi la wenye Astashahada (*Certificate*) na Stashahada (*Diploma*) ambao ni asilimia tano (5). Aidha kundi lililobaki (asilimia 3) linawahusisha watafuta kazi walioshindwa kuhitimmu Elimu ya Msingi na wale ambao hawakupata fursa ya kusoma.

(b)Mheshimiwa Spika, Fani ambazo watafuta kazi hao wameunganishwa ni Ukatibu Muhtasi, Ukarani, Ulinzi, Uhasibu, Masoko, Utawala na Menejimenti, Uhandisi, Ualimu wa awali, Uhudumu wa majumbani na maofisa, ufundi magari na umeme, ufundi wa kompyuta, upishi, utabibu, uboharia, udereva na utunza fedha.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri maswali ya nyongeza. Kutokana na ukubwa wa Jiji la Mwanza. Je, Serikali haioni kwamba idadi hii inayoajiri kwa mwaka ni ndogo sana kulinganisha na vijana walioko katika Mji wa Mwanza? Je, Serikali ina mpango gani ya kuongeza uajiri katika Mji wa Mwanza kulingana na ukubwa uliopo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli jukumu la Wizara kupitia *TAESA* ni kuwaunganisha wale wanaotafuta kazi na waajiri wanaotafuta wafanyakazi. Kwa hiyo, ni jukumu kwa kweli la hawa wanaotafuta kazi. Kwa hiyo, ni jukumu kwa kweli la hawa wanaotafuta kazi

kujitokeza kwenye Ofisi za *TAESA* ili waweze kujiandikisha na kuunganisha na waajiri. Kwa hiyo, si jukumu letu sisi jukumu letu ni kutangaza kwamba tuna ofisi hizi. Nichukue nafasi hii kwa kweli kueleza kwamba ukiacha Ofisi ya Dar es Salaam na Mwanza ambazo tayari zinafanya kazi za *TAESA* tayari Wizara inampango wa kufungua Kanda zingine huko Arusha, Mtwara, Mbeya na hapa Bungeni. Kwa hiyo, tutaongeza wigo wa Ofisi za *TAESA* ili waajiri wengi na wanaotaka kuajiriwa waweze kuunganiswa. Kuhusu kukuza ajira kwa kweli njia mojawapo ni hiyo lakini kubwa kwa kweli ni watu au vijana kuwa na mikakati ya kutafuta ajira na sisi kama Serikali au Wizara tutafanya juhudi za kuwasaidia mbinu mbalimbali za kuweza kujiajiri na namna ya kutafuta mitaji.

Na. 86

**Hisa za Wateja Katika Vitega Uchumi vya Mashirika ya Bima na NSSF**

**MHE. DR. RAPHAEL CHEGENI (K.n.y. MHE. VEDASTUS M. MANYINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mashirika ya Bima, *NSSF* yamewekeza vitega Uchumi vingi katika majengo. Je, wateja wa Mashirika hayo wana Hisa katika vitega Uchumi hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mashirika ya Bima na *NSSF* ni Mashirika ambayo yameanzishwa kwa Sheria maalum kwa makusudi maalum. Mashirika ya Bima yameanzishwa kutoa huduma ya kutoa fidia kwa wateja wanaopata majanga mbalimbali.

Wateja wa Mashirika ya Bima hulipa *(premiums)* kulingana na aina ya Bima waitakayo, na badala yake wanapata fidia kama wakipata ajali kufuatana na Sheria. Fidia zinazotolewa na Mashirika ya Bima ni pamoja na zile za ajali, upotevu wa mali, elimu kwa watoto na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, *NSSF* imeanzishwa kutoa huduma ya mafao kwa wanachama wake kwa majanga wanayopata kama ilivyoainishwa katika Sheria iliyoanzishwa mfuko huo. Wanachama wa *NSSF* hutoa michango yao kila mwezi na shirika huwajibika kuwalipa mafao yaliyo bora wakati unapofika.

Mheshimiwa Spika, mafao haya ni kama Pensheni ya Uzeeni, Pensheni ya Ulemavu na Pensheni ya Warithi kwa upande wa mafao ya muda mrefu. Mafao ya muda mfupi ni Huduma za Matibabu, Mafao ya Kuumia kazini.

Fedha zinazokusanywa huwekezwa katika vitega uchumi mbalimbali ili kuzalisha fedha zaidi ambazo sehemu yake hutumika kujikimu gharama za uendeshaji na nyingine hutumika kuboresha huduma na mafao yatolewayo kwa wanachama.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo ni dhahiri kuwa mwanachama mmoja mmoja wa Mashirika ya Bima au ya Hifadhi ya Jamii kama *NSSF* hasa hisa za moja kwa moja katika vitega uchumi vya mashirika hayo isipokuwa wanachama wananufaika na vitega uchumi hivyo kwa kupata mafao bora zaidi yanayotokana na faida inayozalishwa. Kimsingi, wanachama kwa ujumla wao ndio wamiliki wa vitega uchumi hivyo.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa uwepo wa haya mashirika kama BIMA na *NSSF* kunatokana na michango ya wananchi hawa na wakati huohuo haya mashirika moja ya kazi yanayofanya ni pamoja na kuwekeza katika vitega uchumi kama nyumba na vitega uchumi vinginevyo. Ni Kwanini basi Mashirika haya yasiendelee kuwa yanajenga vitega uchumi hivi kama nyumba na kuwakopesha wananchi wale watumishi ambao hasa ndiyo chanzo cha fedha hizo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli alivyosema Mheshimiwa Manyinyi ndiyo hasa dira ya mifuko kama ya *NSSF*. Shirika kama la Bima ya Taifa kama unavyojua kwa muda mrefu kutokana na mabadiriko ya sera na soko la Bima imekuwa iko katika matatizo makubwa lakini kwa upande wa Shirika la *NSSF* sera ya kujenga nyumba na kuwakopesha wale wananchama ipo ndiyo maana kuna nyumba maeneo kadhaa ikiwepo kule kwangu Ukonga Kinyelezi ambapo Shirika limejenga nyumba na kuwakopesha wanachama kadri faida inavyojitokeza Shirika linaangalia namna gani linaweza likajenga nyumba hizi. Lakini tujue kwamba wanaangalia vilevile Sera ya Uwekezaji kwa Ujumla na Sera ya Nyumba inaangalia vilevile na soko la wakati huo la nyumba. Kwa hiyo, kuna wakati wanakwenda kwenye nyumba za biashara lakini wakati mwingine wanajenga hizi nyumba kwa ajili ya kukopesha wafanyakazi. Tutaendelea kuwahimiza wenzetu wa *NSSF* waendelee utaratibu huu wa kujenga nyumba hasa za bei nafuu kwa ajili ya kuwakopesha wanachama.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri na yeye amekiri kwamba mashirika haya yameanzishwa kwa makusudi maalum. Kwa shirika kama BIMA na *NSSF* kuendelea kuwekeza kwenye majengo na kitu ambacho si rahisi kupata mapema wakati pesa zinahitajika. Je, haoni hata sasa *NSSF* kuendelea kuwekeza kwenye majengo badala ya kuwekeza kwenye kitega uchumi ambacho ni rahisi sana kurudisha pesa pale ambapo yatakiwa na kwa sababu hatuna wathamini kwa Tanzania wenye uwezo wa kuthaminisha mafao ya watu kwa miaka kumi ijayo?

Je, Waziri haoni sasa ni wakati wa kuishauri *NSSF* isiendelee kuwekeza kwenye majengo badala yake iwekeze kwenye miradi ambayo itarudisha mapema fedha kusudi iweze kukidhi malipo ya mafao kwa wananchi kwa wakati muafaka?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba, kama nilivyosema mwanzoni, katika mafao ambayo yanatolewa na Shirika kama la *NSSF*, kuna mafao ya muda mfupi na mafao ya muda mrefu; na katika kwekeza, Shirika linaangalia kwanza kwamba linao uwezo wa kulipa mafao yale anayoweza kujitokeza katika kipindi cha muda mfupi na kipindi cha muda mrefu na ndio maana wana uwekezaji wa kuwepo kwa mfano kwenye *Government Securities* au *Bond* ambazo zina-*mature* baada ya muda mfupi kwa ajili ya kulipa mafao yale yanayoweza kujitokeza kwa muda mfupi.

Lakini kwa muda mrefu wanajua vile vile kuna mafao yatachukua muda mrefu na ndio maana uwekezaji kwenye majengo vile vile unaangaliwa. Yote haya kwa kweli yanaangaliwa kitalaam wakijua kabisa kwamba haitafika muda wakashindwa kulipa kutokana na wao kufanya *investments* kama za majengo.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Kilasi na wote wanaosikiliza kwamba, utalaam wa kufanya *actuarial valuation* upo na unafanyika kabla ya uwekezaji haujafanyika kuweza kujua kwamba ni katika kipindi fulani, mahitaji ya kulipa mafao yatakuwa kiasi fulani na uwekezaji kwenye majengo hautaathiri malipo hayo ya mafao. Kwa hiyo, kwa kweli hili lisilete wasi wasi wowote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Devota! Aah, Mheshimiwa Waziri wa Kazi, majibu ya ziada!

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, unajua hii kuingiza huwa ina utalaam wake hii. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuongezea kidogo kwenye jibu zuri ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri amelitoa. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, ni kwamba uwekezaji wa Mashirika kama *NSSF*, si kwamba unajikita tu katika majengo. Kwa wakati muafaka tutampa Mheshimiwa Mbunge, mpangilio wa uwekezaji na atakuta sehemu inayowekezwa katika majengo katika shirika la *NSSF* ni sehemu ndogo sana.

Wamejikita katika kuwekeza katika maeneo ambayo yanalipa haraka zaidi na yenye faida kubwa zaidi na yenye uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile suala la *acturial* valuation kwa maana ya kupima mafao bora zaidi kwa ajili ya wafanyakazi, kutokana na maagizo ya Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* kwamba *actuarial evalution* ya kuangalia ufanisi wa Mfuko huo unafanywa na mtu anayeteuliwa na Shirika lenyewe la *ILO*. Mwaka jana kwa mfano *NSSF* waliletewa *Actuarial Evaluator* kutoka Canada. Na huyu alipokuja kufanya tathmini ya Mfuko huu alikuta mfuko huu hali yake ni nzuri sana na akashauri kwamba umefika wakati sasa vile vile *NSSF* kwa sababu ya ufanisi huu, wafiki

Hili limeshafanyika na *NSSF* wamepeleka mapendekezo yao kwenye Bodi na Bodi imepitisha. Tathimini hii huwa inafanyika kila baada ya miaka mitatu. Kwa hiyo,

Mfuko wa *NSSF* na Mifuko mingine kama hiyo inajitahidi sana kujali wanachama wao hasa kwa kushirikiana na miongozo ya Shirika la Kazi Duniani *(ILO). (Makofi)*

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *NSSF* inawekeza katika Mikoa mbali mbali hapa nchini kama vile Mwanza, Dar es salaam, Dodoma na kadhalika. Je, Serikali inaweza kuielekeza *NSSF* katika Bajeti ya mwaka huu ikawekeza katika Mkoa wa Ruvuma?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, tutawaeleza *NSSF* ili waangalie uwezekano kutegemea na *feasibility study* kama wanaweza kuwekeza katika Mkoa wa Ruvuma.

Na. 87

**Utaratibu wa Kulipia Huduma za Afya**

**MHE. DR. ALI TARAB ALI (K.n.y. MHE. SALIM HEMED KHAMIS)** aliuliza:-

Kwa kuwa Sera ya Afya ya nchi yetu inawataka wagonjwa kuchangia huduma za afya:-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwasaidia wagonjwa mahututi wanapofika hospitalini wakiwa hawana fedha za matibabu na pia hawamo katika Mfuko wa Afya ya Jamii?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimaudhui swali hili linafanana na swali Na.8 lililoulizwa na Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, na kujibiwa hapa Bungeni tarehe 27/01/2009. Ni kweli kwamba kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Afya ya mwaka 1990 na kama ilivyorusiwa mwaka 2007, huduma za afya ni za kuchangia. Hata hivyo, kwa kutambua kuwa huduma za afya ni haki ya msingi ya kila mtu, Serikali imeweka utaratibu maalum wa kutoa misamaha kwa makundi maalum kama ifuatavyo:-

- Watoto wenye umri chini ya miaka mitano.
- Wanawake wajawazito.
- Wazee wenye umri wa miaka 60 na kuendelea ambao wamethibitika kwamba hawana uwezo.

- Watu wote wa umri wowote ambao wanathibitisha kuwa hawana uwezo.
- Watu wenye magonjwa sugu kama vile saratani, kifua kikuu, ukoma na UKIMWI.
- Wagonjwa wote wanaofikishwa hospitalini wakiwa mahututi na wale ambao si mahututi lakini wasipopata huduma ya dharura maisha yao yanaweza kuwa hatarini.

Mheshimiwa Spika, utaratibu nilioutaja hapo juu unavihusu vituo vya kutolea huduma za afya vinavyomilikiwa na na Serikali na vile ambavyo vinapata ruzuku ya Serikali. Hata hivyo kwa kuzingatia Kanuni na maadili ya utoaji wa huduma za afya nchini, vituo vya watu binafasi vinatakiwa kutoa huduma kwa wagonjwa mahututi na wale ambao wanahitaji huduma ya dharura ili kuokoa maisha yao kabla ya madai ya malipo.Kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kutoa wito kwa watoa huduma za afya wote katika vituo vya Serikali na vile vya watu binafsi kuzingatia Kanuni na maadili ya utoaji wa huduma za afya ili kuhakikisha kila anayehitaji huduma ya afya anaipata bila vikwazo. Aidha, nawaomba Waheshimiwa Wabunge kwa kushirina na Halmashauri zenu, kuhakikisha kuwa wananchi wanahamasishwa na Mfuko wa Afya ya Jamii ili kuwawezesha kupata huduma za afya kwa uhakika.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante! Ni kweli kwa nadharia kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, watoto wadogo chini ya umri wa miaka mitano na wajawazito wanatakikana wapate matibabu bure, wapate huduma bure. Lakini ni kwa uhakika na kwa ukweli kabisa, makundi hayo hayapati matibabu hayapati huduma bure. *(Makofi)*

Je, ni lini nadharia itakwenda sambamba na ukweli kwamba watoto wadogo chini ya umri wa miaka mitano na wajawazito wapate huduma hospitali bure? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, *observations* ambazo anazifanya Mheshimiwa Mbunge ni sahihi, ni sahihi katika maana ya kwamba utaratibu uliokuwa unatumika katika Wizara ya Afya na katika Halmashauri mbali mbali, umekuwa ni ule wa kupeleka *kit*, na *kit* ile haiangalii mahitaji halisi ya kituo kile cha afya au zahanati au hospitali inayohusika. Sasa hivi Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Halmashauri, imeanzisha kitu kinachoitwa *integrated logistical systems* ambayo imeanzishwa katika nchi nzima, ukiacha Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Kigoma.

Utaratibu huu ni utaratibu ambao una hakikisha kwamba dawa zinazopelekwa na vifaa vinavyopelekwa katika kituo kinachohusika ni zile ambazo ziko katika mahitaji yao. Na kupitia utaratibu huo tunaamini kwamba hao wananchi ambao wanapata matatizo hayo matatizoyatakuwa yamekwisha hilo la kwanza.

Lakini la pili Mheshimiwa Spika, nikweli kabisa kwamba sera yetu ni kwamba mama mjamzito akienda hospitali au watoto wenye umri wa miaka 5 kwenda chini, wale wanatakiwa wapate huduma ile bure ndio utaratibu na ndio sera iliyozungumzwa pale.

Nchi hii inatamka katika katiba ya Nchi kwamba ni Nchi ya vyama vingi ambavyo inafuata siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Na ndani yake ndio tunazungumza habari hii ya kwamba huduma hizi zitolewe na zinatolewa bure hata kwa wenye kifua kikuu ukoma na kadhalika na kadhalika.

Kwa hiyo, ninaamini kwamba kwa kutumia huu utaratibu ambao nimeusema hapa tatizo hili litakuwa limeondoka.

**SPIKA:** Nitachukua mmoja wa Upinzani na mmoja wa CCM, Mheshimiwa Arfi halafu Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. SAID A. ARFI**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kutokana na majibu ya mheshimiwa Waziri nataka anieleze kwa nini na kwa sababu gani Mkoa wa Tabora na Kigoma umebaguliwa katika mpango huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimwa Said Arfi, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, nilichokuwa nazungumzia hapa nazungumzia mchakato. Nazungumzia kwamba wakati tulipoanzisha hiyo *Integrated Logistical Systems* haikuanza mara moja kwa nchi nzima. Ilikuwa inakwenda Halmashauri moja moja zilikuwa zinakuja na kwa maana ya kutoa hii ripoti ninayoitoa hapa mikoa ambayo imebakia yaani ambayo ipo katika mchakato ili nayo ikamilishe ni mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Tabora ndicho nilichokuwa namaanisha hapa sio kwamba wamebaguliwa.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa kwa utaratibu wa kuagiza madawa *Indent System* inayotumika sasa kila Mganga wa Zahanati kituo cha Afya inaagiza madawa kulingana na mahitaji ya kituo chake. Na kwakuwa *package* ya madawa inafanyika *MSD.* Je, Mheshimiwa Naibu Waziri unafahamu kwamba madawa ambayo wanapack katika masanduku katika ule mpango wa *research brass program* madawa ambayo wanaomba waganga yapelekwe kwenye vituo vya Afya na Zahanati hayatoshelezi kabisa kulingana na Bajeti inayotengwa pale *MSD?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la nyongeza la mheshimiwa Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nataka nimhakikishie kwamba nafahamu. Ninafahamu kwamba dawa zinazokwenda pale ni kidogo ukilinganisha na kiasi cha

mahitaji yaliyopo katika maeneo yale. Lakini sasa hivi tukubali kwamba masuala ya *MSD* na namna tunavyoagiza dawa mpaka sasa hivi yamekuwa na matatizo ndio maana tumeleta huo utaratibu wa *ILS.* Utaratibu huu ndio utaratibu ambao utaondoa matatizo yote haya ambayo tunayazungumza hapa. Lakini *the bottom line is* kwamba huduma yoyote inayotolewa katika nchi hii itategemeana na uwezo. Na Mheshimiwa Lubeleje anachozungumza hapa anazungumza kwamba madawa yale hayatoshelezi.

Ni mpaka tutakapofika mahali ambapo tutakuwa na uchumi mkubwa ambao unaweza ukabeba majukumu mengi makubwa hayo ndipo unapoweza kuondokana na tatizo kama hili. Kwa hiyo, nakubaliana na wewe kabisa kwamba kuna hilo tatizo la kwamba dawa zinazopelekwa kule hazitoshelezi.

Lakini tunafanya kile tunachoweza kufanya Mheshimiwa Spika, kuhakikisha kwamba tunaondokana na jambo hili. Nafanya hivyo na nasema hivyo nikitambua kwamba hapa tunazungumza habari ya maisha ya watu. Wala sio jambo la mchezo mchezo. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mhehsimiwa Lubeleje kwamba tutafanya tukishirikiana na halmashauri kuhakikisha kwamba tatizo hili la dawa kwamba zinakuwa chache linaondoka.

Na. 88

**Utunzaji wa Watoto Wanaozaliwa Katika Magereza**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wako wanawake wanaofungwa magerezani wakiwa wajawazito na hivyo kujifungua wakiwa bado wafungwa; na kwa kuwa gerezani hakuna uhakika kwa kupata chakula bora na maziwa ya kutosha kwa ajili ya mtoto na kwamba ikiwa mtoto akichukuliwa na ndugu wa mama yake, atakosa maziwa ya mama na kuweza kupata utapiamlo:-

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kuwa watoto hao wanapata chakula bora, maziwa ya mama na huduma bora za afya?

(b) Je, Serikali haioni kwa mtoto kubaki gerezani na mama yake ni sawa na kumfanya mtoto huyo kuwa mfungwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Magereza *(The Prisons Act, 1967)* kifungu 66(3), inaelekeza kwamba watoto wanaozaliwa katika magereza wapate huduma zote muhimu ikiwa ni pamoja na chakula bora, mavazi na huduma bora za afya kwa gharama ya Serikali. Aidha, watoto hao hunyonyeshwa maziwa na mama zao kwa kipindi chote ambacho mama zao wanatumikia kifungo chao gerezani.

(b) Mtoto anayenyonya kubaki gerezani ni kulinda haki ya mtoto kunyonya maziwa ya mama yake kwa kipindi chote kinachokubalika kama inavyoelekezwa katika mikataba mbali mbali ya kimataifa ambayo Serikali yetu imeridhia inayohusu haki ya mtoto na wala si kumfanya mtoto huyo kuwa mfungwa.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ina nia ya kulinda haki za mtoto, na kupunguza vifo vya wajawazito. Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kujenga Gereza la Wajawazito pamoja na wale walio na watoto wachanga ili watoto hao wawe huru na kuepukana na maambukizo mbalimbali na maradhi ya mlipuko?.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Kwa hakika, hali tuliyonayo sasa hivi hatuna ripoti yoyote ya kuonyesha kwamba kuna msongamano wowote upande wa Magereza ya akina mama. Na pili kusema kweli kama Wabunge wanavyofahamu jitihada zinafanyika katika Serikali kuhakikisha kwamba wale watoto ambao wanazaliwa wakati mama zao wakiwa magerezani kila kitu kinafanyika kuhakikisha kwamba hali zao, vyakula vyao na kuvaa kwao kunakuwa salama.

Kwa hiyo, kwa mantiki hiyo hali ilivyo sasa hivi na ukitazama hasa hali tuliyonayo ya kifedha kawa sababu tunao msongamano wa magereza hasa upande wa wanaume katika Taifa letu, katika Tanzania nzima. Kwa hiyo, niseme kwamba Serikali haitokuwa katika nafasi sasa hivi kwamba inaweza ikajenga magereza maalum ya akina mama wajawazito.

Lakini pili, niseme kwamba mama ambao ni wajawazito ambao wako magerezani idadi yao ni ndogo sana kwa sababu hapa tunazungumzia katika Tanzania wakina mama ambao wamefungwa ambao wapo na watoto wako magerezani hesabu yao wanakuja kama 15 ahsante sana.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kucheza ni haki ya mtoto, na mtoto anapoanzia umri wa miaka 6 basi anaanza kujifunza kucheza na kuendelea mbele kutembea.

Je, mtoto huyo amewekewa mazingira gani katika eneo hilo la gereza ya kumfanya aweze kucheza akiwa huru na ili asiweze kupata matatizo mengine ambayo yanaweza kujitokeza dhidi yake na chini ya uangalizi wa mama yake? Ahsante!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Hakika tunatambua kwamba mtoto ana haki ya kucheza, ni haki yake ya msingi. Lakini pia itambulikane kwamba mama yake anakuwa yuko hatiani. Kwa hiyo, sheria inachukua mkondo wake.

Lakini niliarifu Bunge lako Tukufu Mheshimiwa spika, kwamba vipo vipengele ambavyo vinamruhusu kabisa kwa idhini ya mama mtoto anaweza akalelewa na jamaa wa mama ambaye yuko katika kifungo. Anaweza akalelewa nje ya gereza.

Lakini pia tumetengeneza mazingira ndani ya gereza kwamba mtoto kama hana mtu wa kumchukua na kama mama yake hakutoa idhini kwamba yule mtoto anaweza kulelewa nje ya gereza, basi zipo nafasi kabisa za mtoto yule kusoma kwa mfano, nje ya gereza lakini anarejea anakuwa na mama yake ndani ya gereza.

Ni hali ambayo iko tete na ni hali ambayo iko dunia nzima lakini inakwenda kwa sababu hali ndivyo ilivyo. Mama yake anakuwa yuko katika kifungo lakini endapo mama yake anaridhia basi, kwa hakika yule mtoto anaweza akawa nje ya gereza wakati mama yake anaendelea na hukumu yake ambayo imemkabili katika kipindi kile. *(Makofi)*

Na. 89

**Uhaba wa Askari Polisi na Vitendea Kazi Kasulu**

**MHE. FELIX N. KIJIKO (K.n.y. MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Kasulu yenye wakaazi 760,000 ina uhaba mkubwa wa Askari Polisi wa doria kukabili matukio ya uhalifu vijijini na mpakani na nchi za jirani:-

(a) Je, ni kwa nini maeneo yenye matatizo na mipaka tele kama Kasulu yasipewe kipaumbele *(Priority in Police Allocation)*?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kukiongezea majengo pamoja na nyumba za askari katika kituo cha Polisi cha Heru Ushingo na kukipatia gari la doria?

(c) Je, ni lini Serikali itaandaa sera na kuleta sheria hapa Bungeni ili hoja nzima ya ulinzi shirikishi isimamiwe kisheria?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limekuwa likijitahidi kuimarisha ulinzi katika Mikoa na maeneo ya mipaka tete ikiwemo Wilaya ya Kasulu. Tumekuwa na uhaba mkubwa wa Bajeti ambayo imeathiri sana upatikanani wa vitendea kazi. Wizara yangu imelitamka hili bayana kwamba suala zima la Ulinzi na amani katika Taifa letu lipewe kipaumbele.

Pia ni ukweli usiopingika kwamba idadi ya Polisi haitoshi kukidhi mahitaji yetu kama Taifa. Masuala yote haya yanapewa mtizamo mpya katika zoezi zima la maboresho ya Jeshi letu la Taifa. Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi litatoa kipaumbele cha kuongeza idadi ya askari katika maeneo yenye matatizo na mipaka tete kama Kasulu kadri idadi ya Askari Polisi itakavyoongezeka.

(b)Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kujenga majengo katika kituo cha Polisi Heru Ushingo. Hii siyo kwa sababu ya kutokuwa na dhamira au nia. Hili ni tatizo la nchi nzima. Tunajitahidi kulitatua awamu kwa awamu tukitegemea kupatikana kwa fedha. Kuhusu gari la doria tatizo letu la uhaba wa fedha linafanyika utekelezaji wake kuwa mgumu. Askari waliopo katika kituo hicho wataendelea kuishi katika nyumba mbili zilizopo ambazo zinachukua familia 4 wakati serikali inaendelea kutafuta fedha.

(c)Mheshimiwa Spika, Ulinzi Shirikishi ni ushirikiano wa Jeshi la Polisi na Jamii kufanya kazi kwa pamoja, kwa kupanga mikakati na kutafuta njia sahihi na endelevu za kudumisha usalama wa watu na mali zao ili kuleta amani na utulivi katika jamii. Huu ni mkakati mpya wa utendaji wa Jeshi la Polisi wenye lengo la kuweka mazingira ya ushirikiano wa dhati baina ya wananchi na Jeshi la Polisi. Wizara ipo kwenye mchakato wa kuunda sera ya Usalama wa Raia ambapo Ulinzi Shirikishi ni miongoni mwa mikakati ya kutekeleza sera hiyo. Mchakato huu utakamilika katika mwaka wa fedha 2009/2010.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri ambayo Naibu Waziri ameyatoa; na kwa kuwa wananchi wa mkoa wa Kigoma ambao umekuwa na wakimbizi kwa kipindi kirefu na sasa zoezi la *repatriation* limefikia mwisho kwamba wakimbizi wanaondoka, na kwa kuwa katika kipindi hicho wananchi wa Mkoa wa Kigoma wamekuwa wakishuhudia wingi wa askari Polisi ambao wamekuwa wakifanya ulinzi kwa kutumia silaha katika Mkoa mzima kutokana na wingi wa makambi uliokuwa huko. Sasa mwananchi wa Kigoma unamdhibitishia usalama wake kimaisha vipi kwa sababu *repatriation* imeshamalizika?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli zoezi zima la kuwarejesha wakimbizi nchi ambazo wametoka linaendelea na linakwenda vizuri. Lakini basi hiyo isiwe sababu ya kusema kwamba kwa kuwa zoezi zima la kuwarejesha wakimbizi basi litafanya kwamba ile hali ya ulinzi na usalama katika mkoa wa Kigoma itakuwa lisipewe kiupambele. Hata hivyo hivi sasa tuko katika jitihada kwa sababu mbali ya wimbi wa wakimbizi wako wanyang'anyi na majambazi ambao wanatoka Kongo na wanakuja katika sehemu yetu na sasa hivi tuko katika *operation* ya kupambana nao. Kwa hiyo, ningeomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kuondoka kwa wakimbizi kuwarejesha majumbani haina maana kwamba Serikali haitokuwa na mikakati maalum ya kuhakikisha ulinzi na Uslama katika Mkoa wa Kigoma unakuwepo. Lakini kubwa zaidi ni kuzingatia kwamba Mkoa wa Kigoma ni Mkoa wa pembezoni na ni Mkoa ambao nchi yetu imekuwa ikikabiliana na nchi mbalimbali. Kwa hiyo suala la ulinzi na usalama ni suala ambalo ni la muhimu na

ningeomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalitazama kwa umakini sana na inaongeza juhudi na nguvu kuhakikisha kwamba usalama wa raia unakuwepo.

Na. 90

***Medical Store Department (MSD)* Kutotoa Hesabu Ya Matumizi**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwakuwa, fedha zote za Serikali huwa zinasitishwa ifikapo tarehe 30 Juni, kila mwaka, na kwa kuwa, Serikali hutoa fedha kwenda *Medical Stores Department (MSD)* ili Halmashauri na Manispaa zitumie kupata dawa:-

(a) Je, kwa nini *MSD* haitoi hesabu ya mapato na mabaki ya dawa kwa Halmashauri husika?

(b) Je, kwa fedha zinazobaki zinaweza kutumika tena kwa mwaka unaofuata?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** (**MHE. OMAR YUSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mhe. Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Utaratibu unaotumiwa na *MSD* ni kufungua akaunti kwa kila mteja yaani kila kituo cha Afya, Hospitali na Zahanati. Akaunti hiyo, huonyesha kiasi cha fedha alizonazo mteja mwanzoni mwa mwaka wa fedha na kiasi cha fedha mteja anachowekewa katika mwaka wa fedha unaofuata. Aidha, katika hesabu za mteja huonyesha pia thamani ya dawa alizopewa na salio la fedha au deni alilonalo.

Hivyo, Halmashauri zinaweza kupata taarifa ya matumizi na salio la fedha za vituo vyake kutoka *MSD* wakati wowote zinapohitajika.

Kadhalika, Hospitali za Wilaya, Mikoa, Rufaa hupaswa kupewa taarifa za mapato na matumizi katika akaunti zao kila mwezi, wakati zahanati na vituo vya afya hupata taarifa hizo kila baada ya miezi mitatu. Kama zipo Halmshauri ambazo hazipati taarifa hizo, wanaweza kuziomba kutoka *MSD* na ni haki yao kupewa.

(b) Mheshimiwa Spika, Fedha zinazobaki *MSD* katika akaunti ya zahanati, vituo vya afya na hospitali, hutumika kwa ununuzi wa dawa na vifaa katika mwaka wa fedha unaofuata. Hivyo, fedha hizo husaidia kupunguza uhaba wa dawa na vifaa wakati wa kipindi cha bajeti.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize maswali madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza na-*declare interest* kwamba mimi ni mjumbe wa kamati ya *LAAC.* Kwa hiyo, swali langu niliuliza nina, uhakika nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halmashauri nyingi zimekuwa hazipati taarifa ya fedha zinazokwenda kwenye halmashauri zao kwa kipindi kirefu sana. Husababisha kwamba wao pia hawana taarifa za kuweza kujaza kwenye mahesabu yao.

Lakini la pili, Halmashauri nyingi na mansipaa zake huchelewesha kupata fedha kwa wakati muafaka, na kusababisha kwamba inapofika mwaka mwingine wa fedha hushindwa kufanya Bajeti kwa kupitia Wizara ya afya au kupitia *MSD* kutokana na kwamba fedha zile hazipo na kuna kusabisha upungufu mkubwa wa dawa na vitendea kazi kwenye maeneo husika.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, nilisema katika jibu langu la msingi kwamba utaratibu ni kwa Halmashauri kupata taarifa za hesabu za vituo vyao, lakini nikasema vile vile kama zipo Halmashauri ambazo hazipati hizo taarifa hii ni haki yao ya msingi waiombe *MSD* na *MSD* wanahaki ya kuwapa haraka iwezekanavyo, nawashauri Waheshimiwa Wabunge waliomo katika Halmashauri hizo watumie fursa hii.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nimesema kwamba kwa Halmshauri au vituo ambavyo wanakuwa na mabaki ya fedha na fedha zile zinatumika kuweza kununulia dawa mwaka unaofuata kwa sababu mara nyingi fedha huchelewa katika mwaka unaofuata na hivyo kusababisha kuwa na upungufu wa madawa.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo ni mfuko ni msingi kama alivyosema Mheshimiwa Mwanri kwamba sote tunakubali kwamba kunakuwa na upungufu wa madawa katika vituo vyetu lakini hili linatokana na kwamba hali duni ya fedha tunazozitoa katika vituo vyetu vya afya. Hali ya uchumi itakapoimarika basi vituo vyetu vya afya vitakuwa na fedha za kutosha ili na wao waweze kupata dawa za kutosha katika muda wa mwaka mzima.

Na. 91

**Malalamiko Juu ya Mfumo wa Manunuzi**

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa mfumo wa manunuzi unalalamikiwa sana na unatoa nafasi ya ufisadi kwani hauko wazi.

Je, Serikali inasemaje kuhusu kuboresha mfumo huo ili kuondokana na malalamiko hayo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa fedha na Uchumi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakar Faki, Mbunge wa Ole, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya ununuzi wa umma sura ya 410 imeweka mfumo wa ununuzi wa umma ambao unasimamia misingi mikubwa mitatu iliyoainishwa chini ya Kifungu 43 cha Sheria hiyo ambayo ni kama ifuatavyo. Kwanza, haki na usawa kwa kuzingatia vigezo vya tathmini visivyobagua na kuweka utaratibu uliowazi wa kushughulikia malalamiko.

Pili thamani inayolingana na ubora kwa kuhakikisha kwamba taasisi za ununuzi zinapata vifaa pamoja na huduma bora kwa kuweka utaratibu mzuri wa kusimamia mikataba na vifaa pamoja na kupunguza gharama za kushughulikia zabuni. Tatu, kutoa nafasi kwa wote kushiriki zabuni kwa kuweka ushindani, matangazo ya kutosha ya zabuni na masharti rahisi ya zabuni.

Mheshimiwa Spika, wenye jukumu la kusimamia utekelezaji wa sheria ya ununuzi wa umma ipasavyo ni wale ambao wamepewa dhamana kusimamia matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaliangalia suala zima la kuboresha mfumo wa manunuzi nchini ikiwa ni pamoja na kuwasilisha Bungeni marekebisho ya sheria ya ununuzi wa umma. Marekebisho ambayo yataipa mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa umma uwezo wa kutoa maelekezo kwa mamlaka zenye dhamana kwa kuwachukulia hatua watakaokiuka sheria. Aidha, watakuwa na uwezo wa kusitisha zabuni yoyote pale itakapobainika kuwepo kwa ukiukwaji wa Sheria na Kanuni zinazosimamia ununuzi wa umma, pamoja na kutoa adhabu kwa wale wanaobainika kukiuka sheria na Kanuni za Ununuzi wa umma.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa mchakato mzima wa ununuzi wa rada ya Serikali unalalamikiwa hadi leo hii kwamba ulikuwa na dalili za ufisadi, Je, utaratibu wa manunuzi ya umma katika utaratibu mzima wa ununuzi wa *Radar* hii ulizingatiwa?

(ii) Kwa kuwa mradi wa vitambulisho umechukua muda mrefu kutekelezwa tokea pale sheria yake ilipopitishwa na Bunge mwaka 1987 ambapo kama sheria ya manunuzi ingetekelezwa kikamilifu vitambulisho vingekuwa tayari vinatumika.

Je, ni maeneo gani ya sheria ya manunuzi yaliyovunjwa hata mradi huo ukachukua muda mrefu kiasi hicho?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kuhusu *Rader* ni suala ambalo lipo katika mchakato wa uchunguzi na isingefaa kutoa jibu hapa, vivyohivyo kuhusu hili jingine ndiyo kabisa bado jipya kabisa na hata halijafika mwisho bado ni mchakato wa zabuni, Bunge haliwezi kuingilia mchakato wa zabuni wakati unaendelea.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea hayo nimeyatupilia mbali.

**MHE. MWADIN ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Naibu Waziri ameliambia Bunge lako Tukufu kwamba wanaangalia namna bora ya kuboresha mfumo wa manunuzi ya umma, ikiwa ni pamoja na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria. Tunafahamu kwamba utaratibu wa kutumia *electronic procurement* kwa kiwango kikubwa unaweza kupunguza ufisadi katika manunuzi ya umma.

Je, Serikali ipo tayari sasa kufikiria mpango huu na kuuleta katika Muswada wa sheria ambao utaletwa Bungeni?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika**,** suala la *electronic procurement* Serikali tunaliangalia kwa undani zaidi na utekelezaji wake kwa sehemu kubwa tumeshalianza, nataka nieleze tu kwamba hii *procurement* ina sehemu kuu tatu.

Sehemu ya kwanza ni mamlaka kuwa na mtandao, mamlaka ya manunuzi kuwa na mtandao ambao wataweza kuweka zile taarifa ya zabuni mbalimbali katika sehemu mbalimbali ya taasisi zetu, hilo tayari mamlaka ya udhibiti tayari wameshakuwa na mtandao huo na wakati wowote kila ambaye atahitaji kuangalia ataweza kuangalia.

Mheshimiwa Spika, lakini sehemu ya pili ni kwa Wizara zetu na taasisi kuwa na mitandao ambao wao wataweza kupeleka zile information zao kwenye mamlaka ya udhibiti, sehemu kubwa ya taasisi zetu bado hawana mitandao kwa hivyo nao vile vile tunawaharakisha wawe na hiyo mitandao ambao wataweza kupeleka zile taarifa zao katika mamlaka ya udhibiti.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ni kwa wale ambao wanataka kununua au kutuuzia zile bidhaa au huduma ambazo tumezitaja, hawa ni wafanya biashara, wengi hawana mitandao, hasa tukizingatia kwamba tunataka vilevile kuwalinda wale

wafanyabiashara wadogowadogo kwa hivyo eneo hili tunaliangalia kwa undani kabisa na sehemu zote tatu zitakapokamilika Serikali itakuwa haina kipingamizi katika kutumia *electronic procurement*

Na. 92

**Kuendeleza sekta ya Biashara ndogo ili Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kati ya vipaumbele vya Serikali ni pamoja na uboreshaji wa fursa za upatikanaji wa mitaji kwa biashara ndogo na za kati (*SMEs*):-

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani katika kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa kuendeleza sekta ya Biashara ndogo na za kati?

(b) Je, utaratibu wa uanzishwaji wa mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi *(Mwananchi Economic Empowerment Fund*) umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo ina mchango mkubwa katika upatikanaji wa ajira na kukua kwa pato la Taifa. Kwa kutambua umuhimu wa sekta hii, Serikali imekuwa ikiendelea kubuni na kutekeleza sera na programu mbalimbali zenye kusaidia maendeleo ya sekta hii. Kwa mfano, sera ya maendeleo ya viwanda vidogo na biashara ndogo (2003) inalenga kuchochea ukuaji wa shughuli za sekta hiyo kwa kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara, kuimarisha asasi na taarisi zinazohudumia sekta hii.

Mehsimiwa Spika, katika kundi la taasisi za Umma, Serikali imeelekeza nguvu zake zaidi kulijengea uwezo shirika la kuhudumia viwanda vidogo (*SIDO*), ili liendelee kutoa huduma mbalimbali kwa sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo. Hali kadhalika kwa kupitia shirika hilo, asasi mbalimbali za kuhudumia sekta ndogondogo *(*VIBINDO*), Tanzania Food Procesor Association (TAFOPA), Tanzania Women Miners Association (TAWOMA), Hand Craft of Tanzania (HOT) na Women Chember of Commerce* zimeweza kujengewa uwezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inaunga mkono kazi nzuri inayofanywa na *PRIDE* taasisi ambayo hadi sasa tangu ilipoanzishwa imeshatoa mikopo ya shilingi bilioni 241.6 kwa wananchi laki saba, isitoshe Mheshimiwa Rais Mwenyewe kwa kuona

umuhimu wa jambo hili amebuni mfuko maarufu uitwao Kikwete *Fund* ambao nao umetoa mikopo kwa wananchi ili kuendeleza sekta ndogo.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa wajasiriamali wanazalisha bidhaa zenye ushindani, Serikali imekuwa ikijenga uwezo wa Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) ili kuhakikisha ubora wa bidhaa zao ili ziweze kushindana katika masoko ya ndani na nje.

(c) Mhehsimiwa Spika, Serikali ilianzisha Mfuko wa Uwezeshaji wananchi (*Mwananchi Economic Empoerment Fund)* mwezi Januari, 2008. Madhumuni makuu ya mfuko huu ni kuwawezesha wananchi kupata mitaji na mikopo ambayo itawawezesha kushirika kikamilifu katika kujenga uchumi wa nchi yao. Kwa kutumia mfuko huu, wafanyabiashara wadogo na wa kati (*SMEs*) wanapata fursa ya kukopa fedha.

Mheshimiwa Spika, mfuko wa uwezeshaji ulianzishwa kwa mtaji wa shilingi milioni 400 kutoka kwenye Bajeti ya matumizi ya kawaida ya Baraza la Uwekezaji Wananchi Kiuchumi, hata hivyo, kiasi hiki ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji ya mikopo ya wafanyabiashara ndogo na za kati. Kwa mantiki hiyo Serikali ikaona ni vema ikaanza kutoa mikopo katika mikoa mitano na hatimayekuusambaza mfuko huu katika mikoa mingine kadri mtaji utakavyokuwa unaongezeka. Mikoa iliyochaguliwa katika awamu ya kwanza ni Lindi, Mtwara, Manyara, Singida, na Rukwa. Mpaka sasa mikopo yenye thamani ya jumla ya shilingi 143,770,000 imetolewa kwa wafanyabiashara wadogowadogo na wa kati katika mikoa ya Lindi na Mtwara.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja tu la nyongeza, kwa kuwa taarifa za mfuko huu wa mwananchi *economic empowerment fund* bado hazipo katika Wilaya mbalimbali na Mikoa mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Kongwa na Naibu Waziri ameeleza kwamba fungu lililotolewa kwa Taifa zima kwa mfuko huu ni shilingi milioni 400 ambazo ni mtaji chini ya kile kinachotolewa na *SACCOS* ya Kibaigwa kwa Kata ya Kibaigwa, lakini hela hii milioni 400 ndiyo inatolewa kwa Taifa zima.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka kiwango cha fedha cha maana katika mfuko huu ili wananchi waweze kufaidika kwa kukopa ili waimarishe sekta ya biashara ndogo na za kati?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kuna uwezekano mkubwa kabisa kwamba taarifa za mwananchi za *empowerment fund* hazijafika katika baadhi ya Wilaya na hii inatokana na aina yenyewe ya mfuko ambao umelenga kuanza kutekelezwa katika mikoa mitano na kama ilivyopangwa ni kama Mkoa wa Dodoma sio mmojawapo kwa hiyo inawezekana kwa sababu mikoa iliyolengwa Dodoma siyo mmojawapo ndiyo maana labda taarifa hizo hazijafika katika eneo la Kongwa.

Tunachopenda  kusema tu ni kwamba kadi tunavyopanua idadi ya mikoa Mkoa wa Dodoma ukiwepo basi taarifa hizi zinakuwa zinafika kwa walengwa kwa sababu

itasaidia zaidi  zaidi ukimpa mtu taarifa hapo hapo na bado akaweza akapata fedha kulipo kumpa taarifa halafu akawa anangojea na hajapata fedha yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kukubaliana na Mheshimiwa Ndugai kwamba kweli mfuko huu ni mdogo na nimesema kwenye jibu la swali la msingi hautoshelezi mahitaji ya wananchi naomba Mheshimiwa Ndugai na Waheshimiwa Wabunge watambue mifuko mingine ambayo nimeitaja kwamba nayo imelenga katika kumwezesha mwananchi lakini kadri ya uwezo utakavyokuwa umeboreka napenda kuwaahidi kwamba Serikali itaupanua mfuko huu ili wananchi wengi zaidi waweze kupata mikopo.

Na. 93

**Uzalishaji wa Zao la Katani nchini.**

**MHE. PARMUKH SIGHN HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania ni mojawapo ya nchi zinazozalisha katani kwa wingi na kwama wakati wa nyuma nchi yetu ilipata pato kubwa kutokana na zao hilo halizalishwi ipasavyo:-

(a) Je, ni kwa nini zao la katani linashindwa kushindana kwa ufanisi katika soko la dunia?

(b) Je, ni bidhaa gani zinazotokana na zao hilo?

(c) Je, ni nchi ngapi duniani zinazalisha zao hilo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Tanzania ni mojawapo ya nchi zinazozalisha katani kwa wingi. Pili kushindwa kushindana kwa zao la katani kwa ufanisi katika soko la dunia kumechangiwa na sababu nyingi, na baadhi yake ni:-

(i) Usimamizi mbaya wa mashamba ya katani baada ya mashamba hayo kuchukuliwa na Serikali uliosababisha baadhi ya mashamba kutotunzwa, kuchomwa moto na wanavijiji kuyavamia.

(ii) Kushindwa kuwapata wafanyakazi wa kutosha kuyatunza mashamba hayo.

(iii) Kuendelea kutumia mashine za kizamani, ukarabati duni na ubovu wa miundombinu kwa ujumla.

(iv) Watumiaji wa nyuzi za katani kuanza kutumia nyuzi mbadala za bandia (*synthetics*) ambazo gharama ya uzalishaji ni ndogo ikilinganishwa na katani na kwamba nyuzi hizo bandia zinaweza kuzalishwa wakati wowote.

(v) Kupanda kwa gharama za mafuta ya kuendeshea mitambo ya kutengeneza katani.

(vi)Ukosefu wa mitaji, utafiti na mbegu bora.

(b)Mheshimiwa Spika, kuna mazao mengi sana yanayoweza kupatikana kutokana na katani. Baadhi ya mazao hayo ni bidhaa za kufuma mazulia, magunia, maturubai, vitambaa, mapambo, vikapu, kamba, nyuzi na kadhalika, nishati jadilifu *biogas* kutokana na mabaki ya mkonge, karatasi maalum kwa ajili ya kutengeneza mifuko ya chai (*tea bags)* noti pamoja na *filters*; Chakula cha mifugo kutokana na mabaki ya mkonge kemikali za viwandani (*Ethanol and Inulin*); mbolea inayopatikana baada ya kuzalisha umeme; vifaa vya ujenzi(*absestors, vigae*); vifaa vya kupunguza joto katika mashine na mitambo, vinywaji vikali, mchanganyiko au *composite* inayotumika kwenye shughuli za ujenzi wa nyumba na viwanda vya magari, kuzalisha vifaa vya ndani ya gari kama (*dash board*) paa la ndani ya gari, *cover* za siti za magari na vitasa vya milango ya gari, kitambaa msasa *(buffing cloth*) kwa ajili ya kuunganisha chuma (*metal polishing*) kwenye viwanda vya chuma na *Geo-textile* inayoongoza kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa ardhi wakati wa kilimo na kwenye ujenzi wa barabara.

(c)Mheshimiwa Spika, nchi zinazozalisha katani kwa wingi ni pamoja na Brazil, Mexico, jamhuri ya watu wa China na Tanzania. Kwa mfano katika mwaka 2007 Brazil ilizalisha tani 175,000. Jamhuri ya watu wa China tani 55,000 na Tanzania tani 33,327.

**MHE. PARMUKH SIGHN HOOGAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, tatizo jingine kubwa la katani ni kushindana kwa aina ya katani na *jute* na nchi zinazozalisha *jute* hutoa ruzuku kwa wakulima wao.

Je, kwenye suala la katani Mheshimiwa Waziri yupo tayari kutoa ruzuku?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuungana nae kwamba upo ushindani mkubwa kati ya *Jute* na katani na kwamba pengine sababu ushindani huo ni ruzuku kwa wale wenzetu.

Mheshimiwa Spika, napenda niikariri nia ya Serikali ya kupenda kuisaidia sekta ya kilimo, sasa hivi Serikali imeanza kujikita katika kutoa ruzuku kwa mbolea kwa ajili ya mazao mbalimbali hasa yale ambayo ni ya chakula na ambayo tunayategemea sana, kinachozuia ruzuku kwenda kwa kila zao pamoja na mkonge ni uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nia ipo pale pale na ipo mipango mingi ambayo tunaweza tukaifanya kabla hata ya kutoa ruzuku kwa zao la katani kuweza kupanda chati na kuongezeka kiasi chake na kuongezeka thamani, Serikali itakapokuwa na uwezo zaidi basi na ruzuku kwa zao la katani litaangaliwa.

Na. 94

**Kuajiri Walimu Wastaafu kwa Shule za Msingi**

**MHE. SAID AMOUR ARFI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna upungufu mkubwa wa walimu katika shule za Sekondari na za msingi nchini; na kwamba hatua kadhaa zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kuajiri walimu wastaafu kwa shule za Sekondari.

Je, Serikali ipo tayari kutoa kibali cha kuajiri walimu wastaafu kwa shule za Msingi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vibali vya ajira ya mkataba hutolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma baada ya Mwajiri kuomba kibali kufuatana na mahitaji.

Mhehsimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa vibali kwa Walimu wastaafu wa shule za msingi baada ya kupokea maombi kutoka kwenye ofisi za Jiji, Manispaa na Halmashauri nchini. Mathalani katika mwaka 2007/2008 vibali vilivyotolewa vilikuwa ni 833 kwa ajili ya shule za msingi.

Hivyo Halmashauri zenye upungufu wa walimu wanashauriwa kuainisha mahitaji yao na kuomba kibali cha ajira ya mkataba kwa ajili ya wastaafu ambao wana sifa, afya njema na utayari wa kufanya kazi hiyo.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(a)Kwa kuwa mpango huu wa kuomba vibali kutoka Utumishi umekuwa ni wa siri na wenye urasimu sana na tatizo la upungufu wa walimu katika shule zetu za msingi linafahamika, ikiwa Wilaya ya Mpanda ina upungufu wa Walimu karibu 800 na wakati Serikali ilipoona umuhimu wa kuwa na walimu kwa ajili ya shule za Sekondari

waliostaafu walitoa matangazo na watu wakaomba nafasi hizo, kwanini Serikali inasita kutoa matangazo kwa walimu wenye sifa na wenye afya ili waweze kuomba nafasi za kufundisha kupunguza tatizo la walimu katika shule za msingi, Serikali itakuwa tayari kutangaza bayana kwamba walimu wenye sifa hizo wanaweza kuajiriwa?

(b) Kwa kuwa tatizo la upungufu wa walimu wa shule za msingi linafahamika na limewahi kufanyiwa majadiliano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilionyesha utayari wa kusaidia tatizo la upungufu wa walimu wa shule za msingi kwa sababu wana walimu wa kutosha kule Zanzibar, ni hatua gani zimechukuliwa mpaka sasa hivi ili angalau kusaidia kupunguza tatizo la walimu katika shule za msingi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, kuhusu walimu wastaafu kuomba nafasi si suala la usiri isipokuwa watarajiwa hawa au wastaafu wanapaswa kupeleka maombi yao kwenye Halmashauri ambazo wangependa kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kama inaonekana upo usiri tunaomba watuletee nakala za maombi yao Wizarani ili na sisi tuweze kufuatilia kwa karibu kwa sababu walimu shule za msingi wapo chini ya Halmashauri na Halmashauri ndizo zinazofahamu uhitaji wa walimu wao, naomba kusisitiza Wakurugenzi wakishirikiana na Maafisa Elimu wapokee maombi hayo kwa kadri ya mahitaji yao na wayalete haraka ili tuweze kupunguza uhaba mkubwa wa walimu uliopo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu ziada ya walimu waliopo Zanzibar kupangiwa kazi Tanzania Bara, tunaomba Walimu hao kama wanazo sifa waombe kwenye Halmashauri ambazo zina upungufu kwa sababu hata walimu wastaafu huomba kwenye Halmashauri zenye upungufu hivyo watakapoomba watafikiriwa kama walimu wengine au wale wastaafu.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna tatizo kubwa la uhaba wa walimu na katika shule nyingi za sekondari kuna watoto wenye ulemavu waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza, kama vile ulemavu wa macho. Kwa kuwa walimu hawapo kwenye shule hizo ambazo wanafunzi wamechaguliwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha sasa inapata walimu wanaoweza kufundisha watoto hawa wenye ulemavu hususan walemavu wa macho?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhaba wa walimu na hasa walimu wa elimu maalum, kwa maana walimu wanaofundisha wanafunzi wenye ulemavu wa aina mbalimbali. Kwa kuzingatia hilo tumekipanua Chuo cha Ualimu Patandi au tumekiongezea uwezo Chuo cha Ualimu Patandi ili kiweze kutoa idadi kubwa ya walimu. Pale ambapo kuna wanafunzi waliopelekwa kwenye shule ambazo hazina walimu naomba tupokee taarifa.

Mheshimiwa Spika, kwa Mheshimiwa Maneno nimempokelea taarifa yake jana akiniarifu ana wanafunzi 20 katika Sekondari ya Lugoba ambao wana ulemavu wa macho nimemwambia aniletee na mimi binafsi nimeshaagiza jana ile ile Wizarani kwangu waende Lugoba wakawatambue hao wanafunzi tutawapeleka kwenye shule ambazo zina Walimu.

Mheshimiwa Spika, tuko tayari kutekeleza ilani tuliyojiwekea sisi wenyewe. (*Makofi*)

Na. 95

**Kupeleka Umeme Arumeru Magharibi**

**MHE. ELISA D. MOLLEL** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imekuwa kitoa ahadi za mara kwa mara za kupeleka umeme katika vijiji vya Oldonyosambu, Timbolo, Sambasha, Oljoro, Likamba na Midawe tangu mwaka 1996

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi zake za kila mwaka kwa wananchi wa Arumeru Magharibi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, Kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Elisa David Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ilitoa ahadi ya kupeleka umeme katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge wakati Wizara yangu ikijibu swali hapa Bungeni tarehe 14 Februari, 2008. Wakati huo nilimweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba miradi hii ilikuwa imepangiwa utekelezaji chini ya programu ya kufikisha huduma ya umeme vijijini *Electricity Rural Transfomation* (*ERT*) mpango ambao baadaye ulisitishwa na kufuatiwa na mradi wa *electricity IV*, *Phase II*.

Vijiji vya Oldonyosambu, Timbolo, Sambasha na Oljoro vilipangiwa utekelezaji kulingana na fedha kadri ambavyo zingepatikana. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa lengo la Serikali ni kufikisha umeme kwa wananchi wengi zaidi, hususan wananchi wanaoishi vijijini kwa ajili ya kuhakikisha maendeleo.

Mheshimiwa Spika, eneo la Arumeru Magharibi linapata umeme wa *grid* kutoka *Unga Limited, Mount Meru* na Njiro. Hivyo kufanya mipango ya kupeleka umeme maeneo ya vijiji vya Arumeru kuwa rahisi. Njia ya umeme kutokea *Unga Limited* mpaka

Oldonyosambu Jeshini imeyapatia umeme maeneo ya Arumeru Magharibi kama ifuatavyo:-

Eneo la Ngaramtoni, Mtoni, Campasi ya Chuo Kikuu cha Sokoine, Chuo cha Misitu Olmotonyi na kituo cha habari Maalum. Laini nyingine ya umeme kutoka *Mount Meru* imepeleka umeme idara ya Maji Midawe, ambapo ni mbele ya kijiji cha Midawe.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elisa David Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa kijiji cha Midawe kiko kwenye hatua za mwisho za kupatiwa umeme baada ya kijiji hicho kufaidika na mradi wa umeme uliogharamiwa na Mamlaka ya Maji *Arusha Urburn and Sewerage Authority* (*AUWSA*).

Mradi huo unapeleka umeme katika kijiji hicho kutoka katika kituo cha kupozea umeme cha *Mount* Meru. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwaka 2006 na unatarajiwa kukamilika Julai, 2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kimsingi vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge ukiondoa kijiji cha Midawe, viko chini ya mpango wa umeme vijijini, lengo la Serikali ni kufikisha umeme kwa vijiji vyote nchini vikiwemo hivyo vilitajwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

Kama tulivyoeleza hapa Bungeni mwaka jana wakati tunajibu swali lililohusu upelekaji umeme vijiji vya Arumeru, narudia kusema Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, tunamwahidi Mheshimiwa Mbunge kukabidhi suala hili wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) mara tu tathmini za gharama husika zitakapokuwa zimekamilika, tunaendelea kulifanyia kazi.

Aidha, kwa kuwa mara kwa mara tunakabidhi mambo haya *REA*, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge atufanyie subira wakati tukikamilisha nmiradi hii na mingine kulingana na kuimarika kwa hali ya kifedha na uwezo wa kiutekelezaji wa *REA* yenyewe na *TANESCO* kama mtekelezaji.

**MHE. ELISA D. MOLELL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa vifaa vya mradi wa umeme wa Midawe vimeibiwa na mfanyakazi wa *TANESCO*, na kadhalika *transformer* ya mradi wa umeme wa Nduruma imeibiwa. Je, Serikali inawaambia nini wananchi hao wa Kata hizo mbili ambao hawana umeme kwa sababu ya hujuma ya wafanyakazi wa *TANESCO*?

La pili, kwa kuwa, mradi wa umeme wa Oljoro umeishia kilomita 5 kutoka kituo cha Afya cha Mbuyuni katika Kata ya Oljoro kituo ambacho kinatoa huduma za afya kwa vijiji sita Oljoro, Mbuyuni, Ujamaa, Miongoine, Olosenyie katika Wilaya ya Simanjiro na Kilimatinde katika Wilaya ya Monduli.

Je, Serikali haioni ni busara sasa kumalizia mradi huu ili vijiji hivyo sita viendelee kupata huduma ya tiba katika kituo hicho cha afya?

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, huu mradi wa Midawe kama nilivyosema ni mradi ambao unafadhiliwa na Mamlaka ya Maji ya Arusha, na *TANESCO* ni watekelezaji wa mradi ule.

Mheshimiwa Spika, kwanza kwamba vimeibiwa vifaa vile. Lakini pili, Mheshimiwa Mollel amesema kwamba hujuma hii imefanywa na wafanyakazi wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, sina la kusema kwa sababu wao wafanyakazi wa *TANESCO* wenyewe ndiyo wanatakiwa kuwa walinzi na wahimili wakuu wa utekelezaji wa miradi hii.

Sasa ikiwa Mheshimiwa Mollel anao ushahidi kwamba wao wamehusika katika jambo hili, basi ninaomba nimwahidi Mheshimiwa Mollel kwamba ikiwa uchunguzi utafanyika wakaonekana kwamba wao wameshiriki moja kwa moja katika upotevu wa vifaa hivyo hawana nafasi katika Shirika hili la *TANESCO*. Tutalifuatilia na tutawachukulia hatua kali sana tena sana.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, mradi wa umeme wa Oljoro wa kilomita 5 tu kutoka kwenye sehemu ambayo umeme unapatikana kwenda kwenye vijiji vya Oljoro, Mbuyuni na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mollel, kwamba kilomita 5 siyo *distance* ndefu; na kwa kuwa umeme hapo umekwishafika, naomba Mheshimiwa Mollel aniruhusu niwakabidhi hili *REA* kwa sababu naamini kwamba siyo mradi mkubwa sana, na kwa mahitaji haya ya vijiji sita vyote kutegemea huduma ya Afya hiyo. Ombi lake linakidhi kila aina ya vigezo ili mradi huo ufanyike haraka na upewe kipaumbele.

**MHE. MOHAMMED H. J. MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa vijiji hivyo vya Oldonyosambu, Timbolo na Sambasha tatizo lake ni sawasawa na vijiji vilivyopo katika Kata ya Satiria, Iwinji na Irembo kule Mbeya Vijijini,

na kwa kuwa kuna nguzo za umeme ambazo zimesimamishwa tangu mwaka 1995 na hazijavalishwa kofia na nyingine nyingi zimekwishaharibika.

Je, ni lini sasa uharibifu kama huo wa upotevu wa mali hiyo ambapo nguzo nyingi zimekwishaharibika na thamani yake kwa mwaka 1995 ilikuwa nguzo moja ni shilingi 75,000, na leo hii kupata nguzo kama hiyo moja ni wastani wa shilingi 200,000 Wizara ilikuwaje mpaka mradi huo ukaachawa solemba, na wananchi wa Kata hiyo wakawa hawajapatiwa umeme? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mohamed Mnyaa kwamba wakati nikijibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya wiki iliyopita nilifafanua kuhusu masuala ya utekelezaji wa mradi huo. Lakini baadaye nilipata fursa ya kukutana na Waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo wote watatu, na tumekubaliana kwamba tunakwenda kukagua uharibifu huo uliofanyika tunaufahamu, na kwa msisitizo tu na Mheshimiwa John Malecela naye amesisitiza kwamba ameshuhudia nguzo hizo.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo wamenitaarifu tayari na tumekubaliana kwamba mara tu tutakapomaliza Kikao cha Bunge tutakwenda kufuatilia suala hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa swali lenyewe limeuliza ilikuwaje? Labda niseme tu kwamba miradi mingi iliyokuwa itekelezwe kipindi cha mwaka 1996/1997 ilikumbwa na maamuzi ya Serikali ya kubinafsisha Shirika la *TANESCO* ambayo yalifanywa baina ya mwaka 1997 mpaka uamuzi huo uliporejeshwa mwaka 2004.

Kwa hiyo, kipindi kile kidogo kilikuwa kigumu kwenye masuala yote ya uwezeshaji wa miradi ambayo ilikuwa inasimamiwa na *TANESCO*. Kwa hivi sasa tunalifahamu suala hilo na tunalifanyia mikakati ya makusudi.

Baada ya kumaliza ziara hiyo kujua tunafanyaje kuhusu uharibifu huo na namna ya kurudisha umeme kwenye maeneo hayo.

**SPIKA:** Swali la mwisho Waheshimiwa Wabunge kwa leo, linaulizwa na Mheshimiwa Stanley Kevela , Mbunge wa Njombe Magharibi.

Na. 96

**Kero ya Kupanda kwa Bei ya Umeme**

**MHE. YONO S. KEVELA** aliuliza:-

Kwa kuwa bei ya umeme hapa nchini zimekuwa zikipanda kwa kiasi kikubwa sana na kwamba wananchi wa kawaida wanashindwa kumudu gharama hizo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa kero hizo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli bei ya umeme nchini zimekuwa zikipanda mara kwa mara kama anavyoeleza Mheshimiwa Mbunge.

Kupanda kwa bei za umeme nchini kunasababishwa na kupanda kwa gharama za uendeshaji ambazo zinajumuisha gharama za kukarabati na kupanua miundombinu ya umeme, kupanda kwa bei ya shaba duniani, kupanda kwa gharama za vifaa vya usambazaji umeme (nyaya, nguzo na mitambo ya umeme), gharama za mafuta, gharama za kununulia vipuri na gharama za kununua fedha za kigeni (*Foreign Currency Exchange Losses)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa *TANESCO* iliomba ongezeko la asilimia 40 kutoka kwa *EWURA* ili kukidhi gharama za uwekezaji na uendeshaji na badala yake *EWURA* ilitoa ongezeko la asilimia 21.7 kuanzia Januari, 2008. Bei ya umeme iliyopitishwa haitoshelezi gharama za uwekezaji na uendeshaji.

Mwaka 2007 gharama za kumfikishia mteja umeme zilikuwa ni shilingi 159 kwa *unit* wakati wastani wa pato la uuzaji ilikuwa ni shilingi 92 kwa *unit.* Kwa hiyo, *TANESCO* ilipata hasara ya shilingi 67 kwa kila *unit* iliyokuwa inauza na hivyo ilifanya hali ya kifedha ya Shirika hilo kuwa mbaya zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na kero hiyo, Serikali inaendeleza sekta ya umeme kwa kufuata mwongozo wa Programu Kabambe ya Uendelezaji wa Sekta ya Umeme (*Power System Master Plan* (*PSMP*) na kwa maana hiyo kufanya mikakati ya makusudi ya kutathmini mahitaji ya uwekezaji ambayo yatakidhi malengo ya Maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mikakati hiyo inahusu kuangalia mahitaji yaliyopita, ya sasa na ya baadaye kwa kulinganisha ukuaji wa uchumi jumla. Kwa hivi sasa tathmini inatudhihirisha kwamba kwa hali hiyo ya ukuaji wa sasa wa Tanzania, Tanzania inahitaji kuingiza kwenye uzalishaji *MW 70* hadi *MW 75* kila mwaka ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka.

Kwa hiyo, mkakati mikuu ya kupunguza kero ya huduma ya umeme au kwa maana nyingine kuboresha hali ya upatikanaji ya huduma ya umeme, ni mpango kabambe unaoelekeza hatua za haraka zifuatazo:-

1. Kuongeza uwekezaji kwenye mitambo ya uzalishaji kwa kutumia rasilimali tulizokuwa nazo kwa maana ya kutumia gesi asilia ama maji ama makaa ya mawe.

2. Kufanya uwekezaji wa makusudi kwenye miundombinu ya njia ya usafirishaji ambao kwa hivi sasa inapoteza umeme mwingi mno njiani.

3. Matumizi ya fedha za uendeshaji na utekelezaji wa miradi, miradi inayochelewa kumalizika inaongeza sana gharama za miradi hiyo.

4. Kuongeza wateja kutoka 724,000 waliopo sasa hivi hadi wateja 1,200,000 katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Hii haitawezekana isipokuwa kwa kuboresha huduma kwa wateja wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, pia makali ya bei ya umeme kwa watumiaji yanaweza kupunguzwa kwa kuinusuru *TANESCO* kifedha yaani *Financial Recovery Plan*.

Mpaka sasa *TANESCO* wameshapewa *syndicated loan* ya mabenki mbalimbali ya shilingi bilioni 300 chini ya udhamini wa Serikali ambazo zinatumika kulipia madeni ya nyuma, kujenga *service line* mpya, kukarabati mifumo ya usambazaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba kadri malengo haya na mengine yatakavyoweza kufanikiwa ndivyo ambavyo umeme utamfikia Mtanzania kwa bei nafuu zaidi na kwa uhakika zaidi.

Hali hii itamwezesha kutumia nishati hiyo katika shughuli zake mbalimbali za maisha na maendeleo. Mchango wa nishati ya umeme kwa maisha ya Mtanzania umedhihirika hasa pale kwenye maeneo ambayo huduma hiyo imefika.

Mheshimiwa Spika, ni jukumu letu sote sasa kwamba tuchangie kwenye matumizi bora ya nishati, mipango yenye ufanisi, tija na endelevu ya uwekezaji katika uzalishaji na usambazaji na kwa maana hiyo ushirikishwaji katika hili una maana kila mmoja wetu ajitambue kuwa ni mdau wa mikakati ya kufanikisha azma hii.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kwanza kutoa shukrani na pongezi kwa Serikali kwa kuweka umeme kwenye vijiji vya Ingima Mhanji, Ndandu, Kidungara na Wanging'ombe na vijiji vingi katika Jimbo la Njombe Magharibi. Sasa naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza.

Je, Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba pamoja na sababu alizozitoa za kupanda kwa gharama za umeme sababu kubwa ni kwa Serikali kuingia katika mikataba mibovu ya gharama kubwa kama *IPTL, Aggreko* na kadhalika ambapo mzigo huo wanabebeshwa ni wananchi wa kawaida ambao hawana sababu ya kubeba gharama hizo?

Swali la pili, kwa kuwa Naibu Waziri katika jibu la msingi amesema mpaka sasa *TANESCO* wamepewa *syndicated loan* ya shilingi bilioni 300. Je, kwa nini mpaka sasa

hivi ule umeme haujateremshwa kwa wananchi au kwa watumiaji ili kuonyesha kwamba kwa kweli Serikali imebeba mzigo huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, katika sababu nilizozitoa moja nilisema ni gharama za uendeshaji na Mheshimiwa Mbunge amezungumzia suala la mikataba kama ni sehemu ambayo inaongeza gharama katika gharama za umeme zinavyokuwa.

Mheshimiwa Spika, mikataba inafanyiwa tathmini na inawezekana kwamba uwepo wa mikataba ile umeongeza gharama kwa hali fulani ya huduma za umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuzingatie kwamba mikataba ile ilikuwa ni mikataba ambayo ilitarajiwa kukidhi shida fulani iliyokuwepo ya mahitaji ya umeme ya wakati huo.

Sasa mimi nadhani kama nilivyosema kwa kuwa sisi wote ni wadau ili tuondokane na tatizo hili la kuwa na udharura wa kuwa na mikataba ya umeme na kadhalika. Shida iliyoko ni kwamba tujenge uwezo na tufanye maamuzi ya makusudi kabisa ya kuongeza uwekezaji katika uzalishaji na usambazaji.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuna mahitaji ya *MW 75* kila mwaka kuingia kwenye mtandao na tuna miaka mitatu ambayo hatujaingiza zaidi ya *MW 100* au 120.

Kwa hiyo, hapa tulipo tayari tuna *deficit* ya uzalishaji wa umeme ambao unaendelea. Tayari kwa matatizo ya usambazaji ambayo miundombinu kama tunavyosema inapoteza umeme.

Kwa hiyo, nasema kifupi tusiangalie tatizo lile la mikataba, tuangalie tatizo lake linatokana na wapi na kwamba kusema kweli tuondokane na hili tatizo kwa kuwekeza zaidi na maamuzi hayo yanafanywa humu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hili swali lake la pili la kwamba *TANESCO* wamepewa *syndicated loan* ya bilioni 300 naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba kusema kweli bilioni 300 ni sehemu tu ya mahitaji waliyokuwa wanahitaji *TANESCO* ili kuweza kukidhi shida zao za kifedha.

Bilioni miatatum (Bilioni 300) kwa madeni yaliyokuwepo *TANESCO* na mahitaji yaliyokuwepo *TANESCO* ya kuwekeza ni ndogo sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo limefanywa kwa awamu, *TANESCO* wamepewa bilioni 300 tunafuatilia namna ya matumizi yao ya fedha zile halafu Serikali hii kwa maamuzi yatakayofanywa humu humu ndani tutaangalia namna ya kuwaongezea uwezo zaidi ili waweze kumaliza madeni yao na kuweza kuboresha huduma zao kwa wananchi wa Tanzania.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na maswali yamekwisha. Sasa ni matangazo nikianza na wageni. Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wafuatao:-

Kwenye *Speakers Galley* naomba Waheshimiwa Wabunge tutambue uwepo wa Ndugu Utoah, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Pia yupo Dr. Hosea Mkurugenzi Mkuu, taasisi ya kuzuia rushwa TAKUKURU. Naona alikuwepo lakini ametoka. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hapa Ukumbini pia wapo pia kutoka idara ya Mkaguzi Mkuu Bwana Gregory Teu, Mkaguzi Mkuu Msaidizi, yule pale na Bwana Edwin Rweyemamu, Msaidizi maalum wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. (*Makofi*)

Sasa mbele yao pale wapo wageni ambao ni kutoka (Ubalozi wa Uingereza) *The British High Commission in Dar es Salaam*, Bwana John Brutishly ambaye ni *Political Officer* yule pale, Bwana Darleen Wesh ambaye ni Mkuu wa Idara ya Kimataifa na Maendeleo. Bwana Simon *Gill* Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Kimataifa na Bwana Charles Sokine, ambaye ni Mshauri wa Utawala Bora. Basi labda ni Sokine.

Nilipiga Sokine kwa sababu nilidhani ni mzungu. *Charles Sokine. We are very happy to have you with us Members of the Diplomatic from the British High Commission. We have a long history of cooperation between the UK and Tanzania. And it is all the pleasure to welcome you from the High Commission in Dar es Salaam here at Dodoma. You are welcome. (Makofi)*

Nafurahi sana kutangaza uwepo wa rafiki yangu Balozi Dr. Pius Ng'wandu.

Mheshimiwa Balozi Pius Ngwandu, huyu, ni mmoja wa Watanzania ambao wamejichomoza kwa sifa nzuri amefanya kazi nzuri. Ameondoka katika utumishi wa Serikali bila *scandal* na kwa sasa hivi yeye ni Mjumbe maalum wa *International Atomic Energy Agency*, ni mjumbe pia kwenye *Global Energy Initiative* na Makamu Mwenyekiti wa *International Institute on Capacity Building Agency*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, siyo kwamba amestaafu tu na kwenda kulima mananasi. Lakini anaendelea kutumia taaluma yake kama mnavyojua ana *Ph. D.* Nashukuru sana kwa kazi hizo za kimataifa Mheshimiwa Balozi na tunakutakia mema. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine sasa. Wageni wa Mheshimiwa Dr. Chami, ambao hakutaja uhusiano wala wanakotoka, Bwana Hussein Mdoe, Elia Kivuma, Mwema Juma na Mbaraka Sagilu. Nadhani hawa ni wapiga kura kule Moshi Vijijini. Karibuni sana. (*Makofi*)

Halafu wageni wa Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, orodha ni ndefu. Kwa hiyo, nitawaita kwa ujumla tu ni wageni kutoka jimbo lake na wengi ni Makatibu Kata, Kata ya Kipatimu, Kata ya Chumo, Kata ya Mingumbi na Kata ya Njiane.

Hivyo sasa naomba wale wageni kutoka Kilwa, wageni wa Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, tafadhali wasimame tuweze kuwatambua kwa ujumla wao. Ahsante sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu nao hawatamki wanamhusu vipi. Lakini nadhani itakuwa ni wapiga kura kutoka Jimbo lake la Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam ambao ni Bwana Busolo Zungu, Latifa Abdallah, Lucy Samson, Irene Wilson kumbe hawa ni waimbaji wanaitwa *Survival Sisters* na wote ni walemavu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaguswa sana sisi Waheshimiwa Wabunge na jitihada zenu kuweza kufika hapa Dodoma na kuhudhuria katika Bunge. Karibuni sana. Tunawatakia mema katika maisha yenu na tunavutiwa sana na pamoja na matatizo hayo mliyonayo. Lakini mnajitahidi kuishi vema miongoni mwetu. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Zuleikha Haji Yunus ambaye ni mtoto wa Ndugu yake anaitwa Yunus Mzee Yunus, yule pale, ahsante sana karibu sana kijana. Ahsante sana tunashukuru umetoka Zanzibar kuona kazi inayofanyika hapa. Karibu sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Capt. John Komba, ni Emmanuel Mpahi Mwenyekiti wa Wazazi Kata ya Lituhi, Mbinga Magharibi yule pale pamoja na Lawrence Kashingo, Diwani wa Zamani wa Kata ya Lituhi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Sijui mmekuja na wale samaki watamu. Spika anapenda sana samaki. Hasa samaki wa Ziwa Nyasa. (*Makofi*)

Wageni wengine ni kundi la pili la wageni wetu kutoka Bunge la Malawi, kwa majina sasa sijui ni mwanamke au mwanaume, W. Mgone mwanaume na Hopson Chiwawula.

*We are happy to receive you our visitors from Malawi we share a common border and we are good neighbors, it is a pleasure to have you with us all the way from Lilongwe and Blantire. Thank you. (Makofi)*

Mwisho tuna wanafunzi 49 pamoja na walimu kutoka shule ya sekondari ya wasichana Huruma Dodoma. Walimu na wanafunzi Huruma Dodoma, wale pale. Tena sare zao zinapendeza sana hizi. *(Makofi)*

Ahsanteni sana, tunawatakia mema vijana wetu wa Huruma pamoja na walimu shule yenu naambiwa inaongoza kwa nidhamu katika Mkoa wa Dodoma. Ni jambo la kujivunia sana. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa George Lubeleje Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala anahitaji wajumbe wa Kamati hiyo wakutane ukumbi namba 219 baada ya maswali. Kwa hiyo, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala mara baada ya maswali ukumbi namba 219. Mheshimiwa William Shellukindo Mwenyekiti Kamati ya Nishati na Madini anahitaji wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini wakutane saa 7.00 mchana leo katika ukumbi namba 227. Kwa hiyo, saa 7.00 Kamati ya Nishati na Madini ukumbi namba 227.

Mheshimiwa Wilson Masilingi Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama anahitaji wajumbe wake wahudhurie kikao saa tano leo ukumbi namba 231. Kwa hiyo, Kamati ya Ulinzi na Usalama saa tano asubuhi leo ukumbi namba 231.

Mheshimiwa Mohamed Missanga Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu anaitisha kikao cha Kamati ya Miundombinu saa 7.00 mchana Ukumbi wa Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Dr. Zainab Gama Mwenyekiti wa *APNAC* Tanzania anaomba wajumbe wa *APNAC* wote wasikose kuhudhuria saa 7.15 mchana katika ukumbi wa *African Dream Conference Centre*. Itifaki zote zinazohusi semina hii zimezingatiwa na ni kikao muhimu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, leo kwa Muswada huu ambao uko mbele yetu wa kuidhinisha makadirio ya nyongeza ya matumizi ya Serikali nimepokea orodha ndefu ambayo sijui nisemeje.

Kwenye kanuni zetu na hapa nikumbushia kanuni ya 60 (9) nitaisoma ili tukumbushane tu. Inasema “kila Mbunge atalisemea jambo ambalo liko katika mjadala tu na hata rudiarudia maneno yake au yale yaliyokwishakusemwa na wengine inaendelea na kadhalika”.

Sasa kinachojitokeza katika Muswada huu Serikali ilicholeta ambayo kila mwaka huja hii, ni hoja au Muswada ambao matumizi ya ziada yaliyopatikana kutokana na mapato mbalimbali yanaelekezwa katika sehemu ambazo Serikali imeamua ndiyo kipaumbele.

Sasa kusimama hapa na kusema zingepatikana hizi, zingekwenda na mahali fulani, zingepatikana hizi, mimi nadhani tuna fursa nzuri sana Waheshimiwa Wabunge, kuchangia juu ya vipaumbele wakati tutakapokaa siku mbili kama Tume ya Mipango.

Natoa tahadhari hiyo kwa sababu haitawezekana bila kuathiri mpangilio mzima wa shughuli za Bunge kuwawezesha wote 21 hawa wazungumze leo. Haiwezekani kabisa.

Kwa hiyo, nilikuwa natoa tahadhari hiyo ili itakapotokea kwamba inabidi sasa kukatiza mjadala ili tufanye na shughuli nyingine na mimi naona kwa vyovyote vile itabidi Waziri aweze kuhitimisha hoja hii kwa mchana huu.

Kwa orodha hii ingebidi tuendelee mpaka kesho. Sasa haiwezekani kwa sababu kuna mambo mengine ambayo yanatusubiri na lazima katika mpangilio tuweze kuzingatia mpango uliowekwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, la pili, mahusiano yetu na Waandishi wa Habari, Bunge hili tunajitahidi kuwa wazi. Ukitazama Kanuni ya 114, Fasili ya 9, tunasema hivi: "Shughuli za kawaida za Kamati zitaendeshwa kwa uwazi ambapo Kamati itaalika wadau ili kupata maoni na ushauri wao kwa ajili ya kuboresha Muswada, Hoja na kadhalika." Sasa kinachosahauliwa na wengi wetu na naomba Wenyeviti wazingatie hili, ni ile ya 10 sasa inayosema: "Bila ya kujali masharti ya Fasili ya 9 ya kanuni hii, shughuli zote za Kamati zinazohusu kuandaa na kutoa mapendekezo ya kuwasilishwa Bungeni zitafanywa kwa faragha na isitoshe, maoni ya Kamati yatakuwa ni yale yaliyokubaliwa na wajumbe walio wengi." Sasa wengine mnataoka hapo hapo mnasema yaliyoamuliwa na Kamati kabla hayajaja Bungeni na wengine mnasema tofauti zenu, sasa haya ni matumizi mabaya kabisa ya kanuni zetu na kuvunja kanuni ni suala ambalo litatufanya tufikishane mahali pagumu kidogo na kwa sababu ndio wajibu wetu huo, ni lazima tulinde kanuni.

Isitoshe 12 inasema: "Mjumbe yeyote wa Kamati, hataruhusiwa kuzungumza hadharani maoni ya Kamati kuhusu Muswada au jambo lolote litakalokuwa linashughulikiwa na Kamati kabla maoni hayo hayajawasilishwa rasmi Bungeni."

Ni sawa, wengine mnasafiri na waandishi wa habari na kadhalika lakini hiyo ni katika wakati wa kuangalia mambo kwa ujumla, baada ya hapo inabidi mwingie faragha mzungumze yale ambayo mtayafikisha Bungeni ambayo wakati huo yanabaki ni siri hadi yatakapofika hapa. Kwa hiyo, nawaasa Waheshimiwa na hasa baadhi ya Wenyeviti, wamekuwa na tabia ya kutoka tu pale basi anaitisha Waandishi wa Habari na anasema mambo yako hovyo, sijui kumetokea nini?

Natoa tahadhari mapema kwa sababu Katiba, Sheria, zimenipa mamlaka ya kusimamia kanuni hizi. Kama tutakuwa tunatoka kwenye vikao vya Kamati na tunaeleza tofauti zetu, tunaeleza kila kitu kabla mambo hayajaiva ndani ya Bunge, tunaathiri Kanuni ya 114, Fasili ndogo ya (10), (11) na (12). Niliona nitoe tahadhari hiyo kadiri tunavyoendelea ili mambo yetu yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo nina wageni kutoka Uingereza, ambao wanakuja kuzindua kitabu kinaitwa *A Parliament With Teeth,* yaani Bunge letu limeanza kuonekana sasa linaota meno, nami ni mmoja wa wageni ambao watatoa hotuba kwa sababu ya kukizindua kitabu hicho ambacho kimetungwa na *Africa Research Institute* ya

*London* na baadhi yenu mmealikwa. Kwa hiyo, kwa kuzingatia hilo, naomba nimwachie Kiti Mheshimiwa Naibu Spika ili aendeleze shughuli zilizosalia. *(Makofi)*

*(Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti)*

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria wa Kuidhinisha Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 *(The Supplementary Appropriation (For Financial Year 2008/2009) Bill, 2009)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani Mheshimiwa Spika ametoa mwongozo. Kile tunachofanya ni Muswada. Kwa hiyo, Muswada ni lazima uzungumzie maudhui ya Muswada na sio vile unavyopenda kusema. Kwa hiyo, kama alivyosema tuko wengi sana, idadi ya wazungumzaji ni wengi na naomba wasijirudie. Kwa hiyo, mtu atakayekuwa anazungumza nje ya Muswada itabidi tumuambie uko nje ya Muswada. Nitaanza na Mheshimiwa Ndugai, atafuatiwa na Mheshimiwa Mudhihir, baadaye Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Juma Kaboyonga ajiandae.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niwe msemaji wa kwanza asubuhi ya leo kuhusiana na Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Nyongeza kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009. Nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuagiza kupitia hotuba yake Bungeni hapa alipokuja mara ya mwisho na kuelekeza kwamba fedha za *EPA* zielekezwe katika matumizi ya sekta za kilimo na mifugo. Sasa hapa hapa mwanzo nitoe tu ushauri kwamba Wizara ya Fedha na Serikali kwa ujumla kuhusiana na hizi bilioni 53 zisimamiwe vizuri katika matumizi yake katika Kilimo na Mifugo zinakokwenda. Zisiwe kama kule kwenye Halmashauri katika mashamba darasa, kila fedha ikienda shamba darasa darasa, darasa lenyewe halieleweki liko wapi, lakini fedha zimetumika. Zisimamiwe vizuri ziwe ili matokeo yanayoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nalo niliseme hapa hapa mwanzo, mwisho wa siku itakuwa ni vizuri zikija taarifa hapa Bungeni za matumizi ya mabilioni haya na *impacct* yake kwa jamii yetu ya Tanzania, itakuwa ni jambo jema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijakwenda moja kwa moja, hapa niseme tu kwamba hali ya hewa ya mwaka huu ya mvua ni mbaya, kuna uwezekano mkubwa kabisa wa kuwa na njaa kubwa katika nchi yetu na Wilaya ya Kongwa ni moja ya Wilaya ambazo zinaathirika vibaya kutokana na mvua kutokuja kwa wakati. Kwa hiyo, fedha hizi kupelekwa kwenye eneo la kilimo ni jambo linalotia moyo japo zimechelewa kidogo

kwa sababu msimu wenyewe wa kilimo uko nusu hivi sasa, lakini tunatumaini zikitumika vizuri zinaweza zikaokoa jahazi kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa debe la mahindi ni shilingi 8,000 mpaka 10,000 vijijini. Kwa kiwango hicho cha fedha wananchi wetu wako katika hali ngumu sana. Ndio maana naipongeza Serikali kwa kuelekeza fedha hizi katika sekta hiyo ya kilimo na mifugo zinaweza kusadia kupunguza hali mbaya inayokuja kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningefurahi zaidi kama hoja hii ya Mheshimiwa Waziri, ingekuwa na kiambatanisho fulani kinachoeleza zaidi matumizi ya fedha hizi ili Mheshimiwa Mbunge, yeyote anapoondoka hapa kwenda Jimboni kwake, akiulizwa swali na wapiga kura aweze kujibu. Kwa mfano, Wizara ya Mifugo wamepewa bilioni 10 kwa ajili ya madawa ya mifugo, sasa mwananchi akiniuliza hivi hizi fedha zitapatikana patikana vipi au zitagawanywa gawanywa vipi? Kwa kweli majibu hayapo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa ni vizuri kabla Waheshimiwa Wabunge, hatujaondoka hapa tukapata mchanganuo wa fedha hizi zinaelekea kwenye matrekta, hayo matrekta wananchi watayapata kwa utaratibu gani? Itakuwa ni jambo la maana zaidi. Vinginevyo, Waheshimiwa Wabunge tutaondoka tumepitisha Muswada lakini tukiulizwa maswali na wananchi tutakuwa hatuna majibu. Kwa Muswada wenyewe inatosha ulivyoandikwa. Ninachosema, kipatikane tu kitu fulani cha kutoa maelezo zaidi ili tuweze kujibu maswali halisi ya wananchi kwa fedha hizi ambazo zinawalenga. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye yale mafungu kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha hapa Bungeni kuhusiana na Muswada huu wa Sheria ya Matumizi ya Nyongeza ya Bilioni 53. Tukianza na Fungu 21, Hazina ambao wanapelekewa bilioni tatu ili zile bilioni tatu ziende Benki ya Rasilimali kwa lengo la mikopo ya wakulima. Swali hapa, mtandao wa *TIB* unafahamika kwamba ni mdogo mno. Kwa hiyo, moja kwa moja Mbunge wa Kongwa na wananchi wangu tunajiuliza, hivi hiyo bilioni tatu huko *TIB* tutaipata pataje? Kwanza hiyo *TIB* iko wapi? Hapa Mkoani Dodoma hata tawi lipo? Kwa hiyo, wananchi wangu wataipata pataje? Haya ndio maswali ninayosemea kwamba pangekuwa na kiambatanisho ingesaidia sana kufahamu.

Mara kadhaa Serikali imewahi kupeleka hela kwenye mabenki kwa lengo la kuwapelekea wananchi, zikishafika kwenye mabenki zinaanza kwenda kwa taratibu za kibenki. Taratibu za kibenki kwa wananchi wetu hawa, wakulima, ni ngumu sana kuzifikia. Wilaya yangu ni moja ya Wilaya ambazo zina matrekta mengi kidogo katika nchi hii. Ukitaja Wilaya tano zenye matrekta mengi Tanzania, Kongwa ni mojawapo, tuna matrekta japokuwa ni mabovu mabovu lakini yanafika hata 300 katika Wilaya ya Kongwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko mikoa hapa ina matrekta 20 tu Mkoa mzima. Lakini hayo wamehangaika wananchi wenyewe kwa kuhangaika kwao kuyapata, fedha

zinazopita kwenye taratibu kama hizi hakuna mwananchi hata mmoja wa Kongwa amewahi kupata trekta moja, hakuna. Kwa hiyo, tunasimama hapa kulisemea hilo mapema. Utaratibu wa wananchi hawa kufikiwa utakuwakuwaje? Bilioni tatu hizi zinazoenda *TIB* kwa nchi nzima, japo zinaongezea zile ambazo ziko huko, lakini ukichukua hii bilioni tatu ni fedha kidogo.

Ungeigawa kwa Mkoa wa Dodoma peke yake yenye Wilaya sita, maana yake ni kama wastani wa milioni 500 kila Wilaya. Milioni 500 ni kama trekta 10 kwa wastani wa milioni 50 trekta moja. Trekta 10 ukizipeleka pale Kongwa apewe nani na nani asipewe? Itakuwa ni tatizo, kwa hiyo hizo fedha ni ndogo, sasa mgawanyo wake uende vizuri kidogo kidogo hivyo hivyo nchi nzima angalau basi kila Wilaya ikajua kama ina matrekta yake hata kama matano lakini angalau zikafika mahali fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, masharti haya ni vizuri *TIB* wakapewa mapema wasije wakakopesha Dar-es-Salaam, zikakopeshwa kiujanja ujanja kama ilivyokuwa *EPA*. Ujanja ujanja wa *EPA*, sasa huku *TIB* na kwingine wasifanye ujanja ujanja tena. Hili ndio tunalisemea mapema kwamba litazamwe vizuri ili wakulima wetu wapate mikopo kweli. Hilo ni la kwanza kwenye lile fungu la 21. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija Fungu 43, ambapo Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, inapewa bilioni 40. Ni jambo jema sana, sisi Wabunge tunaliunga mkono kabisa. Bilioni 40 hizi zimegawanywa bilioni 30 kwa ajili ya mbolea na mambo mengine madogo madogo, madawa ya kilimo na kadhalika na bilioni 10 kwa ajili ya matrekta madogo, *power tiller*. Sasa nianze na zile 30 zinazoenda Wizara ya Kilimo. Waheshimiwa Wabunge wamezungumza, Mheshimiwa Naibu Spika, umetuambia tusirudie rudie na sina haja ya kurudia rudia, ushauri ni ule ule kwamba je, tukijenga Kiwanda cha Mbolea haitakuwa tumefanya tija kubwa zaidi kwa maana ya uendelevu wa matumizi ya fedha hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaendelea kushauri kwa kurudia kwa sababu ni muhimu kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kuzitumbukiza zote katika kujenga Kiwanda cha Mbolea na tunayo gesi kule Mtwara, tunayo gesi kule Mkuranga na mahali pengine ili tutatue tatizo la mbolea kwa miaka mingi zaidi kuliko kununua mifuko michache mwaka huu, halafu mwakani ikawa haipatikani mahali popote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bilioni 10 ambazo zinalenga kununua matrekta madogo madogo, kwenye mawasilisho ya Mheshimiwa Waziri amesema suala la *power tiller*. Kama nimemwelewa vizuri, *power tiller* ni vile vitrekta vidogo vidogo vile vya kushika kwa mkono namna hii unaburuza. Sawa, vinafaa sana kwenye mashamba ya mpunga na maeneo mengine kidogo, lakini sisi kule Kongwa tunachohitaji ni ama trekta lenyewe ama jembe la kukokotwa na ng'ombe. Ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Waziri na Wizara ya Kilimo ni kwamba jembe la kukokotwa na ng'ombe na lenyewe ni *power tiller*. Ndiyo, unatumia *power* ya ng'ombe au *power* ya punda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, majembe ya kukokotwa na ng'ombe nayo yaingie hapa. Wakulima wengi zaidi watakomboka kwa kupata majembe ya kukokotwa

na ng'ombe ili waondokane na jembe la mkono. Kwa hiyo, katika mkopo huu wa milioni 10 hilo nalo litazamwe. *Power tiller* inategemea dizeli ambayo mara bei zake zipande mara zishuke na spea zake sijui ziko wapi? Katika Mkoa wa Dodoma sijui kama kuna duka? Ukimpa mwananchi *power tiller,* atalimia mwaka huu kwa sababu bado ni mpya, mwakani na mwaka kesho kutwa, *pressure* inapanda, *pressure* inashuka, *power tiller* imeharibika hajui spea inapatikana wapi? Kwa hiyo, jambo hili tulitazame na hoja yangu hapa ni kwamba tupeleke fedha hizi kwa kiwango kikubwa kwenye majembe ya kukokotwa na ng'ombe, yatakuwa na *impact* kubwa zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 99, Wizara ya Mifugo inapata bilioni 10 kwa ajili ya madawa ya mifugo, ni jambo jema sana kwa sababu mara nyingi tunaposema habari ya fedha za Serikali kwenda kwenye sekta ya kilimo, mifugo inasahauliwa. Naipongeza sana Serikali kwamba katika fedha hizi wamekumbuka mifugo. Maswali ni yale yale, madawa gani yatapelekwa wapi kwa utaratibu upi? Ni mambo ambayo ni vizuri Waheshimiwa Wabunge tukayafahamu ili tunapoondoka hapa wananchi wakituuliza maswali tuweze kuyajibu, yatasambazwa vipi madawa haya? Je, kufufua majosho ni sehemu ya mradi huu, itakubalika? Sisi Kongwa kule tuna majosho karibu 15, yanayofanya kazi ni matano tu, 10 hayafanyi kazi. Je, tunaweza tukapata fedha hizi tukakarabati majosho ili majosho yale yaweze kufanya kazi tukaboresha mifugo kama lengo la fedha hizi? Ndio maana nilikuwa nahitaji maelezo zaidi, sio kutoka kwa Wizara ya Fedha lakini kwa Serikali kwa ujumla hasa kutoka katika Wizara zinazohusika ili kutusaidia Waheshimiwa Wabunge kwenda kujibu maswali halisi ya wananchi yanayolengwa na nia hii nzuri ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba niseme kwa kusisitiza kwamba fedha hizi bilioni 53 zisimamiwe vizuri huko Kilimo na Mifugo zinakoelekezwa, zisiwe kama mashamba darasa kama nilivyosema mwanzo na kwamba mwisho wa siku Bunge lipate taarifa tuweze kupima matokeo ya matumizi ya hizi bilioni 53. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba nianze na *Vote 43,* hii ya Wizara ya Kilimo na Chakula. Lakini kabla ya kutoa mchango wangu naomba nitamke mapema kwamba naiunga mkono hoja iliyopo mbele yetu kwa asilimia mia moja. Katika hii *Vote 43* sina mgogoro mkubwa ila nilitaka kutoa angalizo tu. Tunafahamu kwamba kwa msimu huu kwa mazao mengi msaada huu mkubwa wenye manufaa utakuwa umechelewa, lakini kwa zao la korosho kwa mfano, sisi pembejeo zetu tunaanza kuzitumia mwezi wa sita. Kwa hiyo, napenda kutoa angalizo kwamba hivi sasa zile asilimia za *export levy* ambazo zingekuwa zimepelekwa kwenye dawa za korosho ni 59% tu imetolewa. Bado Hazina mmekamatia bilioni 1.95 ambazo hazijafika. Tungeomba pesa hizi zikitoka zitoke kwa wakati na naamini kabisa Waziri wetu wa Kilimo ametuokoa kwa miaka miwili mfululizo kwenye suala hili la korosho mkimwezesha, naamini kwamba tutapata pembejeo hizi kwa wakati na hivyo kupandisha uvunaji wetu kutoka tani 66 mpaka tani 99 ile ambayo tulikuwa tumejiwekea kama lengo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri vilevile basi ununuzi ufanywe katika *source.* Hawa wafanyabiashara tumewakamata kwenye ununuzi, sasa wamegeuka wanatuumiza kwenye madawa haya ya kupulizia mikorosho. Sina ugomvi kabisa na Wizara ya Kilimo, nina uhakika pesa hizi zitatumika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo yangu kidogo yapo kwenye *Vote 99.* Bilioni 10 zilizotolewa zote zimepelekwa kwenye madawa ya mifugo, hii wanayoiita *verterinary services, good,* sina matatizo. Lakini ni kwa nini mara zote mnaonekana kama mna aleji na uvuvi? Hakuna hata senti moja iliyotengwa katika milioni 10 hizi kupelekwa katika uvuvi. Hivi sasa Serikali inafanya kazi nzuri ya kudhibiti uvuvi haramu kwa kuchoma moto nyavu zenye matundu madogo. Tulitarajia kwamba miongoni mwa pesa hizi mngekuwa mnaonesha njia vizuri, huko siko ndiko ni huku, nyavu hizo hazifai zinazofaa ni hizi. Lakini pesa zote mmezipeleka kwenye mifugo. Sasa nashindwa kuelewa matatizo yenu ni samaki au ni wavuvi? Hili jambo ni lazima lizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matundu makubwa, jarife, sio nyavu ambazo unaweza kuvua katika maji ya upondo, hayo unatakiwa uvue kwenye maji nje ya milango ya bahari yenye pima mpaka 100. Bilioni 10 hizi zingesaidia kabisa sio kuleta nyavu tu, lakini kusaidia hata boti badala ya kutegemea upondo kwenye maji ya mita 100, upondo haufanyi kazi na kama upepo hamna tanga linalala kwenye mlingoti vile vile. Kwa hivyo, badala ya kuwasaidia na wavuvi, mpaka wakati mwingine tunajiuliza hivi kwa nini ilitolewa maliasili kule? Maana tunaona tulichokikataa na tulichokifurahia ni yale yale, hatuelezi wala hatuchelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumzia haya sizungumzii tu habari ya Jimbo la Mchinga, nazungumzia Bahari ya Hindi, nazungumzia Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Ziwa Viktoria. Uvuvi unaleta ajira sio kwa wavuvi na wachuuzi tu lakini hata ukipita mitaani wakaangaji wa samaki, mahoteli yetu na hata sehemu ya utalii inategemea uvuvi. Ukienda hoteli yoyote kubwa unategemea ule kaa, ule pweza, ule ngisi, ukimsahau mvuvi mambo haya yote yanakuwa hayawezekani.

Kwa hiyo, sasa hivi ningeshauri, maadamu mchakato wa bajeti umeanza na mmeshaweka kipaumbele katika hizi bilioni 10 kwenye mifugo, tunakuombeni tafadhalini tafadhalini kwenye bajeti inayokuja hiyo sasa muweke mbele uvuvi. Tunatoa hili mapema kwa sababu ndio kipindi hiki mnachoandaa. Jamani wenzetu msije mkatutoka mikononi bure, hili kwetu naona kama ni husuda na husuda tunaamini inaweza kuangusha hata jengo kubwa kama hili la Bunge. Jamani, mkila na kipofu msimshike mkono, harufu inayonukia ni ya biriani yeye kila akimega ni tonge la ugali wa muhogo, bada, mboga fiwi ni lazima mtakosana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, inawezekana kuna watu wanawaona samaki kama nyoka lakini ladha ya chakula sio aina ya chakula ni *taste* ya wewe mwenyewe, ndio maana ukiumwa malaria hata ukiletewa wali wa mpunga kwa kuku unaomba uji wa ndimu. Sasa msichukulie tu kila kitu ng'ombe, mifugo, kondoo, mbuzi, samaki nao wana nafasi yao ya ajira kwa Mtanzania, wana nafasi ya uchumi kwa Mtanzania. Mnapochoma

moto nyavu hebu tupeni nyavu nyingine basi na hizi zinapatikana kwenye hizi bilioni 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sipendi kurudia kama ulivyotuonya, lakini nilikuwa natoa angalizo hili hasa katika *vote* ya 99, mchakato wa sasa mweke na uvuvi mbele. Hizi bilioni 10 zichukueni kawapeni watu wa ng'ombe na mbuzi sisi tutasubiri lakini hiyo bajeti inayokuja mwangalie kwamba mlitusahau ili muweze kutukumbuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia na namtakia afya njema Waziri wa Kilimo ili aendelee kutukomboa watu wa korosho kupitia pesa hizi vile vile. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ili nami nichangie katika hoja iliyo mbele yetu ya Muswada wa Maongezo ya Bajeti kwa kipindi cha mwaka 2008/2009. Kwanza nitamke rasmi kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Kwa hiyo, naafikiana na maelezo yaliyotolewa na Mwenyekiti wangu alipokuwa anatoa maelezo ya Kamati ya Fedha na Uchumi. Kwa hiyo, nataka nitumie fursa hii kusisitiza baadhi ya mambo ambayo nadhani ni vizuri niyaseme kwa manufaa ya uchumi wetu na shughuli nzima tunayoitekeleza hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na matumizi ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba, fedha za *EPA* zikasaidie sekta ya kilimo. Lakini kwa kumbukumbu zangu Mheshimiwa Rais alisema pamoja na mambo mengine kwamba fedha hizi zipelekwe *TIB* ili kuongeza mtaji wa benki yetu ya *TIB* kwa madhumuni ya kuiongezea uwezo benki hii ili kutoa mikopo ya muda mrefu na hususan kwenye sekta ya kilimo. Kutokana na maelekezo haya ya Mheshimiwa Rais, mimi binafsi ninasikitishwa sana na kiasi kidogo kilichotengwa kwa ajili ya kuongeza mtaji wa *TIB.* Chini ya Fungu hili ambalo lina shilingi bilioni 53 eti ni shilingi bilioni tatu tu ndio zinakwenda kuongeza uwezo wa benki ya *TIB* na kwa maana hiyo dirisha litakalowakopesha wakulima. Hiki ni kiasi kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja kwamba *TIB* inafanyiwa mkakati mwingine wa kuiongezea mtaji wake na hoja hiyo ndio inayotupelekea kutaka kuona kwamba hizi bilioni tatu kutoka *EPA* zinatosha. Mkakati huo utaiongezea *TIB* shilingi bilioni 21 kutoka sehemu nyingine lakini mwisho wa siku mtaji wa *TIB* utafikia shilingi bilioni 50. Bilioni hizi 50 zinatarajiwa ndio ziwe msingi wa kukopesha kwa muda wa kati na muda mrefu sekta ya viwanda, sekta ya kilimo na miradi mingine ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ninayojaribu kuijenga hapa ni kwamba shilingi bilioni 50 kwa kuzitamka zinasikika ni nyingi lakini kwa benki ya maendeleo na hasa unapotaka kuelekeza katika maeneo ambayo yataisaidia nchi kwenda mbele, shilingi bilioni 50 ni kitu kidogo sana. Kwa hiyo, nafikiri kwamba, pamoja na dhamira nzuri ya kukipa kilimo kipaumbele lakini tungeweza kukipa kilimo kipaumbele kwa njia nyingine kwa kutumia fedha hizi za *EPA.* Leo hii Serikali inaomba idhini ya kutumia shilingi takriban bilioni 40 izipeleke kwenye kilimo kwa kununulia mbolea na pembejeo, kwa

lugha ya kigeni, hiyo ningesema ni *consumption expenditure, recurrent expenditure.* Maana yake zikishaingia hizo tukija mwaka kesho tukiuliza ziko wapi? Zimekwenda, hatuna cha kuonesha. Lakini tungeweza kufanya vizuri kwa kutumia fedha hizo hizo shilingi bilioni 40 ama kwa kuwa na miradi endelevu katika sekta ya kilimo. Tatizo hapa ni miradi endelevu, hizi pesa ziingie ama moja kwa moja kwenye kilimo lakini kwa miradi endelevu na sio kununulia mbolea peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la msingi ninalotaka kulisististiza hapa ni kwamba nchi yetu katika sekta hii ya kilimo imekuwa inategemea sana mvua. Tunategemea sana mvua kiasi kwamba mvua ikiwa mbaya kama ilivyo msimu huu, wote tunakuwa katika hali ya dharura. Lakini sisi Tanzania tuna sababu gani ya kuendesha uchumi wetu kidharura dharura? Kizimamoto zimamoto? Kuna sababu gani? Mito ipo, mabonde yapo na kama hivi sasa uwezo ndio huo unapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitarajia wenzetu wanaopanga wangezingatia vipaumbele vya Kitaifa na siyo kuanza kwa kutafuta fedha halafu ndiyo tunasema tuzifanyie nini na sio kwamba tunakuwa na mipango halafu inatafuta fedha. Tunatakiwa tuwe na mipango na baadaye tutafute fedha sio tuwe na fedha halafu tutafute cha kuzifanyia, lililo mbele yetu hapa ni kwamba tuna fedha tuzifanyie nini na kwa sababu kuna dharura ya chakula tuzipeleke kwenye kilimo, hata kama ni kununulia mbolea, kununulia pembejeo.  Sasa ninalotaka kuliuliza hapa ni kwamba hivi zisingekuwepo hizi fedha za *EPA* na leo kuna dharura kwamba pembejeo zinatakiwa mbolea inatakiwa tungefanya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wala tusijifiche chini au nyuma ya pazia kwamba kuna dharura ya chakula Mheshimiwa usitukwamishe, kwa sababu sasa hivi hili jambo ni dharura, ni *crisis* kwa hiyo mtu yoyote atakayeonekana kusimama mbele ya Azimio hili au pendekezo hili ataonekana haitakii mema nchi lakini si kweli. Tunalojaribu kulisema ni kwamba tatizo ni chakula tungeangalia tuzipeleke wapi ili tuzalishe zaidi kwa maana ya uendelevu, tuzipeleke katika sekta ya umwagiliaji.  Huko huko kwenye kilimo nilitarajia Waziri wa Kilimo angesema katika nchi yetu maeneo yetu yanayoweza kumwagiliwa ni haya lakini yana mapungufu haya na haya hatuna fedha, tupeni fedha tuendelee kuzalisha huku. Hilo lingekuwa linaeleweka lingeingia akilini vizuri zaidi kuliko *consumption,* leo hii tunapeleka 40 bilioni mwaka ujao hazipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nasisitiza kipaumbele kiwe ni kuzielekeza fedha hizi kwenye benki ya TIB.  Sisi CCM katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, tulitamka rasmi kwamba ndani ya kipindi hiki cha miaka mitano tutafanya kila juhudi tuunde benki ya wakulima. Tatizo kubwa katika sekta ya kilimo ni kukosekana kwa mikopo nafuu na ya muda mrefu.  Kilimo hiki tunachokipelekea 40 bilioni leo kwa jinsi kilivyo cha kujikimu, cha jembe la mkono na kadhalika hakitatuvusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo letu ni mikopo nafuu ya muda mrefu tungetumia fedha hizi kuziweka kwenye Benki ya Maendeleo ili wakulima wenye sifa za

kukopesheka wakakope kwa masharti nafuu walime, wazalishe kwa wingi, nchi yetu ingekuwa na neema ya chakula ambayo ndiyo tunatafuta na ndiyo shabaha yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo bila ya kurejea yaliyosemwa na wenzangu niseme tu huko ambako Serikali imekwishaamua pesa hizi zinakwenda, zisimamiwe kikamilifu kuhakikisha kwamba tunapata thamani ya fedha tunazozipeleka huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na naiunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu unaohusu matumizi ya ziada ambalo Bunge lako Tukufu linaombwa kuidhinisha ili ziweze kutumika kama jinsi ambavyo Waziri wa Fedha ameweza kutufahamisha hapa jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina masuala matatu ambayo nilikuwa napenda tuweze kuangalia kuhusiana na Muswada wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza Waziri wa Fedha katika maelezo ambayo aliyatoa hapa Bungeni amezungumzia kwamba anawasilisha Muswada huu kwa mujibu wa ibara Na. 136(3) na ibara Na. 99 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo kuidhinisha fedha za ziada. Sasa nilipokuwa naangalia Katiba ili kuweza kuona kama maelezo yanaendana kweli na Katiba unakuta kwamba ibara ya 136 ya Katiba inazungumzia idhini ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na fedha zinazotoka kwenye Mfuko wa Hazina. Ibara ya 136(3), haizungumzii idhini ya Bunge kwa hiyo, maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa hayaendani hata kidogo na ibara ya Katiba ambayo nimeisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya Katiba ambayo inazungumzia idhini ya Bunge ni ibara ya 137(3)(b) ambayo pamoja na mambo mengine inazungumza kama ifuatavyo naomba kunukuu: “Ikiwa katika mwaka wa fedha wowote inaonekana kwamba kuna fedha ambazo zimetumiwa kwa ajili ya shughuli fulani kwa kiasi kinachozidi kiwango cha matumizi yaliyoidhinishwa na sheria ya matumizi ya fedha za Serikali kuhusu shughuli hiyo au kwamba fedha zimetumiwa kulipiwa gharama ya shughuli ambayo haikupangiwa fedha za matumizi kwa mujibu wa sheria kutawasilishwa kwenye Bunge makadirio ya matumizi ya nyongeza au kadri itakavyokuwa maelezo ya matumizi ya ziada na baada ya Bunge kuyakubali hayo makadirio ya matumizi ya nyongeza au maelezo ya matumizi ya ziada kutawasilishwa kwenye Bunge Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na fedha hizo zitatumiwa kulipia gharama za shughuli zinazohusika na hayo makadirio au maelezo”.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara hii ya Katiba inazungumzia pale ambapo Bunge limepitisha matumizi, lakini kutokana na shughuli za Serikali imeonekana kwamba matumizi yale yanazidi. Ibara hiyo ya 136(3) ambayo Mheshimiwa Waziri

ameizungumza haizungumzii iwapo kuna mapato ya ziada sasa yanaingizwa kwenye mapato na yafanyiwe matumizi kama jinsi ambavyo yanavyoshughulikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Bunge tuna taratibu za kuhusiana na mapato na matumizi ya Serikali, Serikali huwa inawasilisha vitabu vinne na kitabu cha kwanza *volume* I huwa kinahusu *financial statement and revenue estimates*. Kwa kuwa fedha za EPA hazimo kwenye *revenue estimates* ambayo Bunge lilipewa na likipitisha pamoja na bajeti nilitarajia kwamba Wizara ya Fedha pamoja na kuleta maombi ya matumizi ya ziada ingeleta *schedule* ya kufanya *amendment* kwenye *revenue estimate* za Serikali, lakini *schedule* hiyo haipo kwa sababu fedha za *EPA* ni pato jipya sio fedha ambazo zilikuwepo sasa zimetumika kwa ziada.

Kwa hiyo, naomba niweze kupata maelezo kwa upande wa Serikali kuhusiana na vifungu hivyo vya Kikatiba lakini kuhusiana na *revenue estimate* ambazo zipo lakini ambazo Serikali haikuweza kuleta *schedule* yake ya *revenue estimate*, wameleta *schedule* kwa ajili ya matumizi ya ziada. Lakini matumizi ya ziada yanayozungumzwa kwenye Katiba ni matumizi ya fedha ambazo zipo ndani ya mapato ya Serikali sio pato la ziada ambalo Serikali imeweza kulipata kama jinsi ambavyo pato la *EPA* lipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, napenda Serikali ilifahamishe Bunge fedha hizi ambazo inaziomba hivi sasa, ndiyo inaziomba ikazitumie au imekwishazitumia kwa sababu kama Serikali imekwishatumia fedha hizi tungetarajia Waziri wa Fedha awasilishe nakala ya kivuli cha idhini ambayo Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ametoa kwamba fedha hizi zitumike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu ni kwamba msimu wa kilimo, kimsingi nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Mudhihir kwamba kwa upande wa watu wa korosho bado lakini pembejeo inayozungumzwa hapa ni pembejeo ya mbolea. Mbolea msimu wake umekwisha na tayari Serikali imekwishanunua mbolea ya ziada ya kile kiasi ambacho tulikiidhinisha Bungeni. Kwa hiyo nilikuwa napenda Mheshimiwa Waziri wa Fedha atufahamishe ile mbolea ya ziada ya kiasi ambacho kimekwisha zaidi ya kiasi ambacho kiliidhinishwa Bungeni kama ilitokana na fedha hizi ambazo zilitarajiwa kutoka kwenye *EPA* au fedha ambazo tayari zimekwishatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho baada ya masuala haya ya Katiba na ya kiutaratibu wa Bunge, napenda niungane kabisa na Mheshimiwa Kaboyonga kwamba haiwezekani tupate fedha ndiyo tuseme tunazitumiaje, inabidi kama nchi tuwe na mpango, mpango huo uwe *sequences* tuweze kujua tunafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nakubaliana kabisa na maelezo ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzanin Bungeni kwamba, tungeweza kufaidika sana iwapo fedha hizi zingeelekezwa kwenye maeneo maalum kwa ajili ya uzalishaji wa chakula ili nchi iweze kuondokana na tatizo la njaa kama jinsi ambavyo Serikali imeeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuzipeleka fedha hizi kwenye mbolea na msimu wenyewe umekwisha maana yake ni kwamba mwakani tutahitajika tuwe na bajeti kubwa

zaidi ya kufikia zaidi ya bilioni 60 kwenye mbolea kwa sababu ndiyo bajeti ambayo imeingia mwaka huu. Lakini iwapo fedha hizi, tungezipeleka kwa mfano Benki ya Rasilimali na wakulima wakachukua fedha za kutosha na kulima maekari na maekari ya chakula mwakani fedha hizi zingekuwa ni *revolving fund*, zingeweza kurudi na kutumika zaidi kwa ajili ya maendeleo. Kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Spika alivyosema masuala mengine tutaweza kuyazungumza wakati Bunge limekaa kama Kamati ya Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata maelezo ya Kikatiba ili huko mbele tunakokwenda likitokea suala kama hili tena na kama kuna makosa katika haya ambayo tunayo sasa tusiweze kuyarudia tena. Nilikuwa napenda nipate maelezo ya Serikali kwa upande huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kidogo tu kuhusiana na hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza nianze kwa kusema naunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha na Uchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nilitaka kutoa maelezo machache kuhusiana na suala hili. Nakubaliana na hoja nyingi ambazo zimetolewa na wenzangu Wabunge juu ya umuhimu wa kuwa na mipango ya kilimo ya muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Mheshimiwa Kaboyonga alikuwa anazungumza kwa kirefu sana juu ya umuhimu wa kuwa na mfumo wa kutoa mikopo kwa wakulima. Sisi katika sekta ya kilimo tunaunga mkono sana suala la kuwa na mikopo na suala la kuwa na Benki ya Kilimo. Lakini kitu ambacho nilitaka kutoa ufafanuzi ni kwamba, mipango yoyote ile inatakiwa iwepo ya muda mfupi, iwepo mipango ya muda wa kati na mipango ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la fedha zinazoelekezwa katika ruzuku siyo jambo jipya. Ni kwamba mwaka huu katika Bunge la Bajeti, Bunge hili liliidhinisha matumizi ya fedha za ruzuku shilingi 31 bilioni. Kati ya hizo 23 bilioni zingeelekezwa katika utoaji wa ruzuku kwa mazao ya chakula ili kuwawezesha wakulima waweze kupata mbolea, kulima mazao ili tuweze kujitosheleza na tusitegemee kuagiza chakula kutoka nje kwa sababu kwanza ni ghali na vile vile duniani hakuna chakula cha kutosha. Huo ndiyo msingi wa jambo lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulichofanya wala sio kwamba fedha hizi Serikali inanunua mbolea, Serikali imetengeneza mfumo wa *voucher* na tulikuwa tumekusudia hapo awali kwamba tungetoa *voucher* ya kumwezesha mkulima kwenda kununua mbolea kwa kumpa kitu kinaitwa *support* au *subside* ili anunue mbolea ambayo kama tusingempa angeshindwa kumudu bei. Huo ndiyo msingi wa fedha hizi. Tumetengeneza mfumo huo kwa ajili ya mazao mawili, zao la mahindi na zao la mpunga katika mikoa inayokaribia kumi. Mikoa hiyo ni pamoja na Iringa, Ruvuma, Mbeya,

Rukwa, Morogoro, Arusha, Kilimanjaro na Manyara, Wilaya za Tarime na Wilaya ya Sikonge katika Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Mara. Kwa hiyo, mpango ule wa kutoa ruzuku upo unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia Waheshimiwa Wabunge wanasema kwamba, msimu wa kilimo unakaribia kumalizika. Lakini wakati huu tunapozungumza ndiyo wakulima sasa wanahitaji mbolea ya kukuzia. Kwa hiyo, mfumo huu wa kutoa *voucher* utahitaji fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme kwamba, katika bajeti ya awali tulikuwa tumekusudia kuwapa *support* wakulima wapatao milioni mbili na nusu, lakini kutokana na kupanda sana kwa bei za mbolea ilionekana kama tutaendelea kuwapa ruzuku ile iliyokusudiwa fedha iliyokuwa imetengwa na Bunge hili isingetosha na kazi ya kuwapa ruzuku wakulima inaendelea lakini fedha zile haziwezi kutosha na wakati huo wakulima wanapohitaji mbolea kwa ajili ya kukuzia ndiyo wakati huo ambapo tunahitaji kuwapa fedha ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kurudia, Serikali haiombi fedha ili kununua mbolea, mbolea iko nchini, Serikali inaomba fedha hizi ili kumpa mkulima uwezo kupitia *voucher system* ili aweze kununua mbolea aitumie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mpango wa muda mfupi kwa ajili ya kulisaidia Taifa kupata chakula. Kama tusingeweza kufanya hivyo maana yake ni kwamba tungekuwa hapa tunaliomba Bunge litupe fedha za kuagiza chakula kutoka nje. Naamini shilingi bilioni 30 zinazokwenda kwenye mbolea zisingeweza kuagiza chakula kutoka nje cha kutosheleza mahitaji ya Watanzania katika mazingira ambako mvua zinaleta matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, narudia, huo ni mpango wa muda mfupi wa kulisaidia Taifa kujipatia chakula, kwa kuwasaidia wakulima katika maeneo yanayozalisha mazao ambayo ndio *staple food* ya Tanzania, mahindi na mpunga. Wako Waheshimiwa Wabunge, wanasema hizi fedha zitafikaje kwa mfano, nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa Mbunge wa Busega anasema zitafikaje Busega. Zinaweza zikafika Busega kwa sababu Busega vile vile ikikosa chakula tukipeleka mahindi zitakuwa zimefika Busega. Hapa tulitazame jambo hili kama nchi. Busega na Bunda zinafanana kabisa hatulimi mahindi, kwa hiyo hatuwezi kupeleka *subside* ya mahindi katika maeneo ambayo hayaoti mahindi. Lakini njaa ikija tutapeleka mahindi katika maeneo hayo. Yatakuwa yanatoka katika maeneo ya Tanzania yanayolima mahindi. Hapa tunali-*address* jambo hili kama nchi. Nadhani ni vizuri tulitazame hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika fedha inayoombwa, kuna shilingi bilioni 10 tunazipeleka kwa ajili ya madawa ya mimea ambayo inahusiana na korosho, pamba na mazao mengine ya biashara na miche ya kahawa na miche vile vile ya chai. Kwa hiyo, zinagusa sehemu kubwa sana ya nchi yetu. Kwa hiyo, nilitaka nitoe ufafanuzi huu ili tuelewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo labda niseme juu ya mikopo. Nasema ikiwa huwezi kumpa *subside* mkulima huyu na hawezi kununua mbolea ni *disaster*, lakini hili ni suala la muda mfupi, suala la muda wa kati na mrefu ni kuweka mfumo wa mikopo ili hatimaye wakulima hawa wa-*graduate* kutoka kwenye *subside* waende kwenye mkopo. Kwa hiyo, hapo ndipo naunga mkono kabisa hoja za Waheshimiwa Wabunge wanaosisitiza umuhimu wa kuwa na mfumo wa ukopeshaji hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sisi ndiyo tunaoshughulika na jambo hili kama Bunge, nadhani mawazo haya yanaweza yakatusaidia sana katika bajeti inayokuja, kwamba tuweke mfumo ambao mkulima wetu atasema sasa nimejua namna ya kutumia mbolea na *subside* hakuna kwa hiyo natumia sasa mfumo wa mkopo kupata fedha niende niweke mbolea na mbegu bora katika shamba langu, nizalishe, halafu nitalipa kwa kutumia mfumo wa Benki ya Kilimo mfumo wa *TIB* ambayo ina dirisha au mfumo wa *SACCOS* ambayo itafikisha mikopo na hilo linakuja katika mfumo wa muda wa kati ambao unawasaidia kusukuma mbele kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wa zaidi ya hapo ni kusisitiza zaidi umwagiliaji maji ili tujiondoe kabisa katika kutegemea mvua. Kwa hiyo, masuala haya yote yanakubalika, ninachoweza kusema ni kwamba, lazima tuwe na mpango wa muda mfupi, mpango wa muda wa kati na mpango wa muda mrefu wa kubadilisha kilimo cha Tanzania. Hilo ndio suala la msingi na kwamba tuahirishe kuwapa wakulima mbolea tutakuwa tunaahirisha kuondokana na *problem* ya njaa halafu tutakuwa tunakaribisha njaa wakati tuna *invest* katika muda wa kati na muda mrefu. *Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani *to solve problem* ambayo ni *basic*, ipo tunaiona na wote tunaona hali ya hewa ilivyo mbaya, wakulima wale ambao wanapata mvua tuwasaidie wazalishe chakula kwa manufaa ya Taifa zima. Baada ya maelezo hayo narudia kusema kuwa, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kule kwangu nimepigiwa simu kwamba Mawakala walishapeleka mbolea kwa wakulima, sasa wanapeleka zile *voucher* benki hakuna benki. Nilipomwuliza Waziri wa Kilimo anasema tunaomba hii *Supplementary Appropriation* B*ill* ipite ndiyo hela ziende kwenye mabenki wawalipe Mawakala ndiyo mbolea iagizwe na Mawakala. Kwa hiyo, mbolea iliagizwa na Mawakala wananchi walipewa *voucher*. Sasa Mawakala wengine walikuwa na mbolea, wakasambaza kwa muda mrefu hawajalipwa fedha kutokana na kukosekana hizi fedha. Sasa zikitokea ndiyo wanaendelea kusambaza ile mbolea, wengine walishasimamisha, wengine walisambaza kwa mkopo. Kwa hiyo, kwangu nashukuru sana kwa hili kwa sababu litakuwa limejibu majibu ya matatizo. (*Makofi*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, natoa shukrani na hongera kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tamko la kutumia fedha za *EPA* hasa kwenye mambo ya kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ndio uti wa mgongo, ni vizuri tumeona kuwa kuna umuhimu wa kukiangalia kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naleta ombi langu kuwa fedha zitakazotumika kwa pembejeo zifanyiwe mchakato mapema kabla muda wa kilimo haujapita kusudi wakulima na wafugaji wapate pembejeo kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kupata nyongeza kwenye sehemu ya kilimo na mifugo, mimi kama mdau mkuu wa Serikali na msimamizi wa maendeleo kwa wananchi ombi langu ni kuwa hata sehemu ya uvuvi ifikiriwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado hatujachelewa, hizo fedha zilizopelekwa kwenye mifugo au kilimo kwa kuwa ni kitu kimoja na uvuvi, itengwe hapo fedha kidogo angalau kwa ununuzi wa nyavu za kuvulia samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi pia ni kilimo, ni kilimo cha samaki au ni sehemu ya mifugo, kuwa kilimo cha ufugaji samaki. Kwa hiyo waangaliwe hao wavuvi kusudi nao wafurahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nasema kuwa huu uwe mwanzo, safari ijayo yaani Bajeti ijayo Wizara ya Kilimo iongezewe hela. Kilimo kipewe kipaumbele. Bila ya kuinua kilimo, hatutafika mbali. Ili kuinua kilimo chetu, lazima tukipe kipaumbele. Kwa hiyo uchumi wa wananchi wetu utaongezeka na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za *EPA* zina *stigma* ya wizi mbele ya umma, hivyo wananchi wangependa kuona fedha hizi zinatumika kwa uwazi, *transparency;* kuzipeleka kwenye sekta ya kilimo kwenye pembejeo za kilimo wakati kuna utata mkubwa wa hali ya hewa na matatizo ya miundombinu. Urasimu katika usambazaji pembejeo hizi ni dhahiri fedha hizi zitakwenda na maji na misimu ijayo wananchi watahoji fedha hizo zimeleta manufaa gani au zimetumikaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza fedha hizi ziwe *handled very carefully*' ziingizwe kwenye matumizi ambayo yataweka kielelezo (*exhibit*) kama vile kiwanda cha mbolea au hata barabara.

Kwa mfano, barabara ya Dodoma – Manyoni – Singida, barabara hii imekwama hata kufikia Konoike kuamua kujitoa. Je, ni kwa nini fedha hizo zisipelekwe kumalizia barabara hii na kuwa kielelezo cha kudumu kwamba fedha hizi zimetumika na ushahidi upo?

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi nyingi sana kwa kutuletea Muswada huu na maudhui yake. Hongera Waziri, Manaibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na watumishi wa Wizara yote. Nampongeza Rais kwa kutoa kipaumbele kwa ununuzi wa matrekta mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja, ni faraja kubwa kwa kuelekeza fedha zote katika kunyanyua kilimo. Sisi Warufiji wenye ardhi yenye rutuba nyingi, magugu makubwa na hayalimiki kwa plau au *Power Tiller*, tunahitaji matrekta makubwa mengi ili tuzalishe chakula cha kutosha na mazao mengine ya biashara. Kwa hiyo katika ardhi ngumu kama ya Bonde la Mto Rufiji, ukulima wa uhakika ni kutumia matrekta makubwa. *Power Tillers* zitumike katika sehemu ya nchi yetu yenye ardhi nyepesi kama huko Bara – toka Morogoro kuelekea Kigoma tuleteeni matrekta jamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba mabadiliko ya mgao wa fedha hizo bilioni 40 zilizopewa kilimo zisinunue mbolea tupu, vile vile sehemu kubwa inunuwe madawa ya kupulizia mikorosho yetu. Ni aibu sana kwa Wizara kuliacha zao la korosho kama yatima na kupeleka fedha zote kwenye mbolea, fedha ambazo zitatumiwa na mikoa michache tu (Iringa, Songea, Mbeya, Rukwa na labda Kilimanjaro); il-hali, mikoa ya korosho (Lindi, Mtwara, Pwani, Dar es Salaam na Tanga) wanaachwa solemba!

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha bilioni tatu iliyopangiwa *TIB* haitoshi, napenda kuiomba Serikali kuwa fedha hizo; walegeze masharti ya kukopesha, ama sivyo basi tutawanufaisha wananchi wachache tu (wenye *contacts*). Aidha, tunaomba Serikali ituhakikishie kwamba hakutakuwa na mfumo wa *import support* ambao uliwanufaisha wajanja watupu, fedha hizo zitumike kwa kununulia matrekta na wananchi wakopeshwe hayo matrekta bila upendeleo, kuwepo na tathmini ya nchi yetu yaani *inventory* ya matrekta yote na kisha Serikali ikopeshe matrekta hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. GODGREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada inagwa naona kama Muswada huu umekuja kwa kuchelewa kwa kuwa msimu wa kilimo katika maeneo mengi nchini umepita sana. Hata hivyo naomba kujua yafuatayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 21 - Hazina, kiasi cha shilingi bilioni tatu kinapelekwa Benki ya Rasilimali ya Tanzania (*TIB*). Madhumuni ikiwa ni kuongeza mtaji wa benki hiyo. Naomba nielezwe, je, Mtanzania wa kawaida hasa kutoka kule Mbozi atapataje mkopo kutoka benki hiyo ambayo ipo Dar es Salaam tu? Je, ni sifa gani Watanzania na wakulima wa nchi hii wanatakiwa wawe nazo ili wapate mkopo huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 43 - Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara imeongezewa shilingi bilioni 40 kwa madhumuni ya kuongeza ununuzi wa pembejeo. Ni jambo jema, hata hivyo nataka kujua yafuatayo:-

Je, pesa hizo zipo au tayari zimetumika kununulia mbolea ambayo imesambazwa au inaendelea kusambazwa kwa wakulima?

Je, Mkoa wa Mbeya na Wilaya ya Mbozi ambayo ni mtumiaji mkubwa sana wa mbolea nchini imefaidika kwa kiasi gani na ongezeko la fedha hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, kwa Muswada huu ambao unatokana na mahitaji ya dharura katika kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unaomba fedha za nyongeza kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo za kilimo. Nami nikizungumzia zaidi ufanisi tunaolenga katika kununua mbolea na kuifikisha kwa wakulima napenda kubaini masuala au mambo kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu katika usambazaji wa mbolea na pembejeo kwa jumla ni pamoja na usafirishaji au uchukuzi (*transportation*) wa bidhaa hii *supply chain management*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia kipengele cha usafirishaji au mchukuzi lazima tuangalie aina ya usafirishaji kama ni wa reli au barabara. Hali ya barabara zetu siyo nzuri na hata reli yetu siyo fanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo taarifa kwamba katika Hifadhi ya Taifa ya Nafaka *SGR* Iringa na Rukwa kuna akiba ya kutosha ya chakula (mahindi) lakini sehemu nyingine za nchi yetu zina njaa kubwa. Tatizo kubwa ni *logistics* au *supply chain management* iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo napenda nitahadharishe na hasa kushauri kwamba ili kufanikisha zoezi tunaloombea fedha ni vizuri Wizara ya Miundombinu na TAMISEMI zipewe fedha za dharura ili kuboresha njia za kusafirishia mbolea. Kwa mfano, mikoa maarufu kwa kilimo, Iringa, Ruvuma, Mbeya na Rukwa zitahitaji mbolea ya Minjingu Mkoani Manyara. Kwa sasa barabara inayotumika ni Minjingu – Arusha – Chalinze - Iringa ambayo ni nzuri ya lami lakini ni ndefu mara mbili ya Barabara ya Minjingu – Babati – Dodoma - Iringa ambayo ni ya changarawe na ni mbaya sana; lakini ni *shortcut* nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na observations hizo napenda kushauri kwamba mameneja wa *TANROADS* wa Mikoa ya Manyara - Dodoma - Iringa wapate fedha za kutosha kuhakikisha Barabara ya Minjingu - Babati – Dodoma – Iringa imefanyiwa matengenezo makubwa. Barabara hii iko katika hali mbaya sana. Serikali ielekeze jicho lake kwenye Barabara hii nayo (*TANROADS*) wapate fedha za nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ushauri huo naamini tutakapopitisha matumizi haya ya nyongeza ni hakika mbolea itanunuliwa na kuwafikia wakulima kwa wakati na baada ya mavuno mazao yatafika kwenye soko bila tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache hapo juu, naunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha na Uchumi kwa asilimia mia moja.

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Naipongeza Wizara kwa kuleta Muswada huu kwa wakati muafaka, hivyo nashauri pesa hizo zitumike kikamilifu kama zilivyopangiwa kununua matrekta, mbolea, pembejeo na kadhalika. Vilevile wataalam wa kilimo, pamoja na maafisa wa ugani wataajiriwa. Ninashauri ikiwezekana viwanda vya mbolea vilivyopo nchini, viimarishwe ili tupunguze gharama za kununua mbolea kutoka nje ya nchi. Tathmini za hatua zitakazofikiwa ifanyike ili kujua mafanikio na matatizo na kuweza kufanyiwa marekebisho mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia upande wa uvuvi kuwe na usimamizi wa kutosha wa kutolewa vifaa, nyenzo na kadhalika. Wataalam waongezwe. Vilevile maafisa wa uvuvi na wavuvi wenyewe, wapewe elimu ya kutosha kuhusu uvuvi haramu na hasara zake na taaluma kuhusu uvuvi wa kisasa na vyombo vinavyokubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nautakia Muswada huu, utekelezaji mwema. Nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuleta pendekezo hili na kuletwa hapa Bungeni.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Naipongeza Serikali, kwa maamuzi yake ya namna nzuri ya kuzitumia fedha za *EPA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uamuzi huu, Wizara na Taasisi zote zitakazodhaminiwa fedha hii, mambo yafuatayo yazingatiwe sana:-

Kwa kuwa tatizo kubwa la chakula linazidi kutishia nchi hii, maamuzi ya makusudi yawe ni kuelekeza sehemu ya fedha hiyo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji wa mazao ya chakula; na hasa kwa kujenga mabwawa na kuboresha miundombunu ya umwagiliaji, kama mifereji ya asili inayotumika na wakulima wadogo wadogo, wakiboreshewa na mbolea ya ruzuku itakayotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbolea hii haitakuwa na manufaa yoyote kama ugawaji wake hautazingatia masika yalivyo katika mikoa mbalimbali. Lazima Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, inafahamu mbolea ya kupandia inafaa wakati gani katika mikoa gani, mbolea ya kukuzia hivyo hivyo. Tabia ya kusambaza mbolea wakati mvua imekwisha, haitasaidia kuondoa tatizo la njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mazao ya biashara, ambayo yanatoa mchango mkubwa sana kiuchumi, fedha ambayo inaweza kununua chakula iwapo kutakuwa na

ukame. Nashauri wakulima wa chai na kahawa nao wafikiriwe kupewa mbolea ya ruzuku. Malalamiko ya wakulima na mazao haya ni makubwa kuhusu gharama kubwa za mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya wakulima ili iwe na manufaa, ipitie katika vyama vya ushirika ambavyo ni vyombo vya fedha vilivyo na mkulima. Udhibiti mkubwa unatakiwa sana katika kusimamia mikopo hii ili iwe na manufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya mafuta Duniani ilipopanda na bei ya mbolea ilipanda. Kwa sasa bei ya mafuta imeteremka, lakini bei ya mbolea bado iko juu. Kama tulivyojifunza, wakati makampuni ya mafuta walipokuwa wamekataa kuteremsha bei mpaka *EWURA* walipoingilia kati, vilevile makampuni ya kuuza mbolea wanaweza kubakiza bei ya mbolea kuwa *artificially* juu. Hivyo, Serikali inabidi kufanya juhudi ya kujua gharama ya mbolea *at source*, ili kuweza kudhibiti bei ya mbolea kwa makampuni ya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuboresha zana za kilimo limeonekana ni muhimu sana, kama nchi yetu inahitaji kuongeza wingi wa mazao, pamoja na njia nyingine za kuongeza tija. Zana za kilimo ni pamoja na vitendea kazi kama matrekta. Utaratibu wa kununua zana hizi, unabidi kuwa na utaratibu rasmi, ambao unaweza kuwa rahisi kwa wananchi kuuelewa. Hivyo, uwezeshaji au mikopo ya vifaa hivi inabidi kutoka kwa taasisi rasmi, ambayo itakuwa na uwezo wa kufuatilia urejeshaji wa mikopo hii. Kwa sababu hiyo ni vyema bajeti ya zana za kilimo, itengwe maalumu kutoka kwenye mafungu ya madawa na mbegu ilipojumuishwa kijumla jumla. Ikiwezekana, fungu lililotengwa kwa ajili ya zana za kilimo, liunganishwe na shilingi bilioni tatu zilizotengwa kwa ajili ya *TIB* na fedha itakayopatikana kutokana na Agizo la Rais la kufuta mafungu ya kununua magari Serikalini na mafungu ya kusimamia semina. Kwa kufanya hivyo, bajeti ya zana za kilimo, itakuwa kubwa ya kutosha kuonyesha *impact* katika mkakati alioutangaza Mheshimiwa Rais wa kuongeza zana za kilimo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pesa kuwekwa kwenye maeneo ya tija, shilingi bilioni 53 si nyingi sana katika kutoa mapinduzi ya kilimo, kufuatia kuwa nchi yetu ni kubwa. Ili pesa hiyo iwe na *impact*, badala ya kuisambaza kidogo kidogo nchi nzima, ingekuwa na manufaa kama ingeelekezwa kwa mikoa, wakulima au wafuagaji waliokwishajiandaa ili iwe mfano wa kuonyesha kilimo au ufugaji wa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaweza kuwa mfano wa kuondokana na mfumo wa kusambaza kitu kidogo kwa wengi, mwisho wake mafanikio yaliyotarajiwa hayapatikani na hakuna anayeridhika na kila mmoja analalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango wangu huu, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudi na hatua mbalimbali anazochukua, kuhusiana na kuboresha ustawi wa jamii ya watu wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii, kueleza kuwa, kumsaidia Mheshimiwa Rais, kupo kwa aina nyingi na kumpenda hivyo hivyo. Ni mara chache sana watu huwapenda watu wanaojaribu kutoa michango, ambayo inalenga kuchokoza ili kuongeza utashi wa kufikiri na hivyo kujipanga vizuri zaidi. Ndio maana hata Mungu alimuuliza Musa, mbona uko hapo hapo; yaani kwa nini hutaki kubadilika ili uone na mazuri mengine?

Hivyo basi, pesa hizi naamini zitapangiwa mipango mikakati mizuri na sio ile ya kimazoea ili kuleta mabadiliko halisi ya kilimo, ufugaji na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kawaida, kwa Bunge hili kuuliza swali au kupewa ahadi mfu, isiyo na uhai kwani haitekelezwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara ya mwisho nilimwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Ufagaji na Uvuvi, Mheshimiwa John Magufuli, kuhusu maombi ya boti katika Kata ya Kihagara au Liuli; sasa mwaka karibu unaisha hakuna boti lolote lililopelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, alizungumzia sana juu ya umuhimu wa kuwawezesha wavuvi na tabu waliyonayo. Sasa tunahisi Wizara hii, inakumbuka ufugaji zaidi kuliko uvuvi na huenda uvuvi kama ilivyo ada, ukadumaa kutokana na kumezwa na ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, nashauri tafadhali katika pesa iliyotengwa, angalau kidogo iende kwenye uvuvi hususan ununuzi wa boti kama ilivyoahidiwa kwenye bajeti ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, pesa hizi zina macho makubwa ya watu na zinamjenga vizuri Mheshimiwa Rais wetu, pamoja na Serikali yetu, basi ni vyema zitumike vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na kuunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii, kuipongeza Serikali ya CCM, kwa maamuzi mazuri ya kupeleka Sh. 50,000,000,000 kwenye kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais ni mtu mwenye busara sana, alipoona fedha za *EPA* zimerudishwa, aliagiza fedha hizo zipelekwe katika kilimo. Nampongeza sana Rais, ninasema ameona umuhimu wa kilimo, ukizingatia kilimo ni uti wa mgongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashangaa watu wengine wamedakia na kusema wao walisema; nawauliza walisema kama nani na kwa kutumia ilani gani? Je, n wao wana Serikali waseme eti fedha hizi ziende katika kilimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania ni ya CCM, ina ilani yake, ambayo ndiyo dira ya ushindi 2005. Hivyo basi, Serikali ya CCM ni makini. Lengo la fedha hizi za *EPA* kupelekwa katika kilimo, tusiwapotoshe wananchi, tumpongeze Mheshimiwa Rais na Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri mambo yafuatayo: Mgao wa pembejeo na mbolea uwe sawa na uwe katika mikoa inayozalisha mazao ya mahindi, pamba, korosho na kadhalika. Mgao wa pembejeo na dawa, uwekewe mpango maalum kwa maeneo maalum ili kilimo kibadilike. Benki ya *TIB* iweke matawi mikoani ili wakulima wengi waweze kunufaika na mikopo toka katika Benki hii au wawasiliane na *NMB* ambayo maeneo mengi ipo. *TIB* itumie *SACCOS* kuzikopesha ili wananchi au vikundi vingi viweze kukopeshwa na pia fedha hizi watanufaika wananchi wengi zaidi kwa kupitia *SACCOS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa hotuba ya tarehe 31 Januari, 2009 ya kuona umuhimu wa kupunguza manunuzi ya magari aina ya *GX*, *TX*, sasa Serikali itatenga fedha kwa manunuzi ya matrekta. Hii ni dalili nzuri ya kuwajali wakulima. Naomba aendelee na kuona wavuvi nao waandaliwe vizuri, wakopeshwe mitumbwi yenye *engine* ili wazalishe na umaskini uwatoke, hasa wavuvi wa Wilaya za Ukerewe, Magu, Sengerema na Ilemela.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia kheri Waziri wa Kilimo na Mifugo, hizi fedha zilenge kazi husika si vinginevyo; nitasikitika kama fedha hizo zitatumika kwenye posho, semina na warsha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Rais wetu, kwa kuamua fedha za *EPA* ziende kuwasaidia wakulima na wafugaji. Pili, nampongeza Waziri wa Fedha, Manaibu wake, Makatibu Wakuu na Watendaji wote, waliohusika kuandaa Muswada huu na kuletwa hapa Bungeni kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali izingatie Azimio la Arusha kwamba, siasa ni kilimo na kwa wakati huu siasa ni uchumi endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwekeze katika kujenga viwanda vya mbolea hapa nchini, ili kuepuka kuagiza mbolea nje. Hali hii inamnufaisha mfanyabiashara badala ya mkulima na gharama za kila mwaka zisizoleta manufaa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali na wadau iagize matrekta mengi, yenye teknolojia rahisi ili wakulima wengi, vyama vya ushirika vya wakulima na *SACCOS*

wapatiwe kwa lengo la kuleta tija katika kilimo na mapinduzi ya kijani yawe endelevu na yenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ijikite kwa kupeleka nguvu maeneo machache kama Mkoa wa Morogoro, uzalishe mazao ya chakula kama alivyosema Mheshimiwa Rais, Morogoro uwe ghala la chakula la nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya umwagiliaji iwe kwa vitendo na kwa maeneo machache makubwa, kuliko kuwa na mabwawa mengi madogo madogo yasiyokuwa na tija, hali ambayo huzaa hisia mbaya kwa wananchi wetu, vitu vionekane.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwakopeshe vyama vya akiba na mikopo vya wavuvi, zana za uvuvi kama boti za uvuvi na nyavu, kwa kuzingatia ushirika wao ili huduma hii au fedha hizi, ziwafikie wavuvi wengi zaidi kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ijikite kununua vifaa (zana), kama matrekta, boti, nyavu na zana mbalimbali za kilimo ili wananchi wapewe zana hizi au vifaa, mashine, boti na kadhalika, kuliko kuwapatia fedha. Serikali ikiagiza kiasi kikubwa na gharama za zana hizo au vifaa itakuwa nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Serikali izingatie yafuatayo: Azimio la Iringa liende kwa Ari Mpya, Nguvu na Kasi Mpya, kwa kuzingatia changamoto za sasa. Fedha za mbolea zipelekwe kwenye kujenga viwanda vya mbolea, kuliko kupeleka kiasi kikubwa kwenye mbolea ambayo kila mwaka kuna bajeti yake. Serikali ijenge miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji kwenye maeneo machache, ambayo yataleta tija kwa kuanzia Mkoa wa Morogoro. Serikali vilevile iagize matrekta, boti kwa wingi, ili iwakopeshe vyama vya ushirika, wakulima na wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada huu, lakini nasisitiza uzalendo mbele. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri Mustapha Mkulo, Manaibu wake na Watendaji wote wa Wizara, chini ya Katibu Mkuu Ndugu Ramadhani Kijja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa busara yake aliyoitumia juu ya maamuzi ya fedha hizi za Madeni ya Nje (*EPA*), ambazo zilirejeshwa baada ya kuibiwa na kuelekeza zitumike katika sekta hizi za kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawazo na maelekezo ya Rais ni mazuri sana, kwani amezingatia kuwa pato kubwa la Mtanzania lipo katika sekta hizo. Pamoja na mawazo mazuri ya Rais, ningeomba niuboreshe kidogo Muswada huu ili matumizi ya fedha hizi yawe ya ufanisi na yasiwe ya hasara. Sote tunafahamu, sasa tupo katika robo tatu ya mwaka wa bajeti 2008/2009; ni vyema pakawepo tahadhari katika kuzitumia fedha hizo,

kwani inawezekana kabisa kuziwekeza sasa wakati msimu wa mvua za masika unaelekea ukingoni. Sote tunafahamu, nchi yetu kwa eneo kubwa inategemea mvua za kubahatisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo uwezekano wa kupata hasara na baadaye fedha hizi zikawa hazina tija na hivyo, kuliletea Taifa hasara. Kwa kuwa fedha hizi sio zetu, watakapopatikana wenyewe tutalipa deni lililo na hasara kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima ifanyike *review* kuhusiana na bajeti ya awali, kuhusu fedha za mbolea, kwa kiwango kipi zimefanya kazi katika hatua hii ya awali. Kufahamu hilo kutasaidia kwa hatua za sasa katika matumizi ya fedha hizi (*impact*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri aelewe katika fedha hizo bilioni thelathini, ambazo zimelekezwa katika mbolea ya ruzuku, itatumika katika mikoa minane tu. Je, ni vipi mikoa iliyosalia itafaidika na fedha hizi za *EPA*? Ni vizuri ungeandaliwa utaratibu wa fedha hizi kugusa kila mkoa. Mikoa kama Singida, Dodoma, Tabora, Shinyanga na kadhalika, ingetengewa kupitia fedha hizi kuimarisha miundombinu ya kilimo hasa ile ya umwagiliaji.

Kwa maana hiyo, ingemegwa bilioni kumi nyingine ikapatiwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kwa kazi hiyo hiyo ya kilimo, kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji, ambayo inalo jukumu la miundombinu inayotumika kwa kilimo. Kutokuipatia Wizara ya Maji na Umwagiliaji fedha hizi ni sawa na kutoishirikisha katika mgawo mikoa niliyoitaja katika fedha za *EPA*. Namwomba Waziri, wakati wa majumuisho basi aone haja ya umwagiliaji kupewa fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni utaratibu upi utakaotumiwa katika kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima wadogo wadogo hasa wale wanaotumia jembe la mkono, wanyama kazi, kutoka katika kilimo hicho na kwenda kwenye matumizi ya *power tiller*, *tractor* na kadhalika? Fedha hizi zikiwekwa kwenye Mfuko wa Pembejeo, bado haitakuwa sawa kwani takwimu zinaonyesha Mfuko huu kushindwa kumfikia mkulima mdogo mdogo na badala yake imeonekana ni Mfuko wa wenye nacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yangu hizi *power tiller* au *tractors* zipelekwe moja kwa moja kwenye Halmashauri za Wilaya, ili sasa wakulima iwe rahisi kufanya mawasiliano ya taratibu za mkono na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi bilioni tatu zilizotengwa kwa ajili ya mikopo ya wakulima kwa Benki ya *TIB*, bado zina mgogoro kwani utaratibu wa Benki hii unajulikana Dar es Salaam peke yake. Tutafanya vipi fedha hizi ziwafikie wakulima wenye nia, walio mbali na maeneo ya Dar es Salaam au wasiojua utaratibu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri busara ingetumika juu ya uanzishaji wa Benki ya Wakulima, badala ya kuziweka *TIB*. Yawezekana kabisa fedha hizi kukopwa na watu wasio wakulima, lakini wakijivalisha joho la ukulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya nyongeza hii ya bajeti, lakini kwa ufafanuzi wa hoja zangu.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizipongeze kwa dhati, jitihada anazozionyesha Mheshimiwa Rais wetu za kutaka kuipeleka nchi kwenye Mapinduzi ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazipongeza pia jitihada za kuhakikisha fedha za *EPA* zinarudi na kutumika katika sekta hizi mbili muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, asilimia themanini ya Watanzania, hujishughulisha na sekta hizi mbili (kilimo na mifugo). Hivyo basi, jitihada za kuongeza bajeti ya Wizara hizi ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo kwa wakulima imekuwa ni kilio cha muda mrefu, niiombe benki hii ya (*TIB*) itoe masharti nafuu ili wakulima wetu waweze kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapinduzi ya Kilimo katika nchi yetu, yatawezekana tu pale tutakapoondoa dhana hii mbovu ya siasa ni kilimo na kuweka dhana mpya isemayo kilimo ni kupanga!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhana hiyo hapo juu ni vizuri tukaainisha mikoa michache yenye mvua za kutosha na kuifanyia mikakati kabambe ya kilimo, kuhakikisha miundombinu katika mikoa hiyo inaboreshwa, vilevile ipatiwe pembejeo za kutosha. Binafsi, nina imani kwa mpango huo, mikoa hiyo itaweza kulisha mikoa mingine yote ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini si mikoa yote hujishughulisha na kilimo, kwani ipo mikoa mingine hujishughulisha na ufugaji; hivyo, nashauri katika ongezeko hili, tuache siasa na tupange namna nzuri ya kujielekeza kwenye mapinduzi ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuanzisha/kurudisha michepuo ya kilimo kwenye sekondari zetu ni muhimu, kwani wataalam wa kilimo watapatikana kwa njia hii, ambapo wanafunzi wote wa mchepuo huu watachaguliwa *direct* kwenye vyuo vya kilimo kwa ajili ya *certificate course*.

Mheshimiwa Spika, hata sekta hii ikiongezewa fedha nyingi ni vigumu kufikia tunapopataka bila ya wataalam hawa. Iainishwe mikoa yote inayotumia mbolea na ndiyo pekee ipewe mbolea na si kuipoteza mbolea hiyo katika mikoa ambayo haiitumii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vyetu vya utafiti vya kilimo navyo viboreshwe na kuhakikisha majibu/maoni yatokanayo na tafiti hizo yanawafikia wakulima, mfano, mbegu za mazao ya muda mfupi, ustawi wa aina za mazao katika hali tofauti za hewa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni muhimu kuzingatia mara kwa mara, Taarifa ya Idara ya Hali ya Hewa, kwani imebainika nchi yetu inaingia mara kwa mara katika janga la njaa, kutokana na tatizo la kutokuzingatia mabadiliko ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuunga mkono Muswada huu, ambao kwa kiasi kikkubwa, una lengo la kuboresha na kuinua uchumi wa wakulima wetu pamoja na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia hoja hii kwa kuangalia eneo la kwanza la Muswada huu, linalohusu matumizi ya nyongeza ya shilingi bilioni 40 kwenye sekta ya kilimo. Malengo makuu ya kutumia fedha hizo ni kununulia pembejeo za kilimo (mbolea) na kununulia zana za kilimo (matrekta madogo - *power tillers*).

Mheshimiwa Naibu Spika, sina pingamizi yoyote kuhusiana na ununuzi wa mbolea; hili ni jambo zuri ambalo litasaidia sana kuongeza mazao ya wakulima. Lakini ni vizuri Serikali ikafuatilia kwa karibu, namna ya kufikisha mbolea hizo kwa wakulima na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri kuwa, kwa maeneo ambayo mbolea hiyo itapelekwa usimamizi mzuri wa kugawa mbolea hiyo uwepo ili wakulima wote wapate. Aidha, kwa maeneo ya mikoa inayolima korosho ni vizuri pembejeo hizo zikafika katikati ya mwezi Mei, ili ziweze kupulizia mikorosho mwanzoni mwa mwezi wa Juni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ununuzi wa matrekta madogo (*power tillers),* binafsi siridhiki na ununuzi huo peke yake. Kwa muda mrefu, tulikuwa tunaishauri Serikali inunue matrekta ili yaweze kutumika katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Nchi hii ina ardhi zinazotofautiana, kuna maeneo mfano ya Wilaya ya Rufiji, ardhi yake inayofaa kwa kilimo ni ngumu sana kiasi ambacho matrekta madogo (*power tillers*) hayawezi kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata baadhi ya matrekta yenye *horsepower 50,* hayalimi katika ardhi hiyo ambayo ina rutuba sana, kutokana na kushindwa kupenya kwa majembe yake kwenye udongo huo. Kutokana na hilo basi ni vizuri Serikali isinunue *power tillers* peke yake, bali pia inunue na matrekta makubwa, ambayo yatafaa katika ardhi ya Rufiji na baadhi ya maeneo ambayo yana udongo mgumu kama Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ununuzi huo, ningependa kushauri kuwa ni vizuri mgawanyo huo ukazingatia pia mahitaji ya matrekta hayo katika kila mkoa na wilaya. Kwa mfano, hadi sasa Wilaya ya Rufiji ambayo ina eneo kubwa sana la kilimo, zaidi ya kilometa za mraba 4000.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili linalofaa kwa kwa kilimo, hasa cha mazao ya chakula; mpunga, mahindi na kunde, pia linafaa sana kwa kilimo cha pamba na

miwa, kama mazao ya biashara. Kati ya kilometa zote hizo, eneo linalolimwa kwa sasa ni dogo sana, chini ya asilimia tano. Hii inatokana na ukosefu wa matrekta katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, napenda kuishauri Serikali, kuipa kipaumbele Wilaya ya Rufiji, kwa kununua matrekta makubwa na siyo *power tillers* iliyoweza kuinua mapato ya Wakulima wa Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaomba kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa uamuzi wake wa kuelekeza kiasi cha pesa zitokanazo na pesa za *EPA* zielekezwe/zitumike kuinua kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu Mawaziri wake, pamoja na Watendaji wote, kwa kuitikia wito huo wa Mheshimiwa Rais na kutuletea Muswada huu mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii, pamoja na mapendekezo ya matumizi yake, ila ninaomba nishauri mambo machache yafuatayo:-

Kwa kuwa Mwenyezi Mungu ameendelea kutujalia kuwa na gesi asilia, ambayo ni kitu muhimu sana katika utengenezaji wa mbolea, ninashauri tuazimie kujenga kiwanda/viwanda vyetu vya mbolea, kwa ajili ya matumizi yetu ndani ya nchi na hata kuuza nje ya nchi. Kwa kuwa Benki ya *TIB* hijaenea katika maeneo mengi hapa nchini, ninapendekeza kuzitumia Benki za *CRDB* na NMB ili kuzifikia *SACCOS* kote nchini, ambazo ndio zipo karibu sana na walengwa, yaani wakulima wadogo na wa kati na wanatambuana vizuri; ikiwa ni njia mojawapo ya uhakika wa kurejesha mikopo.

Katika eneo la maendeleo ya mifugo na uvuvi, ninapendekeza kiasi cha pesa zitumike katika kuweka mizani katika minada ya mifugo yetu ili wafugaji wetu nao wasiendelee kuibiwa na wafanyabiashara (yaani rumbesa kwenye mifugo). Ninapendekeza kama kitakuwepo kiasi kingine cha pesa kwenye Mfuko Mkuu, basi zielekezwe katika miundombinu ya barabara, kwani uzalishaji bila barabara hapatakuwepo na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Mawaziri na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi kubwa wanazozifanya za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya *TIB* ilipewa pesa za *EPA* zilizorejeshwa ili benki hiyo iweze kuwakopesha wakulima nchini na sasa Serikali inaiomba Bunge lako Tukufu, kuidhinisha shilingi bilionii tatu kuiongezea TIB mtaji ili benki hii iendelee kutoa mikopo kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hofu yangu kubwa ni kwa namna gani mkulima wa mikoa ya mbali kama vile Mwanza, Kigoma, Mtwara, Kagera, Mara na kadhalika, watakavyoweza kunufaika na mikopo itakayotolewa na Benki ya *TIB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya *TIB* ipo Dar es Salaam na haina matawi mikoani; hivyo, huduma za benki hii siyo rahisi kuwafikia wakulima walio wengi. Nachelea kusema kuwa, mikopo kutoka *TIB* itawafaidisha wachache na hasa wananchi wanaoishi Dar es Salaam na mikoa ya jirani. Serikali iangalie utaratibu muafaka wa benki hii kutoa huduma zake nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni uamuzi wa busara, Serikali kutenga shilingi bilioni kumi kwa ajili ya ununuzi wa zana za kilimo. Nashauri matrekta madogo yanayotarajiwa kununuliwa, yasambazwe mapema kwenye Halmashauri zetu ili kuwahi msimu wa mvua unaoendelea. Pia ningependa kujua kama zana hizo za kilimo zitatolewa bure kwa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa mchango wangu kuhusu Muswada uliowasilishwa na Wizara ya Fedha, napenda kusema kuwa ninaunga mkono hoja hiyo kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuunga mkono hoja hiyo, napenda kugusia baadhi ya vipengele kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huo hakuna fedha ambazo zimepangwa kwa ajili ya kuwapa *support* wavuvi, kwa mfano, shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika zinawawia ngumu kutokana na vifaa vya kizamani, ambavyo wavuvi hao wadogo wadogo wanatumia. Kwa mantiki hiyo, ninashauri uwepo mpango mahususi wa kuboresha uvuvi kwa watu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo ambalo linaweza kujitokeza, endapo usimamizi wa fedha hizo hautakuwa wa kutosha. Upo uwezekano mkubwa wa fedha hizo kuyeyuka kama fedha za Rais Jakaya Kikwete, ambazo hazikuwafikia wananchi kutokana na usimamizi mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwepo na usimamizi mzuri ni vyema fedha hizo zikakabidhiwa Wakuu wa Mikoa, ambao watakuwa wanazitoa kufuatana na watakavyoridhishwa na matumizi ya fedha hizo kwa kuwafikia walengwa.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais, kwa kupeleka fedha iliyopatikana kutoka kwa wadaiwa wa *EPA* kwenye kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu ni kuwa, je, fedha hiyo kupitia ruzuku ya mbolea na ununuzi wa madawa ya mifugo, wakulima wenyewe wanatarajiwa

kunufaika na fedha hiyo kwa kiwango gani? Je, mbolea sasa itapatikana kwa wakulima kwa kiasi gani ukilinganisha na faida itakayopatikana kwa wafanyabiashara? Ni vyema bei ya mbolea na madawa vikajulikana, japo kwa wastani kutokana na ongezeko la fedha hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi kirefu, ruzuku ya mbolea imekuwa ikielekezwa kwenye mikoa kadhaa tu. Je, ruzuku hiyo inawanufaisha namna gani wakazi wa mikoa iliyo mbali na mikoa inayopatiwa ruzuku ya mbolea, hasa ukizingatia ukweli kuwa mikoa mingi ipatayo ruzuku iko mipakani na mara nyingi huuza mazao yao nje ya nchi na safari nyingine kwa njia ya magendo? Ni vyema utaratibu bora zaidi ukaandaliwa wa kuinufaisha nchi nzima kutokana na ruzuku zitolewazo kwa makundi yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inayo shida kubwa ya maji kwa wananchi wetu, kama fedha hizo bilioni 53 zingalikusudiwa kuchimba visima virefu; je, ni visima virefu vingapi vingalichimbwa kwa kila kijiji kisima kimoja?

Je, asilimia ngapi ya wananchi wetu wangaliweza kupata maji safi na salama?

Je, tungalitekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005 kwa kiwango gani?

Je, ni matokeo yapi yanayopimika tunayoyatarajia kutokana na mabadiliko haya ya bajeti?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, namtakia Mheshimiwa Waziri, utekelezaji mwema wa mabadiliko haya ya bajeti. Ninaunga mkono hoja hii, mimi binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wangu.

**MHE. DKT. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niipongeze Serikali kwa kuona umuhimu wa kutumia pesa za *EPA,* zinazorudishwa kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, matumizi ya fedha kununua mbolea na madawa ya mifugo, yamepititwa na wakati katika maana kuwa msimu wa kilimo cha mazao yanayohitaji mbolea (mahindi), kwa mwaka huu unafikia ukingoni. Mbolea haihitajiki tena kwa mwaka 2008/2009 na haitunziki kwa muda mrefu. Hata kama pesa itatumika kuongeza mbolea, je, nyongeza hiyo itadumu katika Bajeti zijazo za Wizara ya Kilimo? Bila hivyo tutakuwa tunafanya kitu kisicho endelevu, hata madawa ya mifugo, msimu wa usambazaji ulishapita. Pia hiaeleweki kama Bajeti zijazo za mifugo, zitazingatia ongezeko hili na pesa za ruzuku kwa madawa ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri yafuatayo:-

Pesa hizi nyingi zipelekwe kwenye mfumo wa matumizi endelevu, yaani kukopwa, kurudishwa na kukopwa tena (*re-cycling expenditure*). *TIB* ingepewa kwa mfano si chini ya shilingi bilioni 30, kwa ajili ya kukopesha uwekezaji katika sekta ya mifugo, hususan kilimo, viwanda vya nyama na mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafahamu kuwa, wawekezaji wabia wa Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga, hawajajiondoa kwenye mradi huo, bali wamechelewa kupata pesa kwa upande wa wabia kutoka nje, kutokana na matatizo ya uchumi ya Dunia kwa upande wa mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingekuwa busara basi kwa wabia wa kiwanda hicho wa hapa nchini, kupewa fursa ya kukopa pesa kutoka *TIB* ili kuwezesha kiwanda kukamilishwa na kuanza kazi. Zinahitajika shilingi bilioni 6 – 8 tu kuwezesha hili. Watanzania wabia wa kiwanda, wakopeshwe pesa hiyo kupitia *TIB*. Wabia wa nje, wataleta mtaji mkubwa zaidi pindi uchumi/mabenki yakikaa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanza kufanya kazi Kiwanda cha Nyama Shinyanga, kutawezesha kuimarisha uvunaji wa mifugo mingi tuliyonayo, upatikanaji wa nyama bora, kuongeza mauzo ya nyama nje, kuongeza uzalishaji wa ngozi bora, kuongeza mapato ya Serikali na wananchi, pamoja na ongezeko la ajira nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji katika Viwanda vya Maziwa, pia wangeweza kukopa pesa hizi kupitia TIB. Vivyo hivyo shilingi bilioni 10 zingeweza kutengwa kwa ajili ya kukopeshwa mwekezaji ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, natumaini nimeeleweka kuwa, matumizi makubwa ya pesa hizi yawe kwenye maeneo yanayowezesha kuzitumia kwa muda mrefu na kuleta matunda mengi zaidi (*sustainable use of funds for sustainable returns*).

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Wabunge waliotangulia, kukipongeza Chama cha Mapinduzi, kwa ushindi mkubwa wa Kiti cha Ubunge Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii ya matumizi ya ziada katika Bajeti hii ya mwaka 2008 – 2009 ni ya kupongezwa sana. Hii ni ahadi iliyotekelezeka, baada ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuthubutu mapema kuwafahamisha wananchi kwamba, fedha hizi za *EPA* zikirejeshwa, zitarudi kuboresha kilimo na pembejeo zake, pamoja na kuelekeza uanzishwaji wa benki ya kuendeleza kilimo. Kupitia zoezi hili gumu na la kiungwana, mimi pia nawapongeza waliosikia wito wa kurejesha fedha za *EPA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwanzo wa safari ya maendeleo, basi tayari tumeanza kwani katika hizo nchi zilizoendelea, kuna benki za kilimo, viwanda, madini na kadhalika. Hivyo, sisi kwetu tumeanza na kilimo kwa mtaji wa shilingi bilioni tatu. Wajibu wetu ni kuutunisha Mfuko huu mpaka pale wakulima wetu ambao ni asilimia 70 watanufaika. Mimi nasisitiza kwa hili, uwekwe mkazo kwa walengwa wa mkopo huu,

kupatiwa elimu ya kilimo cha kisasa na ikiwezekana kuhakikishiwa maji katika mashamba yao, kama ilivyoelekezwa hivi karibuni Sera ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini sisi Watanzania tukiamua kukiendeleza kilimo kama tulivyoanza, tunaweza kujitegemea kwa chakula na hata kutengeneza bajeti yetu, kwa sababu ardhi tunayo ya kutosha tena iliyorutubika; maji tunayo ya kutosha yaliyo chini ya ardhi na yanayotiririka bure bila matumizi maalum; lakini pia wataalam waliobobea tunao wa kutosha, cha msingi hapa ni maamuzi tu. Katika pembejeo, mimi nashauri kutokana na ughali wa matrekta, hivi sasa tusianze kwa vishindo kwani hizi *power tillers* zinatosha kabisa na baada ya muda mfupi tutanunua matrekta makubwa kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya yote hayo, pia tubadilike kwa kuhamasisha kilimo kwa njia ya uelimishaji kupitia television zetu hasa hii ya Taifa, badala ya fleva mchana kutwa. Lazima tuige nchi zinazofanya vizuri kama China, ambayo kila dakika moja unapata elimu ya kupiga hatua kimaendeleo katika kilimo, ufugaji, tiba na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi bado namuunga mkono Balozi Sato wa Japan aliyeondoka nchini, kwa kuaga na kusema, Tanzania bila kuelekeza nguvu zenu katika kilimo, mtaendelea kutoa lawama katika uchumi wenu na viongozi wenu. Ilikuwa Morogoro katika *Pilot Project* ya *Rice Irrigation*. Hivyo, tumepata *formula* tuitumie, tuwajibike, tutajikwamua na hatimaye kumaliza dhiki zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa Serikali kupeleka fedha kiasi cha shilingi mbilioni 53 zilizotokana na marejesho ya fedha za *EPA* ni uamuzi wa msingi. Kiasi cha fedha kinachoongezwa mtaji Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*), kwa ajili ya mikopo kwa wakulima ni dhahiri kwamba, benki hii sasa itaanza kutoa msaada mkubwa kwa wakulima wetu, ambao wameshindwa kujikomboa kutoka kwenye jembe la mkono na hivyo kuendelea kuwa maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, bado Serikali isimamie vizuri utoaji wa fedha hizo ili wakulima wanufaike na mikopo hiyo. Wafanyabiashara wasije kuzichukua kwa nguvu kubwa waliyonayo, kama ilivyotokea kwenye mabilioni ya Rais Jakaya Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, fungu la 43, shilingi bilioni 40 kuongezwa katika Mfuko wa Ruzuku ya Mbolea kwa ajili ya pembejeo za kilimo. Kwa muda wote, mbolea ya ruzuku imekuwa haisaidii au kunufaisha walengwa. Serikali imekuwa inawapa wafanyabiashara wafanye wafanyavyo kujinufaisha wao na bila Serikali kufuatilia. Mbolea hiyo ya ruzuku inatolewa kwa bei ya soko kwa wakulima hao, wanaonufaika ni wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejiandaa vipi kwenye mgao wa pembejeo hizi za kilimo zinazoelekezwa hapa, kuhakikisha kila mkoa wakulima wake wanafaidika na fungu hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, fungu 99 shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kununua madawa ya mifugo. Kuna utaratibu gani endelevu wa kuhakikisha wafugaji watanufaika na fedha hizi? Isingekuwa wazo la busara kwa Serikali, kuwekeza fedha hizi kujenga Kiwanda cha Nyama kwenye mkoa mmojawapo ili kuongeza soko la mifugo na kuongeza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hofu yangi ni kwamba, Watanzania wengi na haswa viongozi watendaji siyo wazalendo. Kama Serikali haitakuwa makini sana fedha zote hizi zitaishia mifukoni mwa wachache na kuwaacha wananchi Watanzania kuendelea na maisha magumu.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu wangu kutokana na utoaji na usimamizi wa mbolea za ruzuku Mkoani Iringa, hususan Wilaya ya Ludewa; wakulima waliotarajiwa katika zoezi hili hawakuandaliwa. Mwanza ilikuwa yatima, wajane na wasiokuwa na uwezo wa kulima na kuzalisha, mawakala ndio waliofaidi sana kwa kuwadanganya na kuwaibia Wananchi maskini. Mbolea iliwafikia wakulima kwa kuchelewa, bei za mbolea hazikueleweka, malengo ya kuzalisha chakula cha kutosha hayatafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yangu ni kama ifuatavyo: Kwa vile mbolea hufika kwa kuchelewa, mkazo uwe kwenye matrekta. Bei za mbolea na majukumu ya mawakala yafafanuliwe. Vilevile uvuvi wafikiriwe katika mgao huu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nataka niunge mkono hoja iliyowasilishwa jana na Mheshimiwa Mustafa Mkullo, Waziri wangu wa Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuunga mkono hoja hii nina nukuu kama tatu, nne, naomba nichangie. Kwanza, nataka niseme kimsingi Serikali inakubali kwamba nchi yetu Tanzania ni kubwa na kimsingi Serikali inakubali kwamba nchi yetu bado ina matatizo mengi hasa ikiwemo ile ya miundombinu. Kadhalika kupanga ni kuchagua, wakati tulipokuwa tunawasilisha bajeti mwaka jana ndugu zangu Wabunge watakubaliana nami kwamba tulikuwa tuko kwenye *crisis* ya chakula. Siyo kwa Tanzania tu lakini ilikuwa ni dunia nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, *crisis* ile iliyotokana na kupanda kwa bei ya mafuta ilifikisha bei ya mbolea kutoka dola 250 kwa tani hadi kufikia bei ya mbolea dola 1250 kwa tani. Tumemaliza bajeti fedha ile ambayo tuliyowawekea Wizara ya Kilimo kwa maana ya kwamba kusaidia wakulima kutoa ruzuku haikuweza kutosha na kufanyakazi ambayo tulikusudia katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika hali ya chakula duniani bado siyo nzuri. Ziko nchi tayari zimeshazuia, haziuzi tena chakula nje. Ndio kwa maana Serikali imeketi kwa kina na kuliangalia suala hili na kuona kwamba kuna haja kubwa ya kuzalisha chakula ndani ili tuweze kukidhi haja yetu ya chakula. Hali hii ya kupanda kwa chakula Waheshimiwa Wabunge imepelekea mpaka mfumko wa bei kufikia asilimia 13. Ukiuchambua mfumko wa bei utaona kwamba zaidi ya asilimia 50 unachangiwa na mazao ya chakula. Kwa maana hiyo sisi kama Wizara ya Fedha tunaelewa kabisa kwamba matatizo tunayo mengi, lakini lipi lianze mwanzo tupeleke miundombinu ya umwagiliaji au tule chakula? Lipi linaweza likasubiri barabara au njaa? Ndiyo kwa maana katika mipango yetu baada ya kujitokeza hizo fedha tukaona kwamba hebu tujinusuru katika hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumezipeleka kilimo fedha hizo bilioni 40 kwa dhamira hiyo. Tunaelewa kabisa kwamba huyu mkulima lazima tumwezeshe ili akue na hatimaye aweze kwenda katika mikopo. Leo mikopo hakuna hatumwezeshi tutakula? Jibu rahisi hatutaweza kula. Lakini tumefanya hivyo kwa kuzingatia na wao wanafanyaje. Naomba ninukuu au nitoe mfano wa nchi moja. Mkulima wa Malawi yuko nyuma kuliko mkulima wa Tanzania, Serikali yake ya Malawi inatoa ruzuku asilimia 90, sisi tunatoa asilimia 40 kumsaidia huyu mkulima ili kesho mkulima huyu awe na uwezo wakati huo huo tumeshamfungulia dirisha la kukopa. Tunamwambia mkulima tumekusaidia uwezo sasa unao, dirisha tayari lipo kakope. Hiyo ndiyo dhamira ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa nini vile vile nataka niseme tumeweka bilioni 10 kwa ajili ya madawa ya mifugo. Leo Tanzania ina soko nje ya ng'ombe na nyama ya ng'ombe kwa sababu mifugo yetu ni mizuri. Tukiacha hii mifugo bila kuwa na madawa ya kuitibu hili soko tutalipoteza. Tunahitaji *sustainability* ya hili soko. Kwa hiyo, Serikali ikaona kwamba ni vema kuweka hii bilioni 10 ili iweze kusaidia katika kuendeleza hili soko letu la mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelewa bilioni tatu ni kidogo na ni azma ya Serikali kuongeza zaidi *TIB* ili tuwe na dirisha ambalo litakaloweza kuwasaidia, dirisha la wakulima. Tunasema hatutachanganya zile za maendeleo na za wakulima. Ukichanganya kwa sababu benki siku zote wana *principle first come first serve* watashindwa na wafanya biashara wengine. Tunataka kuwa na dirisha kwa ajili ya wakulima na tumesema kwamba hizi bilioni tatu zilizosalia wacha zianzishe na baadaye tuweze kuongeza kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile kuna taaluma lazima tuanze kuitoa kwa wakulima wetu, siyo kila mkulima anaelewa njia ya kukopa benki. Lakini vile vile kama ni Wizara ya Fedha tuna taratibu, tunatakiwa tuzianzishe ili benki iweze kuwaongeza wakulima na kuwapa fursa nyepesi za kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yote tumesema lakini tumesema ni lazima tuanze na tungeweza kuanza na bilioni 10, bilioni moja na hata bilioni tatu na tungeweza kuanza na bilioni zozote zile lakini la msingi ni kuanza *a step forward*, ndiyo la msingi na hili

ndilo tulilolifanya Serikali. Bilioni 53 tunaelewa ukizitaja ni pesa nyingi lakini kimatumizi ni pesa kidogo. Tunawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, kwamba tukizipeleka kilimo zitaweza kusaidia sana. Leo kilimo kinakwenda na sayansi, huwezi ukalima ukategemea usiwe na mbegu bora lazima uende na sayansi, katika pesa hizi kuna *amount* fulani inakwenda kwa ajili ya mbegu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka niseme kwamba tumeleta Muswada huu kuwaomba Waheshimiwa Wabunge mambo mawili. La kwanza, ni nyongeza ya bajeti bilioni 53, lakini la pili kuwaomba Wabunge wakubaliane na Serikali kuzipeleka katika maeneo ambayo Serikali imeyaainisha. Matatizo yetu ni mengi na *this country is not static* tuna-*move*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasikiliza sana, baadhi ya Wabunge walikuwa wanasema miaka 45 ya uhuru. Tusikatishwe tamaa, huu muda toka tumepata uhuru siyo mkubwa ukilinganisha na maendeleo ambayo tumeyafikia. Wenzetu sasa hivi wanazungumzia miaka 205 toka wamepata uhuru, sisi tunazungumzia miaka 48. Tusikate tama, kitu muhimu ni kuona kwamba tuna *move* na hatua hizo za kuondoka kule tuliko zinaonekana. Sekta yoyote utakayoitaja hatua za kuondokana tulikotoka zinaonekana sekta yoyote *you can name it*. Kuna baadhi ya maeneo leo hatuyazungumzii tena hapa lakini mwanzo tulikuwa tunapiga kelele kwa sababu *we are committed*. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, hatuwezi tukafanya chochote bila ya kukiunga mkono kilimo, tunaelewa kuna sekta nyingine ambazo ni tegemezi kwa kilimo, lazima nazo zisaidiwe ili kilimo kiweze kufanya kazi. Nchi hii ni kubwa sana, tuna eneo kubwa sana lakini ni lazima tuwasaidie wakulima wetu, wavuvi na wafugaji ili tuweze kuondokana na tatizo hili tulilonalo sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nieleze hayo tu na nilikuwa nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge kwamba tuunge mkono hoja hii kwa faida ya wakulima, kwa faida yetu sote na kwa faida ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga tena mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa nitamwita mtoa hoja aweze kumalizia mazungumzo.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada huu kwa kuzungumza humu Bungeni na wale waliochangia kimaandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo ada naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia. Kwanza, nitawataja waliochangia kwa kuzungumza:-

Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi; Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani; Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mbunge wa Peramiho; Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mbunge wa Kisarawe;

Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah, Mbunge wa Mafia; Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani; Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mbunge wa Kongwa; Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini; Mheshimiwa Mudhihir Mohammed Mudhihir, Mbunge wa Mchinga; Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini; Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee Naibu Waziri wa Fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni pamoja na:-

Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini; Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi, Mbunge wa Bukoba Vijijini; Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi; Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mbunge wa Kibiti; Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mbunge wa Hai; Mheshimiwa Felister A. Bura, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mbunge wa Muhambwe; Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mbunge wa Kwimba; Mheshimiwa Dkt. Charles Ogesa Mlingwa, Mbunge wa Shinyanga Vijijini na Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwa maoni na ushauri wao na pia kwa kuunga mkono Muswada. Aidha, napenda pia kutoa shukrani zangu kwa Kambi ya Upinzani kwa maoni na ushauri wao pia. Naahidi kwamba Serikali itaufanyia kazi ushauri wote uliotolewa na Kamati zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijibu baadhi ya hoja kwa sababu hoja kadhaa zimejibiwa kwa kiasi fulani wakati Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira akichangia na wakati Naibu Waziri wa Fedha akichangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi ilikuwa na mambo makuu mawili. Moja liligusia msukosuko wa kiuchumi ambao umeikumba dunia na ambao unawezekana ukawa na athari kwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niliambie Bunge lako Tukufu kwamba kesho siku nzima nimepangiwa pamoja na Gavana wa Benki Kuu kuelezea suala hili kwa Bunge hili Tukufu. Kwa hiyo, tuna *paper* nyingi tu na suala hili tutalielezea kwa kirefu na kwa undani na tutawapa nafasi Waheshimiwa Wabunge mchangie ili tuweze kuona jinsi gani nchi nzima tunaweza tukajiandaa kukabiliana na matatizo hayo na kwa sababu ni kesho tu naona nisiondoe utamu, ni afadhali tusubiri mada hizo nizitoe kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo Kamati ya Fedha na Uchumi ilisisitizia ni kwamba, tuhakikishe kwamba Shirika la Mbolea au Kampuni ya Mbolea yaani *Tanzania Fertilizers Company* inapewa dhamana ya kutosha ili kuhakikisha kwamba wanashughulikia ununuaji, usafirishaji na usambazaji wa mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, kwanza Shirika la Mbolea limeshapewa *rolling guarantee* yaani *guarantee* ambayo wanayo mwaka mzima ya bilioni 32 kwa ajili ya kununua, kusafirisha na kusambaza mbolea. Fedha hizo wanazitumia na ikiwa itatokea kwamba wale wanaotaka *guarantee* wangetaka ku-*up stamp* ile *guarantee* Wizara ya fedha itakuwa tayari kulifanya hilo. Kwa hiyo, ushauri wa Kamati ya Fedha na Uchumi tunaupokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za Kambi ya Upinzani karibu zote zimejibiwa na Naibu Waziri wa Fedha lakini pale panaposema kwamba fedha hizi ni za Serikali au si za Serikali, nadhani Bosi wangu Rais Kikwete katika hotuba yake ya tarehe 21/8 alilizungumzia kwa kirefu na kwa kina. Kwa hiyo, kwa kweli kama *subordinate* wa Rais wangu sidhani kama nina chochote cha kuongezea yale aliyoyazungumza Mheshimiwa Rais tarehe 21 ndiyo hayo hayo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya kwamba fedha hizi tunazoziomba tayari zimeshatumika, nataka kueleza kwamba hilo kwa kweli si sahihi. Wizara au Serikali nzima haiwezi ikafanya maamuzi halafu ikaja ndani ya Bunge kufanya Bunge liwe *rubber stamp* na namshukuru Mheshimiwa Naibu Spika alipoelezea pale kutoa *clarification* kwamba kwake kule Njombe Wakala wameshasambaza mbolea, wanazo vocha, wamekwenda Benki wameshindwa kulipwa. Kama pesa hizi zingekuwa zimetumika wale Wakala wasingezikosa hizo pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba pesa hizi hazijatumika, tunakuja kuomba Bunge liidhinishe na baada ya Bunge kuidhinisha ndipo pesa hizi sasa zitapelekwa kule ambako tumesema sasa zipelekwe ambapo ni pamoja na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika bilioni 40, Wizara ya Mifugo na Uvuvi bilioni 10 na Hazina kwa maana ya Tanzania *Investment Bank* bilioni tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningependa nifafanue kwa sababu tumepata karatasi inayojaribu kusema kwamba Waziri wa Fedha amevunja Katiba na kwamba tunachokifanya kilishafanyika. Sasa waraka huu umewasilishwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge 107.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba ninukuu, Kanuni ya 7, inasema hivi: “Mapendekezo yoyote kwa ajili ya matumizi ya nyongeza ya fedha za Serikali au kwa ajili ya kutoa fedha yoyote ya nyongeza zaidi ya fedha za matumizi ya mwaka huo:-

(a) Yataitwa makadirio ya nyongeza ya matumizi;

(b) Yatapelekwa kwenye Kamati ya matumizi kufuatana na masharti ya Ibara ya 99 ya Katiba"

Waraka wangu unazungumzia kwamba mapendekezo haya yamepelekwa kwa kutumia Ibara ya 99.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mengi yameshazungumzwa ningependa nijikite pengine kwenye yale makubwa ambayo yamezungumzwa:-

La kwanza hili la Katiba, nafikiri nimeshalieleza lakini la pili ni kwamba pesa ambazo zinapelekwa *TIB* bilioni tatu ni kidogo. Hata wakati tunasema nilisema hivyo kwamba pesa hizi ni kidogo hazitoshi. Wakati Mheshimiwa Rais anazungumza hapa Bungeni tarehe 21/8 alizungumzia kupeleka bilioni 20 katika zile pesa bilioni 53 ambazo tulikuwa tuzitumie kwa ajili ya mbolea na pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya matatizo ambayo hata kaka yangu Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga ameyazungumza kwamba sasa hivi tuko kwenye *crisis*, hesabu zilipofanyika ikaonekana kwamba kwa kweli ni vizuri tukijikita katika kutafuta mbolea na pembejeo ambayo ni pamoja na mbegu bora ili angalau kule ambako mvua inapatikana basi wakulima wale walime chakula kiweze kupatikana angalau kiweze kupunguza tatizo la upungufu wa chakula nchini. Ndiyo uamuzi ukafanyika kwamba bilioni 30 zipelekwe Wizara ya Kilimo na Chakula ili zikanunue mbolea na bilioni 10 zikanunue pembejeo ambao ni pamoja na mbegu bora. Tarakimu hizi hatukuzitunga pale Wizara ya Fedha, tarakimu hizi zimeletwa na Wizara husika, zimezunguzwa ndani ya Serikali na ndiyo tukakubaliana kwamba mgao huo ndio ambao kwa wakati huu unaweza ukatuletea tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtaji wa *TIB*. Wakati nawasilisha makadirio ya bajeti ya mwaka ulikuwa bilioni 29, katika bajeti yenyewe tumeshaiongezea *TIB* bilioni nyingine 21 kwa hiyo sasa hivi mtaji wa *TIB* umeshafikia bilioni 50 kutoka bilioni 29 zilizokuwepo na mpango uliopo wa Serikali tuna vyanzo vingi lakini kwa sababu hatujavikamilisha, hatuwezi kuvizungumza ndani ya Bunge mpaka tuwe tumevikamilisha. Kwa hiyo, uko mpango wa kutafuta pesa mahali pengine ili kuongeza mtaji wa *TIB*. Sasa tutakapokuwa tayari tunaweza tena tukaja na Waraka namba 2 wa Nyongeza ya Mapato na Matumizi lakini mpaka tutakapokuwa tayari kwa sababu hatuwezi kuzungumza ndani ya Bunge kabla hatujasaini na wale ambao wanatazamiwa kutupa pesa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba *TIB* ni kipaumbele na kama Waziri wa Fedha nimekiweka kama ni kipaumbele kwamba katika wakati wangu wa Uwaziri ni lazima nihakikishe *TIB* inakuwa *capitalised* vilivyo na kwamba dirisha la kilimo linakuwepo. Lakini pia nataka niwaambie kwamba hata kama halijawa tayari Mheshimiwa Rais ameagiza kwamba dirisha la kilimo liwe la muda, *ultimate objective* iwe ni kuanzisha Benki ya Kilimo kama jinsi ambavyo tulikuwa tumeahidi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kubwa ambalo nilikuwa nataka niwahakikishieni ni kwamba, hizi bilioni tatu ni kweli si fedha ambazo tunaweza kusema tunaweza kuanzisha lakini angalau dirisha lianze, kwa hiyo hii bilioni tatu ni ya kuanzishia dirisha hilo la kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, mikopo ya kilimo sasa hivi inatolewa siyo na *TIB* lakini na *NMB* (*National Microfinance Bank).* Kwa hiyo, kama kuna mtu anataka kununua trekta asiende *TIB* kwa sababu *TIB* zile pesa ambazo tumewapa kwa kweli ni za miradi mingine ya kimaendeleo lakini benki hasa ya kutoa mikopo ya ki- *Micro Finance* ni *National Micro Finance Bank*, hiyo tayari inatoa mikopo hiyo na taratibu ambazo benki yenyewe imejiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa wale wanaotaka kukopa matrekta ndani ya Bunge hili mwaka jana tulileta Muswada wa *Lease Finance* ambao unaweza ukakopa trekta au vyombo vyote hata vyombo vya ujenzi. Muswada ule ulishapita, Rais ameshasaini kinachosubiriwa sasa hivi wanakamilisha Kanuni yaani *Regulations, Regulations* hizi zikiwa tayari mikopo ya matrekta msiende *TIB*, tumeshaunda chombo cha kufanya hayo. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba kwa kweli hizi bilioni tatu ambazo zimezungumzwa sana kwamba ni kidogo, nashukuru kwa kweli kwa ushauri na nasema kama Serikali tunakubali kwamba ni kidogo na hata wakati tunawasilisha tumesema kwamba ni kidogo. Lakini mipango mikakati ipo ya kuweka pesa za kutosha, kuweka mtaji wa kutosha katika benki ya raslimali ili iweze:-

(i) Kutoa mikopo kwa miradi ya maendeleo

(ii) Kutoa mikopo inayohusiana na miradi ya kilimo.

Kwa hiyo, wale Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao mlikuwa mnasema hizi pesa ni kidogo, kwa kweli hatukukaa tu tukasema tupeleke huku 40, huku kumi na kadhalika, ni hesabu ambazo zimefanyika ndani ya Serikali na naomba mtuamini Serikali kwamba huo mgao tuliouweka ndiyo mgao tunaofikiri kwamba kwa wakati huu ambao tuna *crisis* ndiyo mgao wenye tija. Mgao wowote mwingine ni wa muda mrefu kwamba ukitaka sasa kumkopesha mtu aende kwenye kilimo tunaweza tukapata hayo katika muda wa miaka mitatu au miaka mitano ijayo. Tuna *crisis* leo, njaa inatusogelea, kwa hiyo ni vizuri kama Serikali tujiandae kuondoa tatizo hili la njaa sasa na ndiyo maana tumeweka hizo pesa huko tulikopendekeza kwamba zipelekwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nitamke kwamba kuna wachangiaji wengine walichangia lakini sikuwatamka majina yao mmoja wapo naomba radhi ni Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi Mbunge wa Ludewa. Waliochangia kwa maandishi ni pamoja na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi, Mheshimiwa Christine Ishengoma, Mheshimiwa John Paul Lwanji na Mheshimiwa Godfrey W. Zambi wa Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Wabunge kama Mbunge wa Mafia na Mbunge wa Mchinga walizungumzia kwamba uvuvi umesahauliwa. Nataka niwahakikishie kwamba nia kubwa ya Rais kuunda Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni kuhakikisha kwamba uvuvi nao unapewa kipaumbele. Kwa hiyo, hizi pesa kidogo ambazo tunazo bilioni 10 ipo sehemu ya pembejeo zinazohusiana na uvuvi na nataka kumhakikishia Ndugu yangu Mudhihir Mudhihir kwamba uvuvi hata katika hizi bilioni 10 umefikiriwa lakini katika bajeti ya mwaka 2009/2010, tutaweka kiwango maalum kwa ajili ya kuendeleza uvuvi. Sasa hilo litasemwa na mwenzangu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, nisingependa nilizungumzie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika kwamba nahitaji kuendelea na mengine, lakini nataka kumhakikishia Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto kwamba kwa kweli hatukuvunja Katiba, tumefuata taratibu zote zinazohitajika ili Bunge liidhinishe mapato. Likishaidhinisha ndiyo tukae, *Controller and Auditor General* hawezi ku-*approve* kitu ambacho hakijaidhinishwa na Bunge.

Kwa hiyo, kwa *Controller and Auditor General* ni hatua ya pili kwamba ni lazima Bunge kwamba liidhinishe nyongeza hii, baada ya kuidhinisha sasa ni kwamba, zile pesa ambazo ziko kwenye Mfuko ndiyo *Controller and Auditor General* anaidhinisha kwamba sasa pesa hizi zitoke zikafanye kitu fulani. Kwa hiyo, ni *stage* ya pili na siyo *stage* ya kwanza, kwanza Bunge lipitishe halafu ndiyo *Controller and Auditor General* aweze kuidhinisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwahakikishia kwamba, hata siku moja Wizara ya Fedha au Serikali nzima kwa ujumla wake haitaleta hapa ndani ya Bunge mambo kama hayo, kama tumetumia tutasema tumetumia, tunaomba *restrict to approve*, hapa hatujatumia tunasema tunaomba Bunge liidhinishe ili pesa hizi zitumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kusema humu Bungeni na kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 (*The Supplementary Appropriation for Financial Year 2008/2009) Bill,* 2009**

Fungu 21 - Hazina …. … … .... .... .... .... ... .... Sh. 3,000,000,000

Fungu 43 – Wizara ya Kilimo na Chakula… … … …Sh. 40,000,000,000
Fungu 99 - Wizara ya Maendeleo ya Mifugo
na Uvuvi … … … ... .... .... ..... ..... ..... .... … Sh. 10,000,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 (*The Supplementary Appropriation for Financial Year 2008/2009) Bill,* 2009**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Nyongeza ya shilingi bilioni 53 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2008/209, yaani *The Supplementary Appropriation for Financial Year 2008/2009 Act 2009* pamoja na marekebisho yake sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa umemaliza hatua zake zote na kama ilivyo ada baada ya kupitisha hii *Supplementary estimate expenditure* ndiyo *addendum* kwenye kitabu cha *revenue* kwamba matumizi ya Serikali siyo yale tuliyopitisha hapa yameongezeka mengine na ndiyo maana yanaitwa *estimates*. Kwa hiyo, katika *revenue* pia kutakuwa na ongezeko la kiwango kinacholingana.

Lakini pia mkisoma hii *Supplementary Bill* mtakuta kinatimiza masharti yote ya *double entry,* imetimiza masharti yote ya *double entry* katika hesabu hizi. Kwa hiyo, nafikiri iko katika hali nzuri.

Waheshimiwa Wabunge, tukirudi mchana tutakuwa na maazimio kwanza azimio la Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. La pili, ni azimio linalohusu kuridhia itifaki ya Jumuiya ya *East African* kuanzisha chombo cha kusimamia usalama na ulinzi wa anga. Kwa hiyo, naomba mjiandae tunao wachangiaji wa chache kwa hiyo mjiandae wale wanaotaka kuzungumza.

Baada ya kusema hayo, sina shughuli nyingine, kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.30 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

### Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki (*Protocol on the Establishment of the East African Science and Technology Commission*)

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge lako Tukufu katika mwaka huu 2009, naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya familia yangu na wananchi wote wa Jimbo la Kilolo kukutakia wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika, Spika, Waheshimiwa Wabunge wote, kheri na fanaka ya mwaka mpya 2009. Aidha, natoa salamu za pole kwa familia ya ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu Richard Nyaulawa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo naomba pia kumpongeza Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale Mbunge wa Mbeya Vijijini CCM kwa ushindi alioupata katika uchaguzi mdogo wa Jimbo hilo uliofanyika hivi karibuni. Vilevile nampongeza Dkt. Thomas Kashililah kwa kuteuliwa kwake kuwa Katibu mpya wa Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, naomba sasa kutoa maelezo yanayohusu Itifaki ya Kuanzishwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki. Kabla ya kusoma Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mohamed Hamis Missanga Mbunge wa Jimbo la Singida Kusini (CCM) kwa kujadili kwa kina Itafiki hii na kutoa ushauri. Itifaki ya Kuanzishwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ilisainiwa na Mawaziri wa Sayansi na Teknolojia wa Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 18 Aprili, 2007 katika Makao Makuu ya Jumuiya iliyopo Mjini Arusha Tanzania.

Lengo la Itifaki hii ni Kuanzishwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kukuza ushirikiano katika masuala ya utafiti na maendeleo,

ugharamiaji wa tafiti, kukuza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano pamoja na kubuni sera za sayansi na teknolojia za kikanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la Itifaki ya kuanzishwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki ni kuanzishwa tena kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Umuhimu wa nchi wanachama kushirikiana katika maeneo ya sayansi na teknolojia ulijitokeza upya katika vikao mbalimbali vya Wakurugenzi wa Idara za Sayansi na Teknolojia na Wakurugenzi Wakuu wa Tume, Mabaraza ya Kitaifa ya Sayansi na Teknolojia ya Nchi za Tanzania, Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, majadiliano ya wataalam hao yalibaini umuhimu wa kuwepo kwa Itifaki ya Kuanzisha Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki. Aidha, Kamati ya Sekta ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliandaa rasimu ya Itifaki ambayo ilisainiwa na Mawaziri wanaohusika na masuala ya Sayansi na Teknolojia kutoka nchi za Tanzania, Uganda na Kenya. Ibara ya 21 ya Itifaki hii inazitaka nchi wanachama zilizosaini Itifaki hii kuuridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui ya Itifaki yamejikita katika kuchochea ushirikiano miongoni mwa nchi wanachama katika nyanja za sayansi, teknolojia na ubunifu ili kutoa msukumo katika kukuza uchumi na maendeleo ya jamii kwa kutumia rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii ina jumla ya vifungu 24 ambavyo pamoja na mambo mengine vinaeleza matumizi ya wigo yaani *scope*, malengo, majukumu na aina ya wajumbe watakaounda Bodi ya Tume, utekelezaji wa majukumu yaliyomo ndani ya Tume, masuala ya fedha, hadhi, maslahi, kinga na kanuni, namna ya kushughulikia migogoro, muda wa kuanza kutumia Itifaki na namna ya kufanya marekebisho katika Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida ya kuridhia Itifaki. Baadhi ya faida ambazo Tanzania itapata endapo Bunge litaafiki na kuridhia Itifaki hii ni pamoja na yafuatayo:-

Moja, kushirikiana na nchi wanachama katika kufanya utafiti, kusambaza matokeo na ubadilishanaji wa taarifa zinazohusu Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, kulingana na taratibu zitakazoandaliwa na nchi wanachama.

Pili, kushirikiana na nchi wanachama kujenga uwezo wa wataalam katika nyanja za sayansi, teknolojia na utafiti.

Tatu, kupata fursa ya kuweza kuwa mwenyeji wa Makao Makuu ya Tume pamoja na faida nyingine kama zilivyoainishwa kwenye Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya raslimali. Endapo Bunge litaridhia Itifaki Serikali kwa kupitia Bunge itaweza kutenga fedha katika Bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kama zinavyotengwa kuendesha vyombo vingine vya Jumuiya. Michango kutoka kwa wafadhili na wadau wa masuala ya sayansi na teknolojia vitakuwa miongoni

mwa vyanzo vya mapato ya Tume. Endapo Tanzania itaomba na kukubaliwa kuwa Makao Makuu ya Tume hii basi kwa kuanzia majengo ya Tume ya Sayansi na Teknolojia yaliyopo Kijitonyama Dar es Salaam yataweza kutumika katika kuendesha shughuli zake. Wizara kwa kutambua uwezekano wa suala hili kukamilika mapema iliomba na kupitia Bunge lako Tukufu imetenga kiasi cha shilingi milioni 474 kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa jengo hilo katika mwaka fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa utaratibu wa kuridhia Itifaki hii unazingatia Ibara ya 21 ya Itifaki, nchi wanachama zinatakiwa kuridhia na kisha kuwasilisha hati ya kuridhia itifaki kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kufuatia matakwa haya ya Itifaki, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sura ya Pili, imepewa madaraka ya kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi matamkwa ya Itifaki na masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki husika kama ifuatavyo:-

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki yaani *Protocol on the Establishment of the East African Science and Technology Commission.*

KWA KUWA Jamhuri ya Mungano ya Tanzania ni nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani *the East African Community* kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Uanzishwaji wa Jumuiya hiyo;

NA KWA KUWA lengo la kuanzishwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki yaani *East African Science and Technology Commission* ni kukuza na kuratibu maendeleo, usimamizi na matumizi ya Sayansi na Teknolojia kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

NA KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatimiza masharti ya kukuza ushirikiano katika masuala ya utafiti na maendeleo, ugharamiaji wa utafiti, matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano pamoja na teknolojia mpya na zile zinazojitokeza kwa kubuni sera za sayansi na teknolojia za kikanda;

NA KWA KUWA inakusudiwa kuwa Makao Makuu ya Tume hiyo kuwa nchini Tanzania;

NA KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakusudia kushirikiana na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kubuni sera na mikakati madhubuti ya kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu kwa ajili ya kuleta maendeleo endelevu kwa nchi za Jumuiya ya Afrika;

NA KWA KUWA kwa kuridhia Itifaki hii Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itanufaika na matokeo ya tafiti mbalimbali za kisayansi na teknolojia zinazofanyika katika nyanja mbalimbali za uchumi ndani ya Afrika Mashariki;

HIVYO BASI kwa kuzingatia umuhimu wa kuridhia Itifaki hii na mafanikio ambayo Jamhuri ya Muungano ya Tanzania itapata, Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Nne na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaazimia kuridhiwa kwa Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Kuanzishwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki yaani *Protocol on the Establishment of the East African Science and Technology Commission.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu kuwasilisha mbele ya Bunge maoni ya Kamati ya Miundombinu kuhusu kuridhia Itifaki ya Uanzishwaji wa Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 70(2) ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la mwaka 2004, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Miundombinu kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Kuanzishwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki chini ya Mpango wa Ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Sophia M. Simba kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania katika uchaguzi uliofanyika mapema mwezi Januari mwaka 2009. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale aliyeshinda katika kinyang’anyiro cha uchaguzi mdogo wa Ubunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini uliofanyika mapema mwezi Januari 2009. Nawatakia wote mafanikio katika majukumu yao mapya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki, kunafuatia kwa kuanzishwa upya kwa Jumuiya ya Afrika. Nia kubwa ni kujenga na kuendeleza ushirikiano wa Nchi Wanachama katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Aidha, kubuni sera na mikakati madhubuti ya kuendeleza fani ya sayansi na teknolojia na hivyo kuleta maendeleo endelevu kwa nchi zote za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki ya kuanzishwa kwa Tume ya Sayansi na Taknolojia ilikwishasainiwa na Mawaziri wa Sayansi na Teknolojia wa Nchi wa Wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki tarehe 18 Aprili, 2007 katika Makao Makuu ya Jumuiya yaliyopo mjini Arusha nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kuu la Itifaki ya Kuanzishwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki (*Protocol on the Establishment of the East African Science and Technology Commission)* ni kukuza na kuratibu usimamizi wa maendeleo ya matumizi ya sayansi na teknolojia ikiwa ni pamoja na kubuni uanzishaji wa Sera za Sayansi na Teknolojia kwa Nchi Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Aidha, itifaki hii inalenga katika kukuza ushirikiano katika nchi wanachama, juu ya masuala ya utafiti na maendeleo na ugharamiaji wa utafiti huo, kukuza na kuendeleza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano pamoja na teknolojia mpya na zile zinazojitokeza kwa kubuni sera za sayansi na teknolojia za kikanda.

Mheshimiwa Spika, kuhusu faida za kuanzishwa kwa Tume. Kwa kuridhia itifaki hii Tanzania itanufaika na faida zifuatazo:-

Moja, ushirikiano na nchi nyingine katika kufanya utafiti, kusambaza matokeo na ubadilishwaji wa taarifa zinazohusu sayansi na teknolojia na ubunifu kulingana na taratibu zitakazoandaliwa na nchi wanachama.

Pili, kushirikiana katika kujenga uwezo wa watalaam, katika fani za sayansi, teknolojia na utafiti.

Tatu, upo uwezekano mkubwa kwa Tanzania kupata fursa ya kuwa mwenyeji kwa maana ya Makao Makuu ya Tume kuwa hapa Tanzania.

Nne, kupata fursa ya ajira kwa wanasayansi wa Kitanzania na faida ya jumla kwa nchi Wanachama kutokana na kuwa na mazingira na matatizo yanayofanana ya kijiografia na kuwepo fursa za maendeleo yanayoshabihiana kutokana na kwamba fursa hii itakuwa chachu ya kupata msaada kutoka katika nchi wahisani katika kugharamia shughuli za Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe maoni ya Kamati. Kwa kuwa Itifaki hii imekwishasainiwa na nchi wanachama, wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwa kuwa kifungu cha 24 cha Itifaki kinatoa fursa na maelezo ya jinsi ya kufanya marekebisho katika Itifaki pale itapobidi kufanya hivyo, yapo maeneo ambayo Tanzania kama nchi wanachama ni vyema yakazingatiwa kwa uzito unaostahili kwa sasa na hapo baadaye kadri Tume itakavyokuwa ikitekeleza kazi zake. Hivyo Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Moja, Tanzania itumie fursa hii kama mwanachama kuwa na umakini mkubwa katika kuchochea wanasayansi wa Kitanzania kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi na kitaaluma katika Tume hii.

Pili, Wizara iwezeshwe kwa maana ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa kiwango kinachostahili ili iweze kuipa Tume hadhi inayostahili kimajengo, ofisi na vitendea kazi vyote muhimu.

Tatu, ajira katika Tume hii izingatie usawa baina ya nchi wanachama kwa kuwapata wataalam wa jinsia zote wenye sifa, uwezo, uzoefu na taaluma inayostahili.

Nne, kuanzisha, kudumisha na kuendeleza ushirikiano na Tume kama hii kutoka nchi zilizoendelea ili kupata fursa ya kujifunza na kupata ujuzi zaidi.

Tano, katika kuridhia Itifaki hii tahadhari na umakini mkubwa uwepo katika kuzingatia maslahi ya Taifa letu pasipo kukaribisha mianya ya kutumika kwa faida ya wenzetu.

Sita, pamoja na kuridhia Itifaki hii tusikubali chombo hiki kiwe ni mbadala wa vyombo vyetu vya sayansi na teknolojia vya hapa nchini.

Saba, Taasisi zetu za Sayansi na Teknolojia pamoja na vituo mbalimbali vya utafiti hapa nchini viimarishwe zaidi na kamwe tusisahau majukumu yetu katika masuala mbalimbali ya Sayansi na Teknolojia.

Nane, kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Kimataifa kama vile *UNESCO* Wizara iongeze kasi ya kuandaa na kukamilisha Sera ya Sayansi na Teknolojia.

Tisa, Tanzania itakapoteuliwa kuwa Makao Makuu ya Tume itakuwa busara kushawishi mapema nchi wanachama kupata mahali na sehemu patakapojengwa Makao Makuu ya Tume hiyo hapa nchini.

Kumi, kwa kuwa nchi za Rwanda na Burundi zilijiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki baada ya nchi ya Tanzania, Kenya na Uganda kuunda Jumuiya hiyo na kwa kuwa nchi hizi nazo zilikwishasaini Itifaki hii basi ni vyema kuwepo kiambatanisho kinachothibitisha kujiunga kwao ndani ya Itifaki hii.

Mwisho, Kamati inashauri Muswada wa Kuanzishwa kwa Bodi na Sekretarieti ya Tume uwasilishwe mapema katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki ili chombo hicho muhimu kiweze kuanza kufanya kazi zake kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa ni jambo la busara kwa nchi zetu kuchangamkia ajira katika ushirikiano huu na wala tusiwaachie nchi nyingine peke yao na hasa Makao Mkuu yakiwa Tanzania ni muhimu kuwa na Watanzania katika Sekretarieti. Ili kujenga uzoefu na kuimarisha uongozi na utawala, muda wa uongozi wa Mtendaji Mkuu kwa maana ya *Executive Secretary* uwe wa awamu mbili au zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati yangu imepitia na kujadili kwa kina Itifaki hii na kuridhia katika ngazi ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa michango na maoni mbalimbali na mabadiliko madogo madogo yaliyopendekezwa ambayo kimsingi Mheshimiwa Waziri ameyakubali na kuyazingatia na kuiwezesha Kamati kuwasilisha taarifa na maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati yangu kama ifuatavyo: Wa kwanza ni mimi niliyesimama mbele yenu na ndiyo Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Makamu Mwenyekiti…

**NAIBU SPIKA:** Hatujui jina. Mheshimiwa Mwenyekiti, inaingia kwenye *Hansard*, ukisema ni mimi niliyesimama hapa, *Hansard* itasema hivyo!

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Narudia kusema kwamba napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati yangu kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Alhaj Mohamed Hamisi Missanga, Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Anne Killango Malecela, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Paschal Constantine Degera, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu, Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Joyce Martin Masunga na Mheshimiwa Herbert James Mntangi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Balozi Getrude Ibengwe Mongella, Mheshimiwa Alhaj Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mheshimiwa Sigifrid Seleman Ng'itu, Mheshimiwa Mwaka Abdulrahaman Ramadhan, Mheshimiwa Philemon Mikol Sarungi na Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Peter Msolla, Waziri na Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari Mbunge, Naibu Waziri; kwa kuwasilisha mbele ya Kamati Itifaki hii muhimu na kwa wakati muafaka na pia kutoa maelezo ya kina na fasaha. Aidha, napenda pia kumshukuru Prof. Evelin Mbende, Mkurugenzi wa Sayansi na Teknolojia kwa ufafanuzi na michango yake aliyotoa mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Dkt. Thomas Kashililah kwa kuteuliwa kwake na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuwa Katibu wa Bunge. Aidha, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Katibu huyo wa Bunge ndugu yetu Kashililah pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa huduma mbalimbali zinazoisaidia Kamati yangu katika kutekeleza wajibu wake. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati hii Bwana James Warburg na

Bibi Justina Shauri kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ya kila siku na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii kwa ufanisi unaostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 naomba Bunge lako Tukufu liipokee Itifaki hii, liijadili na kuipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Sasa nitamwita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani kuhusu Itifaki hii. Nafikiri Said Arfi.

**MHE. SAID A. ARFI – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kambi ya Upinzani ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Uanzishwaji wa Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki *(Protocol on the Establishment of the East African Science and Technology Commission*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6) Toleo la 2007. Naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki hii la Kuanzishwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nitoe salamu za mwaka mpya kwako wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, wananchi wote wa Mkoa wa Rukwa hasa Wilaya ya Mpanda hususan wakazi wa Jimbo la Mpanda kati, nawatakia kheri na kujituma katika kuinua uchumi wao binafsi na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba kutoa machache kuhusiana na Azimio hili kwa kweli ni jambo la msingi kuanzishwa kwa Tume hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati iliyopata bahati ya kupata maelezo ya kina juu ya Azimio hili kimsingi Kambi ya Upinzani haina pingamizi na kuridhiwa kwa Itifaki hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo tu ni jinsi gani Watanzania wameandaliwa ili kuwa nao ni washiriki halisi na siyo kuwa watu wa kuhudhuria vikao katika Tume hii. Aidha, tunamtaka Mheshimiwa Waziri awaeleze Watanzania Mpango Mkakati wa Serikali katika uanzishwaji wa Tume hii.

Pili, Serikali na vyombo vyake, na taasisi zake ziwe makini sana katika kulinda na kuhifadhi haki na miliki za wavumbuzi wetu wa Kitanzania.

Kadhalika, fursa zote zinazopatikana katika kuridhia Itifaki hii, basi ziwanufaishe Wanasayansi na Wataalam wa Kitanzania, pia katika kukuza na kuendeleza utafiti kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mwisho, wananchi nao pia wanufaike katika Itifaki hii, kwa kupewa taarifa ambazo zinawagusa katika ustawi na maendeleo hususan zana za kilimo ambacho ni tegemeo la Watanzania wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa haya machache, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia mambo machache sana, kuhusu Itifaki ambayo imewasilishwa hivi punde.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba niseme kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, ambayo imehusika sana katika kuupitia Muswada huu au Itifaki hii na baadaye kuiwasilisha hapa ndani ya Bunge lako Tukufu. Kwa sababu na mimi leo ni mara yangu ya kwanza kusimama kwa ajili ya kutoa hotuba kwenye Bunge lako Tukufu, naomba nitumie nafasi hii, kumpongeza sana ndugu yangu na kaka yangu, Mchungaji Luckson Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kwa kushinda katika uchaguzi mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wa Mbeya tulikuwa wakiwa, baada ya kifo cha aliyekuwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa, lakini leo Mbeya hatuna ukiwa tena, kwa maana ya kwamba, lile pengo ambalo tuliachiwa limeshazibwa. Naomba nimhakikishie ndugu yangu, Mchungaji Mwanjale kwamba, tupo naye na tutaendelea kufanya kazi pamoja katika kuendeleza maslahi ya Mkoa wetu wa Mbeya na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu huu ni mwaka mpya, naomba nichukue nafasi hii, niwatakie wananchi wote na wapiga kura wangu wa Jimbo la Mbozi Mashariki, kheri ya mwaka mpya na baraka za Mwenyezi Mungu ili tuweze kwenda vizuri katika mwaka huu mpya. Vilevile nampongeza sana ndugu yangu, Dkt. Kashillilah, kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Matumaini yangu ni kwamba, atafanya kazi vizuri na sisi Wabunge tufaidike na utumishi wake, lakini pia na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge. Namtakia mema katika jukumu lake jipya na zito.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba niseme kwamba, kwa sababu nimetangulia kusema mimi ni mdau, naomba niseme mambo machache sana ambayo kimsingi mengi tumeyasema kwenye Kamati na ambayo kama yalivyowasilishwa na Mwenyekiti na Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Kwanza, nimpongeze Waziri wa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Mawasiliano, Mheshimiwa Profesa Msola, kwa kuwasilisha vizuri Itifaki mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu, tumezoea kusema mambo haya yanachelewa; ni kweli ushirikiano katika nyanja kama ya sayansi unapokuja leo, lazima tuseme umechelewa. Tunamshukuru Waziri kwamba ameweza kuwasilisha. Sababu kubwa za kumpongeza ni kwamba, tunahitaji umoja katika eneo la Sayansi na Teknolojia, kwa sababu ni mwanzo wa chimbuko la maendeleo mengi sana katika nchi mbalimbali duniani. Kwa hiyo, kwa kushirikiana katika eneo la Sayansi na Teknolojia ni hakika kwamba, kunaweza kutusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wasiwasi kidogo unaotokana na ukweli kwamba, leo hapa nchini tuna Taasisi nyingi sana, zinazohusiana na mambo ya Sayansi na Utafiti katika maeneo mbalimbali. Tafiti nyingi sana zimefanywa katika maeneo mbalimbali, lakini tumezitumiaje katika kuwaletea Watanzania maendeleo; huu ndio wasiwasi wangu hata tunapoingia kwenye Itifaki hii ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna vyuo vingi vinavyojihusisha na utafiti, kwa mfano, mbegu za mazao mbalimbali. Vyuo kwa mfano, Uyole, Ukiligulu, Naliendele, Mlingano, Ilonga na vinginevyo, vinajihusisha sana na utafiti wa mbegu ya mazao mbalimbali, lakini taarifa tulizonazo ni kwamba, tunatumia asilimia 25 tu ya mbegu ambazo zinazalishwa nchini na asilimia 75 tunaagiza kutoka nje. Sasa pamoja na vyuo vingi hivi tulivyonavyo vya utafiti, lakini bado sioni kama vimetusaidia sana. Sasa tunakwenda kwenye ushirikiano mkubwa, ninafikiri tuna sababu ya kuongeza nguvu na kasi. Ninaomba nimshauri Mheshimiwa Waziri; tatizo kubwa tulilonalo kwenye vyuo vyetu hata ambavyo vipo hapa nchini ni kwamba, hatuvipi fedha zinazotosheleza kwa ajili ya kuendeleza shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vyote hivi havipewi fedha za kutosha na tafiti nyingi na ushahidi unaonesha. Mimi kama Mjumbe, tulitembelea Taasisi ya Sanyansi na Teknolojia pale Kijitonyama, wakatuambia tafiti nyingi sana zimefanywa lakini utekelezaji wake umeshindikana kwa sababu ya kutokuwa na fedha za kutosha. Tunatumia fedha kuwatuma wataalam wetu kwenda kufanya utafiti, lakini inapokuja sasa kwenye *implementation* ya tatifi zenyewe fedha hazipo. Kwa hiyo, tunaona tunavyopoteza fedha kufanya kazi ambayo mwishoni haitunufaishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika kama hali itakwenda hivi kwenye ushirikiano huu wa Afrika Mashariki na kama huu ni mwenendo tunao nchini na huko ikaenda hivyo, sina hakika kama tutapata tija sana. Ndio sababu ninaomba Waziri, pamoja na Mawaziri wenzake wa nchi hizi, wawe na *commitment* ya kutosha, kuhakikisha kwamba, Tume hii tunayoianzisha ya Sayansi na Teknolojia, inapewa fedha za kutosha ili iweze kufanya kazi zake sawa sawa. Vinginevyo, tutakuwa tunakuja hapa tunapitisha Itifaki ambazo haziwezi kutusaidia Watanzania. Kwa hiyo ni matarajio yangu kwamba, hili litafanyika na Mheshimiwa Waziri, pamoja na wataalam wataweza kulisimamia vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni la kukazia; tumeingia kwenye taasisi hizi wakati mwingine bila kujiandaa vizuri, kwa maana ya wataalam na kwa maana

ambayo nimetoka kuisema muda mfupi uliopita.  Hili limekaziwa sana kwenye Kamati na mimi naomba nilikazie kwamba, tuhakikishe wataalam na Watanzania wengi, wanakwenda kufanya kazi kwenye taasisi hizo ili na sisi kama nchi tuweze kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, mimi ni Mjumbe wa Kamati na nilikuwa na tatizo moja kuhusiana na tafiti ambazo zinafanywa, lakini utekelezaji wake haufanyiki inavyopaswa.  Hili ni eneo ambalo bado naendelea kusisitiza kwamba, Wizara ihakikishe inalifanyia kazi kubwa sana ili tuweze kuona matokeo ya Itifaki yenyewe itakaposainiwa na nchi zote na kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.  Ahsante sana.  *(Makofi)*

**MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE:**  Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia kwenye hoja iliyopo mbele yetu, kuhusu Itifaki ya Kuanzishwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu waliochangia jioni hii, kumpongeza Mheshimiwa Luckson Mwanjale, kwa ushindi mzuri alioupata katika Jimbo la Mbeya Vijijini.  Vilevile nampongeza Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Jumuiya muhimu sana hapa nchini.  Pia nampongeza Katibu wetu wa Bunge, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Katibu wa Bunge na kuondoa lile neno la ukaimu ambalo alikaa nalo kwa muda mrefu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa kuwasilisha hoja hii kwa ufasaha mkubwa.  Faida za Tume hii ya Jumuiya ziko dhahiri na hasa kwa Tanzania ambayo itakuwa Makao Makuu ya Tume hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, imeanza kujitokeza tabia ambayo ni ya kawaida tu kwamba, mtu anayefaidika zaidi ndiyo anayekimbilia kutekeleza haraka hilo suala na wale wengine ambao wanaona kama hawafaidiki, kwa nguvu sana hukwepa.  Nasema hili kwa sababu Itifaki hii ilisainiwa na Mawaziri hawa akiwepo Profesa, karibu miaka miwili iliyopita.  Sasa najiuliza ni tatizo lipi lilitokea miaka yote miwili lile faili kuhama kutoka Arusha kuja hapa Dodoma, lakini vilevile ninavyoelewa nchi zote za Afrika Mashariki hazijaridhia huu mkataba?

Sasa tulikuwa tunawasubiri wenzetu waridhie, nafikiri tulitakiwa sisi Watanzania tuwe wa kwanza kuwasukuma wenzetu, kwa sababu tutapata faida zaidi katika Tume hii. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, atakapojibu anieleze ni kitu gani kimeleta tatizo sana, kusukuma hilo faili kutoka Arusha kuja Dodoma; tunahitaji kweli miaka miwili? Vilevile tunaambiwa Makao Makuu yatakuwa Tanzania, atudokeze kidogo Tanzania sehemu gani.  Vile vile ni vizuri kujua ili kuweza ku-*spread benefits* za Jumuiya ya Afrika Mashariki.  Kila kitu kisirundikwe Arusha tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano wa nchi zetu za Afrika Mashariki hususan Kenya, Tanzania na Uganda, katika hii nyanja ya Sayansi na Teknolojia si mgeni; tulikuwa nao katika Jumuiya yetu iliyopita, ambayo iliyoanguka mwaka 1977. Tulifanya vizuri sana chini ya Jumuiya iliyopita. Kwa kuwa *scientific research* ni ghali sana, nchi moja moja kubeba huo mzigo ni kazi kubwa sana na ndiyo maana nchi nyingi za Kiafrika, tuko nyuma kabisa kwenye *research and development,* tuko nyuma zaidi kuliko mwaka 1977 wakati tunachangia hili suala la utafiti.

Kwa hiyo, mimi naliunga mkono suala hili la kuunda hii Tume na tuna wajibu wote sisi kama Bunge la Jamhuri ya Muungano, kuridhia Itifaki hii. Ninaomba nisisitize kidogo neno moja hapa; utafiti msingi wake ni elimu, elimu bora ndiyo inazaa watafiti. Mimi nafurahi kwamba, Profesa Msola, ambaye ni bingwa na wenzake, wamelitambua hili na ndiyo maana ukiangalia kwenye maamuzi yao mbalimbali kwenye Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki, limeanza kuchukuliwa hatua za kuboresha elimu kijumuiya. Nitatoa mfano mmoja mdogo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2004, Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki, liliamua kwa kauli moja, kuvilazimu Vyuo Vikuu vyote vya Umma vya Afrika Mashariki, kutoza ada zinazofanana kwa wanafunzi wote wanaotoka katika nchi wanachama. Kwa mfano, mwanafunzi anatoka Tanzania anakwenda Makerere, uamuzi wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ulikuwa unazuia huyu kijana kutoka Tanzania apewe ada tofauti au awe *treated as a foreign student,* anakuwa *treated* kama vijana wengine wowote kutoka Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka mwaka 2004 ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam peke yake, kinachoheshimu uamuzi huo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Makerere bado wanabagua vijana kutoka Tanzania. Kenya bado vijana wa Tanzania wanabaguliwa, kwa ada na masharti mengine ya udahili. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, anielezee kwa nini kuna ukaidi wa aina hiyo, hatupati *motivation* hata tukiridhia vitu kama hivi tukishaamua basi kuna nchi nyingine ndiyo *super members* na wengine ni *junior members?*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuiomba sana hii Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ieneze elimu ya usajili wa uvumbuzi tunaofanya huko vijijini na sehemu mbalimbali. Watanzania ni watundu sana, lakini elimu ya kusajili uvumbuzi wao haipo kabisa. Ninawafahamu watu wengi wanaohangaika kwamba, mimi nimegundua hiki na kile, nimegundua dawa hii unamwuliza ulifanyaje anasema nilimwachia yule Mzungu e sasa amekwenda atakuja kuniona baadae! Bado tupo nyuma mno, lakini tuna taasisi hapa ya *BRELA*, ambayo inashughulikia hayo masuala. Pengine ni kwa sababu tu *BRELA* itakuwepo chini ya Wizara nyingine, lakini bado hii ni Serikali moja na Wizara hii haiwezi kujitoa kabisa kutokana na hilo. Kwa hiyo, nilikuwa nasema kuna umuhimu kwa Serikali kueneza elimu ya kusajili uvumbuzi wa wananchi wetu na kupata *patterns* na *data*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kusema ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kama nilivyosema, mambo yakiwa yameeleweka vizuri na wachangiaji wanakuwa wachache. Sasa nawaita sijui mtoa hoja au watoa hoja, ataanza Naibu Waziri au Mheshimiwa Waziri?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nami nichangie hoja iliyoko mbele yetu ya Itifaki hii. Kwanza kabisa, niungane na wenzangu, kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Kashililah kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge letu hili na Mheshimiwa Sophia Simba, dada yangu, kwa kuwa Mwenyekiti wetu mpya wa UWT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii, kwa sababu ndiyo mara yangu ya kwanza kusema hapa, nikupongeze wewe binafsi, Naibu Spika, Spika na Wenyeviti wote, kwa kutuongoza vyema katika Vikao vyetu vya Bunge kwa mwaka 2008. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, atupe busara na akuongezeeni busara na ujuzi, muendelee kutupa uwezo wenu, mapenzi miongoni mwetu na uadilifu ili pamoja tuweze kuwatumikia vyema waliotupa ridhaa ya kuwa hapa. *(Makofi)*

Pongezi za pekee kwa Wananchi wa Mbeya Vijijini, kwa kuamua kuunga mkono juhudi za Chama cha Mapinduzi na kutupa ushindi. Nasema hongera sana Mbunge wa Mbeya Vijijini, Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale na hongera sana Wananchi wa Mbeya Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme machache, kwa sababu mengi yaliyozungumzwa ni maoni mbalimbali, ambayo mimi na Mheshimiwa Waziri, tumekubaliana kwa dhati kabisa kuyashughulikia ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi ulioifanya nchi zetu tatu za Tanzania, Kenya na Uganda, ulifanyika katika Vikao vya *EAC* mwaka 2007 na kweli alisema Mheshimiwa Mwakyembe hapa muda umepita. Hili suala lilikuwa kwenye Sekretarieti, sisi tumeamua sasa hivi kulivalia njuga na kwamba, Sayansi na Teknolojia inachukua mkondo wake katika kuona uchumi wa nchi hii unafaidika na Sayansi, Teknolojia na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa nchi zilizoendelea, unatokana na kuboreka kwa Sekta ya Sayansi na Teknolojia na ubunifu katika nyanja za kilimo, *electronics* na viwanda, umerahisisha sana uzalishaji na kunyanyua Pato la Taifa na Mataifa mbalimbali ulimwenguni. Utafiti katika nyanja ya kilimo na matumizi ya tafiti hizo, zinasaidia sana katika maeneo kadhaa kupunguza baa la njaa kwa kuongeza uzalishaji. Hivi sasa watu wanafanya utafiti, *GMOs* na matumizi yake, haya yote ni masuala ya Sayansi na Teknolojia. Wenzetu wametumia sayansi, hata jana tulisoma kwamba, wamerusha *satellite* kule Iran na watajitegemea kupata taarifa zao kwa wepesi zaidi. Sayansi ina nafasi ya pekee katika ulimwengu huu wa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nchi zetu zikaona umuhimu wa kushirikiana katika maeneo ya Sayansi na Teknolojia. Tume hii tutakayoiridhia leo

baada ya kupitisha Itifaki hii, itasaidia sana kukuza ushirikiano katika masuala ya utafiti na maendeleo, ugharimiaji utafiti, kubadilisha taarifa za utafiti na matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano, teknolojia mpya ambazo zitajitokeza na kubuni Sera ya Sayansi ya Teknolojia za kikanda, kulingana na taratibu ambazo Tume hii na nchi wanachama itaziweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikubali kwamba, maoni yaliyotolewa na wachangiaji wote ni mazuri sana na kwamba ni wakati muafaka sasa, kuona umuhimu wa wataalam wetu kuchukua nafasi zao katika Tume hii. Ninawahakikishia kwamba, nitamsaidia sana Mheshimiwa Waziri, kuona hilo linatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa sababu mengi ni maoni mazuri, tutayafanyia kazi. Naomba niunge mkono hoja hii iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kutoa shukrani zangu za dhati, kwa wote waliochangia na kutoa maoni yao kuhusu Itifaki ambayo tunaipitisha hapa hivi sasa. Napenda nitumie nafasi hii, kuwatambua wale waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na vilevile waliochangia kwa maandishi. Kwa wale waliochangia kwa kuzungumza, napenda kuanza na Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe na Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aliyechangia kwa maandishi ni Mheshimiwa George Malima Lubeleje. *(Makofi)*

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote. Katika kuchangia, wamesisitiza umuhimu wa kutumia Sayansi na Teknolojia katika kuleta maendeleo ya haraka nchini mwetu na katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Umuhimu wa Itifaki hii ya nchi za Afrika Mashariki ni kwamba, tunaishi katika mazingira yanayofanana, wanadamu wote tuna matatizo yanayofanana; iwe kwa upande wa kilimo au kwa ufugaji, kwa hali ya hewa au kwa magonjwa ya mifugo.

Kwa hiyo, *development partners* ambao wanashirikiana na sisi katika maendeleo, mara nyingi wameona kwamba ni busara kutoa msaada kwa eneo kubwa zaidi, kuliko kusema nitakwenda kuisaidia Tanzania peke yake ama Kenya peke yake au Rwanda peke yake na kadhalika. Kwa sababu faida ambayo itatokana na kusaidia nchi katika eneo zima ni kubwa zaidi, kuliko kusaidia kila nchi moja ikawa inaomba peke yake.

Michango yote iliyotolewa ni katika kuboresha eneo hili la ushirikiano. Napenda niwahakikishie Wabunge kwamba, kuanzishwa kwa Tume hii, hakutakuwa ni mbadala wa Taasisi zetu za Utafiti tulionao hapa nchini. Tunatumia fursa hiyo vile vile kama nilivyoeleza kwenye faida zake kwamba, tutashirikiana katika utaalamu, tutabadilishana taarifa, tutashirikiana kutumia vyombo vya maabara, kwa mfano, kama kuna chombo fulani cha gharama ambacho kinapatikana hapa Tanzania, mtu wa Uganda, Kenya,

Rwanda hana haja ya yeye kununua chombo kama hicho hicho ambapo angeweza kununua kitu kingine. Kwa hiyo, kushirikiana katika kutumia vifaa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza haya ya jumla, napenda kutoa maelezo kwa kifupi sana katika yale ambayo yametamkwa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Nianze na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge na Miundombinu.

Kwanza, amesema Tanzania iwe makini katika kuchochea Watanzania kushika nafasi katika Tume hii. Mimi nafikiri ni wazo zuri sana kwamba, nafasi zitakazojitokeza tutajaribu kuwashauri Watanzania wengi na kutoa matangazo kwenye sehemu zetu mbalimbali, hata kwenye Taasisi ili Watanzania walio wengi na wenye sifa waweze kuomba.

Vilevile ameeleza kwamba, Wizara ni vizuri ikatoa ofisi na mazingira mazuri kwa ajili ya kuanzisha ofisi hiyo. Ningependa nijumuishe na mazungumzo aliyoyasema Mheshimiwa Mwakyembe, pamoja na hili kwamba, sisi tumeomba Tanzania iwe Makao Makuu ya hii Tume na Jumuiya ya Afrika Mashariki, ilituma ujumbe wa kutembelea nchi zote ambazo ziliomba. Walioomba ni sisi Tanzania, Kenya na Rwanda na kila Serikali ilichagua mjumbe mmoja awepo huko na walipita katika nchi zote hizi na kueleza nini ambacho tunacho kuweza kuvutia Tume hii Makao yake Makuu yawe hapa Tanzania. Kwa hiyo, kusema kweli bado mchakato unaendelea.

Katika yale tuliyowavutia, tulisema kwamba, sisi tupo tayari kwa kuanzia kwa sababu ni kitu kipya, kutoa nafasi ya ofisi na ndiyo maana nilitaka *hostage* ambapo tunaongeza *wing* moja inakarabatiwa na kwamba ule Sekretarieti inaweza kupata nafasi pale kwa muda. Tukasema tutaoa ofisi angalau kwa mwaka mmoja bure. Vilevile ili kuvutia Watanzania wengi wawemo humo, tukasema tupo tayari kutoa watafiti kwenye Sekretarieti hiyo angalau watano wa kuanzia na watalipwa mshahara na Tanzania. Tukaeleza pia kwamba, utakapokwisha mwaka mmoja, baada ya kutumia hizo ofisi basi kwa muda unaofuata, hiyo Tume itabidi kulipia hizo ofisi na vile vile tutakuwa tayari kutoa eneo ili Makao Makuu hayo yaweze kujengwa.

Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, ameuliza hizo ofisi Makao Makuu yake yatakuwa wapi? Kusema kweli ni mapema, kwa sababu hata kuambiwa kwamba ni sisi kweli ndio tutakuwa Makao Makuu bado hatujafikia huko. Mara itakapotokea, nafikiri busara zitatuma tuone ni mahali gani ambapo tutajenga. Kwa sababu nchi zote zilikuwepo, tuliambiwa katika nchi zote hizi tano za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania peke yake ndiyo kwenye kisiasa na usalama na ndiyo nchi pekee ambako Makao Makuu hayo yanaweza kufika. Kwa hiyo, uamuzi hatimaye utafanywa na *Summit*, yaani Wakuu wa Nchi hizi tano za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kwa hiyo, bado hatujapewa hiyo nafasi, lakini nina mategemeo na tunafuatilia maana tuliangalia vigezo wenzetu walitoa nini. Kama Rwanda walichotoa tunaona ni kidogo, Kenya nao walichotamka ni kidogo, tunafikiri huenda tukawa na nafasi hiyo, japokuwa bado na sisi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki tumekuwa ni Makao Makuu

ya Sekretarieti nyingi, pamoja na Sekretarieti yenyewe, upande wa Mahakama na mambo mengine, lakini tunaamini kwamba tutaweza kupata nafasi hiyo.

Vilevile karibu Wabunge wote wamesisitiza, pamoja na Mheshimiwa Zambi kwamba, tuhakikishe Watanzania wanaajiriwa. Mkakati mmojawapo ndio ule tuliosema kwamba, tutatoa watu wawe kwenye Sekretarieti na kuhamasisha sehemu nyingine. Kamisheni lazima iwe na uhusiano na vyombo vingine vinavyofanana navyo, hili ni jukumu mojawapo na katika majukumu, nafikiri hilo limejiweka sawa sawa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sikumbuki kifungu gani, lakini ni kifungu (g) ambacho kinaeleza kwamba, tuwe na mashirikiano na vyombo kama hivi ambavyo viko mahali pengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, imesisitizwa juu ya kuimarisha vyombo vyetu, nakubalia kabisa kwamba, hiki hakitakuwa mbadala, vyombo vyetu vya ndani vinataimarishwa zaidi na kwamba Sera ya Sayansi na Teknolojia iimarishwe. Napenda kuwaeleza kwamba, Sera ya kwanza kabisa ya Sayansi na Teknolojia iliandikwa mwaka 1986, ikaaridhiwa tena mwaka 1996 na sasa hivi ndiyo tunakamilisha Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, ambayo hatimaye italetwa hapa Bunge ili iweze kupitishwa.

Vilevile ilizungumziwa juu ya umuhimu wa Makao Makuu. Kama nilivyosema, hii inasubiri mpaka tupate jibu kamili kama Tanzania imeteuliwa au la. Mheshimiwa Zambi, pia aliuliza kwamba, Rwanda na Burundi walipojiunga ilikuwa vizuri kuonyesha makaratasi ambayo walitia sahihi mikataba. Sasa hili napenda kuelezea kidogo kwamba, Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, waliandaa vigezo maalum vya kutathmini maombi ya nchi zinazotaka kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vigezo hivyo vina sehemu nne:-

Sehemu ya kwanza, kuridhia Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ikiwa na maana ni Mkataba pamoja na Sheria, maamuzi na Itifaki zote zitokanazo na Mkataba wa Jumuiya. Pili, Bajeti ya Jumuiya, yaani uchangiaji wake na taratibu za Mfuko wa Pamoja. Tatu, Mfuko wa Uendeshaji wa Jumuiya kwamba, nao lazima auridhie. Nne, Mikakati ya Maendeleo ya Jumuiya. Hivyo basi, Wakuu wa Nchi Wanachama, waliziingiza nchi za Rwanda na Burundi katika Jumuiya, baada ya kuridhika na utekelezaji wa vigezo hivyo. Mkataba wa kujiunga ulisainiwa katika Mkutano wa Kilele wa Viongozi Wakuu wa Jumuiya, uliofanyika tarehe 18 Juni, 2007, Jijini Kampala Uganda. Kutokana na maelezo hayo, kuanzia tarehe hiyo nchi hizo zilijiunga rasmi na Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki, ikiwa ni moja ya Itifaki za Jumuiya pasipo kuhitaji kusaini upya Itifaki hiyo.

Nchi hizo zitajiunga kwa njia za kuridhia kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 22 cha Itifaki yenyewe, ambayo imetolewa kwa Wabunge wote. Ukiisoma hiyo *Article 22* ambayo ipo ukurasa wa 14, inazungumzia juu ya *Accession* na maelezo yale ndiyo yanayoridhia. Mtu anapojiunga siyo lazima arudi kutia saini Mkataba ule ambao ulisharidhiwa na wengine, baada ya kusaini Mkataba mkubwa wa kujiunga kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kuhusu Watanzania kujiunga kwenye Sekretarieti, hili limeshazungumzwa. Imeulizwa kwa nini Katibu Mkuu anakuwa na kipindi cha miaka mitano *fixed*, wakati Manaibu wake wanakuwa na vipindi vya miaka mitatu, lakini wanaweza ku-*renew contract*. Kimsingi ni kwamba ni miaka mitano na nchi hizi zipo tano. Iwapo huyu atapewa *renewal of contract* akawa na miaka kumi na hivi vitu ni *rotation*, basi huyu atakaa miaka kumi katika hizi tano pengine itachakua miaka 40 kabla watu wengine hawajafikiwa bado. Kwa hiyo, nafikiri kwa busara huyu Katibu Mkuu akae kwa kipindi kimoja cha miaka mitano.

Mheshimiwa Said Arfi anasema, Watanzania waandaliwe ili washiriki kikamilifu; nakubaliana na nimeshatoa maelezo kwamba, tuwaeleze Watanzania Mpango Mkakati wa Kuanzisha Tume hii. Ninafikiri katika hoja yangu ya kuwasilisha nimefanya hivyo kwa kueleza, lakini tutazidi kuwaelimisha Watanzania kutumia vyombo mbalimbali.

Mheshimiwa Zambi, nafikiri yale yote aliyoyazungumza ni ya msingi, nakubaliana naye kwamba, Sayansi na Teknolojia ni chimbuko la maendeleo ya nchi nyingi, lakini matumizi ya matokeo ya tafiti nyingi hayajatumika ipasavyo. Alitoa mfano wa mbegu ambazo zinazalishwa hapa nchini ni asilimia 25 tu na asilimia 85 zinakuwa *imported*. Tatizo la utafiti hapa nchini ni moja kama alivyosema yeye mwenyewe kwamba, *funding* ni ndogo sana. Nchi za Umoja wa Afika zilikubaliana kwamba, katika utafiti na maendeleo, kila Serikali ilijitahidi kutumia angalau asilimia moja ya pato ghafi la taifa.

Ninasikitika kusema kwamba, kiasi tunachotumia kwenye utafiti Tanzania kwa sasa hivi ni asilimia 0.028, ambayo ni kidogo sana. Nchi pekee ambayo imesukuma mbele katika hili ni nchi ya Afrika Kusini, ambapo kwa sasa hivi inatumia karibu asilimi 0.96 ya Pato la Taifa, lakini nchi nyingi sana hazijafika hata kwenye moja, angalau hawa wamesogea. Vilevile vifaa vya utafiti kwenye maabara sehemu mbalimbali ni tatizo. Tatizo lingine lilikuwa ni mishahara, lakini kwa upande wa utafiti inazidi kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uendelevu wa hii Tume ni kwamba, bajeti itatokana na bajeti ya nchi mbalimbali inayokwenda kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Maeneo mengi aliyoyataja Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe nimekwishayaeleza. Aliuliza vilevile kwa nini tumechelewa; Naibu Waziri amekwisha eleza. Nakubaliana na yeye kwamba, ushirikiano wetu si mpya kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki; kulikuwepo na *East Africa Research Organisation*, kulikuwepo na *East Africa Common Services Organisation* na vitu vingine vyote. Kuhusu vyuo kutokutoza aina moja ya ada isipokuwa Chuo cha Dar es Salaam tu, linatakiwa kufanyiwa ufuatiliaji na bahati nzuri Wizara inayohusika na hayo ipo watalitazama hili; kwa nini wakiuke yale mengine ambayo yalikwishakubaliwa.

Elimu ya Usaili wa Uvumbuzi wetu haipo; ni kweli lakini napenda kueleza kwamba, COSTECH sasa hivi ina Mfuko kabisa wa kuhamasisha wale wavumbuzi na

wanapewa zawadi. Mwaka 2008 nilitoa zawadi kwa wavumbuzi watano; wawili wa mambo ya *pump;* wengine madawa. Mfuko huo pamoja na kwamba hauna fedha nyingi sana, lakini umekuwa ukihamasisha watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli *BRELA* ipo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, lakini nafikiri kwa ajili ya kuwa na Sera, kuna haja kati ya hizi Wizara mbili tukae pamoja ili tuweze kuona hayo. Ukiangalia upande wa watafiti, Tanzania tuna watafiti wachache sana, hata *patents* ziko kidogo sana na tumekuwa-*ranked very low*. Mwaka 2007, katika nchi 131 kwa upande wa utafiti, Tanzania tumeonekana ni watu 130. Vilevile tatizo kubwa ni kwamba, vijana wengi sasa hivi hawapendi masomo ya sayansi, wengi wanakwenda kwenye michepuo ya masomo ya sanaa na biashara, kwa sababu wanaona haya yanatoa majibu ya haraka kuliko mahali pengine.

Mchango wa Maandishi kutoka kwa Mheshimiwa George Malima Lubeleje; nashukuru kwa maoni yake na kwamba, tutayafanyia kazi. Anasema pamoja na kuunga mkono hoja, anapenda kuchangia maeneo yafuatayo: Moja, marubani wote wanaoendesha ndege lazima wawe na sifa zinazotakiwa. Nafikiri haya hata jana yalizungumzwa, lakini sielewi kama hii ni sayansi kweli au ni ujuzi. Anasema kwamba, ndege zote zinazoruka ni lazima ziwe nzima kwa ajili ya usalama wa abiria.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mtoa hoja kuna utaratibu.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE**: Mheshimiwa Naibu Spika, haya anayojibu Mheshimiwa Waziri yanahusiana na Wizara ya Miundombinu, yamekwenda kwake kwa bahati mbaya. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa marekebisho hayo. Mwisho, napenda kutoa shukrani zangu za dhati, kwa wale waliochangia na napenda kuwahakikishia kuwa, yale yote waliyoyachangia, ushauri walioutoa na maswali waliyouliza, tutayafanyia kazi kwa ajili ya kuboresha. Bahati nzuri katika Itifaki hiyo, *article* ya 24 inatoa nafasi ya kubadilisha vipengele pale ambapo tutaona inafaa tufanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Kuanzishwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia liliridhiwa na Bunge)*

**Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ya Mwaka 2007 ya Kuanzisha Chombo cha Kusimamia Usalama na Ulinzi wa Anga** ***(Protocol on the Establishment of the East African Community Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency)***

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, kwa kuwa na mimi ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa tangu mwaka huu wa 2009 uanze, ninataka niwatakie wote kheri ya mwaka mpya wa 2009. Aidha, niwaletee salamu za mwaka mpya kutoka kwa mke wangu Vailet na wapigakura wote wa Jimbo la Chilonwa. *(Makofi)*

Naomba pia na mimi niungane na Wabunge wenzangu wote waliotangulia, kutoa salamu za rambirambi kwa kifo cha marehemu ndugu yetu, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini.

Sambamba na hilo, nitoe salamu za pongezi kwa Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale wa CCM, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Mbeya Vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, tamko la kukubali kuridhiwa kwa Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2007 ya Kuanzisha kwa Chombo cha Kusimamia Usalama wa Usafiri wa Anga *(Protocol on the Establishment of the East African Community Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency- CASSOA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kutoa shukrani nyingi, kwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, inayoongozwa na Mheshimiwa Alhaji Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, kwa kuijadili Itifaki hii kwa kina na kutoa ushauri kwetu kwa ajili ya utekelezaji wa chombo hicho kipya kitakachoanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, iliyoanzishwa kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 1999. Makao Makuu ya Jumuiya hiyo yapo Arusha, kama wote tunavyofahamu. Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, unazitaka nchi wanachama kuoanisha Sera zao zinazohusu usalama wa usafiri wa anga ili kufanya anga za nchi wanachama kuwa salama na kujiendesha kwa ufanisi na kiuchumi.

Lengo la Mkataba wa Jumuiya ni kuendeleza miundombinu, stadi za kifundi na teknolojia ili kusaidia nyanja nyingine za kiuchumi katika kutimiza malengo hayo. Katika kuanzisha malengo hayo, Jumuiya imeanzisha Wakala wa Kusimamia Usalama wa Ulinzi wa Anga, yaani *Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency - CASSOA* kwa lengo la kuimarisha usafiri wa anga na kuzitaka nchi wanachama kuridhia au kukubali Itifaki inayoundwa wakala huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya kuanzishwa kwa Wakala wa Kusimamia Usalama na Ulinzi wa Anga katika Afrika Mashariki ni kutimiza moja ya kanuni za usalama za usafiri wa anga, ambazo huwekwa na Shirika la Kimataifa la Usalama wa Anga Duniani, yaani *International Civil Aviation Organization,* yaani kifupi *ICAO.* Katika kutekeleza majukumu yake, *ICAO* huweka kanuni, viwango vya usalama na taratibu za usimamizi wa viwango hivyo katika maeneo mbalimbali kama vile viwanja vya ndege, ndege zenyewe na mafunzo. *ICAO* ilipitisha Azimio No. A 35/7 kupitia Mkutano wake Mkuu wa 35, chini ya azimio hilo linalohusu mkakati wa pamoja wa kutatua upungufu wa kiusalama, yaani *unified strategy to resolve, safety related efficiencies* ikawa inatambua uanzishaji wa mashirika ya kusimamia usalama ya kikanda, *Regional Safety Oversight Organizations*, kama hatua muhimu ya kusaidia nchi wanachama kutekeleza majukumu yao ya kusimamia usalama chini ya Mkataba wa CHICAGO wa Mwaka 1944.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala kama huu ulianzishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki katika maeneo mbalimbali duniani kama vile Visiwa vya Pacific na Visiwa vya Caribbean. Huko Visiwa vya Pacific, Shirika lao linaitwa *The Pacific Aviation Safety Office (PASO),* likiwa na Makao Makuu huko Port Villa Vanuwattu, wakati huko Caribbean linaitwa *The Regional Aviation Safety Oversight (RASOS),* likiwa na Makao yake Makuu huko Kingston Jamaica. Kila shirika limeweza kuzihudumia nchi zake wanachama kwa gharama ndogo kuliko ambavyo ingegharimia nchi moja moja kuzifikia ikiwa peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki, ilianzisha Itifaki inayohusu kuanzishwa kwa Wakala wa Usalama wa Ulinzi wa Anga *(The Protocol on Establishment of the East African Community Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency (CASSOA),* kwenye mkutano uliofanyika tarehe 18 Aprili, 2007 Arusha. Mkutano huo ulizitaka nchi wanachama kukubali Itifaki hiyo, kimsingi Itifaki inahusu kuunda chombo cha kiutawala kushughulikia maeneo ya ulinzi na usalama wa anga ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. *CASSOA* imeanza kazi tangu tarehe 1 Juni, 2007 kwa kuajiri watendaji wanaotakiwa. Wakala huu unafanyia kazi zake kwa muda kwenye ofisi za Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini kuanzia Julai, 2009 Makao Makuu ya CASSOA yatakuwa Entebe nchini Uganda. Kazi kubwa ya CASSOA ni kuratibu shughuli za ulinzi na usalama kwa kutumia wataalam wa nchi wanachama. Itifaki hii imeridhiwa na Uganda, ambapo Kenya ipo katika mchakato wa kuridhia, wakati Rwanda na Burundi zitajiunga na Itifaki baada ya kuridhiwa na nchi ambazo ni wanachama waanzilishi wa Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki ya *CASSOA* ina maeneo matatu muhimu; sehemu ya kwanza inahusu kuanzishwa kwa *CASSOA,* ambayo kisheria inaruhusiwa kuingia Mikataba kupata mali na kushtaki au kushtakiwa. Sehemu ya pili, inahusu uanzishwaji wa vyombo mbalimbali vya utekelezaji ndani ya *CASSOA.* Vyombo hivi ni pamoja na Bodi, Sekretarieti na Baraza la Mawaziri. Pamoja na kufafanua majukumu ya nchi wanachama, sehemu ya tatu inahusu masuala ya kifedha, ambapo vyazo mbalimbali vya mapato ya *CASSOA* vimeainishwa. Vyazo hivyo ni pamoja na michango ya nchi wanachama kupitia kwenye mamalaka yao ya usafiri wa anga, fedha zitakazotafutwa na

Jumuiya ya Afrika Mashariki, misaada kutoka kwenye vyombo vya Kanda na Kimataifa, mapato yatokanayo na shughuli za Wakala na vyanzo vingine vitakavyokubaliwa na Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, manufaa ya Tanzania kuridhia Itifaki ya *CASSOA* ni pamoja na haya yafuatayo: Kwanza, kupunguza matumizi makubwa ya rasilimali kwa kuwa na mfumo unaofanana wa Sheria, Kanuni na Udhibiti wa Usalama wa Usafiri wa Anga. Pili, kutumia wataalam na rasilimali zilizopo katika Jumuiya kwa pamoja. Tatu, kuoanisha mifumo ya kikanda, pamoja na kudhibiti mambo hatarishi kwa pamoja. Nne, kuimarika kwa ushirikiano kwa nchi za Jumuiya kwa kuongezeka eneo la ushirikiano wa usalama wa usafiri wa anga. Tano, kuboresha utendaji mahili na huru wa Wakaguzi wa Usalama wa Anga. Sita, kuendeleza uwezo wa kutunga na kuboresha Sheria na Kanuni za Usafiri wa Anga ili kuridhia kanuni na taratibu za kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhusiano uliopo kati ya Mamlaka za Usalama za Nchi Wanachama wa Jumuiya *(Civil Aviation Authorities)*, katika muundo wa sasa wa *CASSOA* ni kwamba, Mamlaka hizi zitaendelea na majukumu ya kudhibiti ulinzi na usalama wa anga katika nchi zao, kutoa leseni na vibali mbalimbali, kudhibiti wavunjaji wa sheria na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi. Upande wake litakuwa na majukumu ya kuoanisha kanuni za uendeshaji na kutengeneza viwango vitakavyofanana vya taaluma ya leseni, taratibu za leseni na vyeti.

*CASSOA* pia itakuwa na jukumu la kuongoza na kusaidia nchi katika kudhibiti Sekta ya Usalama wa Anga kwa kuweka namna ya kutumia pamoja rasilimali za kiufundi na rasilimali za watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Tanzania iweze kunufaika na Itifaki hii ni sharti kuikubali na kuiridhia kupitia Bunge lako Tukufu. Kwa mujibu wa ibara ya 19 ya Itifaki; ni kwa msingi huo Serikali inapendekeza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania likubali kuridhia Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Ibara ya 63(3)(e), Bunge la Jamhuri ya Muungano lina mamlaka ya kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano, ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa. Itifaki hii ni moja kati ya mikataba ambayo mashari yake yanahitaji yaridhiwe na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa manufaa yatakayopatikana kwa nchi yetu kukubali kuridhia Itifaki hii ni makubwa, Serikali inapendekeza Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuhusu kuanzishwa kwa Wakala wa Kusimamia Usalama na Ulinzi wa Anga ya Mwaka 2007 *(The Protocol on the Establishment of East Africa Community Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency 2007)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lifuatalo ni Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki:-

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(East African Comminity)* kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Uanzishsaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 1999;

NA KWA KUWA katika Kikao cha Baraza la Mawaziri cha tarehe 7 Novemba, 2008 Baraza la Mawaziri liliazimia kuridhiwa kwa Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2007 ya kuanzishwa kwa Chombo cha Kusimamia Usalama na Ulinzi wa Anga;

NA KWA KUWA kwa kuridhia Itifaki hii Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa imetimiza mojawapo ya viwango vya usalama wa usafiri wa anga ambavyo huwekwa na Shirika la Kimataifa la Usalama la Anga Duniani *(International Civil Aviation Organisation – ICAO),* ambayo inatambua uanzishwaji wa mashirika ya kusimamia usalama wa kikanda *(Regional Safety Oversight Organisations)* kama kitu muhimu cha kusaidia nchi wanachama kutekeleza majukumu yao ya kusimamia usalama chini ya Mkataba wa Chicago wa Mwaka 1944.

NA KWA KUWA Itifaki hii inazitaka nchi wanachama kuoanisha sera zao zinazohusu usalama na ulinzi wa anga ili kufanya anga za nchi wanachama kuwa salama, kujiendesha kiufanisi ili kuendeleza miundombinu, stadi za kiufundi na ukuaji wa tekinologia na nyanja nyingine za kiuchumi;

NA KWA KUWA katika kutimiza malengo hayo Jumuiya ya Afrika Mashariki imeanzisha Wakala wa Kusimamia Usalama na Ulinzi wa Anga kwa lengo la kuimarisha usafiri wa anga na kuzitaka nchi wanachama kuridhia Itifaki;

NA KWA KUWA kwa kuridhia Itifaki hii Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaweza kuimarisha ushirikiano wake na nchi za Afrika Mashariki katika kuimarisha usalama na ulinzi anga wa Afrika Mashariki na hivyo kupunguza ajali za ndege na kukidhi viwango vya ulinzi na usalama vinavyotakiwa na *ICAO*, hivyo kupelekea uchumi wa nchi wanachama kuimarika kwa kupungua kwa gharama za kusimamia usalama na ulinzi kutokana na wataalam wa usalama na ulinzi wa kutoka kila nchi wanachama kutumika katika Jumuiya;

HIVYO BASI kwa kuzingatia umuhimu wa Itifaki hii na manufaa ambayo Tanzania kwa mujibu wa Ibara 63(3)(a) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Sura ya Pili, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Nne sasa linaazimia kuwa Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2007 ya Kuanzishwa kwa Chombo cha Kusimamia Usalama na Ulinzi wa Anga *(Protocol on the Establishment of East African Community Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency – CASSOA*) ya 2007 iridhiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 63(3)(e) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kinachotamka kuwa, Bunge litajadili na kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa na kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 114(11) ya 2007, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu kuanzishwa kwa Chombo cha Kusimamia Usalama na Ulinzi wa Anga, 2007 *(Protocol on the Estabilishment of the East African Community Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency - CASSOA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kuhusu Itifaki hiyo, naomba nitumie nafasi hii, kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Sophia Mnyambi Simba, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), pamoja na wote walioshinda nafasi mbalimbali katika Uchaguzi huo wa UWT uliofanyika mapema mwezi Januari, 2009.

Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, aliyeibuka mshindi katika Uchaguzi Mdogo wa Ubunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, uliofanyika tarehe 25 Januari, 2009. Ninawatakia wote heri katika majukumu yao mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 23 Januari, 2009 Kamati ilipokutana Jijijini Dar es Salaam, Serikali iliwasilisha Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu kuanzishwa kwa Chombo cha Kusimamia Usalama na Ulinzi wa Anga, 2007 ili kujadiliwa, kupata maoni na ushauri wa Kamati na hatimaye kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu kwa kulijadili na hatimaye kuliridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, CASSOA ni Wakala wa Usalama na Ulinzi wa Anga. Wakala huu umeanzishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki, kupitia Itifaki ya Mwaka 2007. Mkutano ulioanzisha Wakala huu, ulifanyika tarehe 18 Aprili, 2007 Mjini Arusha. Chimbuko la kuanzishwa kwa Wakala huu ni tarehe 12 Novemba, 2004 ambapo Nchi za Jumuiya Afrika Mashariki; yaani Uganda, Kenya na Tanzania, zilitiliana sahihi makubaliano ya Ushirikiano katika kuboresha usalama na ulinzi, uongozi na kujenga uwezo katika usafiri wa anga ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Itifaki ya CASSOA, ibara ya 20 inasema; nchi itakayojiunga na Jumuiya Afrika Mashariki, itabidi pia ikubali na kujiunga na Itifaki hii. Kwa msingi huo, Rwanda na Burundi zinasubiri Itifaki hii iridhiwe na nchi Waanzilishi wa Jumuiya, yaani Uganda, Kenya na Tanzania, ndipo nazo ziweze kuikubali. Itifaki hii itaporidhiwa, itakuwa na nguvu ya kisheria *(enter into force).*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuwa na Wakala kama huu siyo mgeni, kwani hata Jumuiya iliyovunjika ya Afrika Mashariki, ilikuwa na Chombo kama hiki. Aidha, Jumuiya ya *SADC* ipo mbioni kuunda ushirikiano kama huu katika masuala ya Usafiri wa Anga. Upo pia msukumo wa kuziunganisha Jumuiya za *EAC, SADC* na *COMESA* katika masuala ya usalama na usafiri wa anga. Nia ni kuwa na ushirikishwaji mpana zaidi katika masuala ya usalama wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Kimataifa la Usalama wa Anga Duniani *(International Civil Aviation Organization – ICAO),* ambalo Tanzania ni Mwanachama, linaunga mkono uanzishwaji wa vyombo kama *CASSOA* kwa nchi maskini. Shirika hili ndilo linalosimamia usalama na ulinzi wa usafiri wa anga duniani, kwa kuweka kanuni, viwango vya usalama na taratibu za usimamizi wa viwango hivyo katika maeneo mbalimbali kama vile viwango vya ndege, ndege zenyewe, mafunzo na kadhalika. Pia huweka viwango mbalimbali vya huduma *(Standard and Recommended Practices (SARPs),* vitolewavyo kama viambatanisho *(Annexes)* vya Mkataba wa Chicago wa 1994. Pia kuratibu usafiri wa ndege duniani ili kuhakikisha kuna uwiano wa Kimataifa wa Usalama wake na kutoa maelekezo kuhusu njia bora ya kufanya biashara ya usafiri wa anga kati ya nchi na nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa *CASSOA,* ulitokana pia na Mkakati wa pamoja wa kutatua upungufu wa kiusalama (*Unified Strategy to Resolve Safety Related Deficiencies),* uliofikiwa na *ICAO* katika Mkutano wake Mkuu wa 35 kupitia Azimio A 35 – 7. Kupitia Azimio hilo, *ICAO* ilitambua uanzishwaji wa Mashirika ya Kusimamia Usalama wa Kikanda *(Regional Safety Oversight Organisation),* kama kitu muhimu cha kusaidia nchi wanachama zenye uwezo mdogo kiuchumi, kumudu kutekeleza majukumu ya kusimamia usalama wa usafiri wa anga chini ya Mkataba wa Chicago.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi Kanuni za Kimataifa, inabidi Taifa liwe na Wataalam wa kutosha katika nyanja zote na vilevile wenye mafunzo, utaalamu, uwezo na uzoefu *(trained, qualified, competent and well experienced).* Jambo hili siyo rahisi sana, kwa nchi masikini kama Tanzania; ndipo uanzishwaji wa *CASSOA* unakuwa ni njia mojawapo ya kuboresha shughuli za kudhibiti usalama wa usafiri wa anga na kuboresha shughuli hizo. Kimsingi, chini ya *CASSOA,* nchi wanachama zitakuwa na utaratibu wa kuazimana wataalam pamoja na ufundi mwingine. Aidha, *CASSOA* itakuwa inahakikisha kwamba, Sheria, Kanuni na Miongozo ya Kiufundi ya Usalama na Ulinzi kwa Usafiri wa Anga zinaoana. *CASSOA* pia itahakikisha kuwa, nchi wanachama zinakuwa na viwango vinavyofanana vya kiufundi vya ndege zitakazokuwa zikifanya safari katika Jumuiya. Nchi hizo pia zitakuwa na mipango ya pamoja ya kufundisha wataalam wa fani za usalama wa ulinzi wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza sana Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu, kwa kuleta Itifaki hii mbele ya Bunge lako Tukufu ili iweze kuridhiwa, kwani faida zake kama tulivyoona hapo juu ni nyingi sana. Kwa kuwa Kenya ni nchi pekee ambayo imeridhia, baada ya Tanzania kuridhia, nchi iliyobaki ya Uganda iombwe kuridhia haraka. Kwa kufanya hivyo, kutazifanya Burundi na Rwanda nazo ziikubali Itifaki hiyo.

Kamati ina maoni kwamba, kama Itifaki ingekuwa imeanza kufanya kazi mapema, pengine kile ambacho kililipata Shirika letu la Ndege la Tanzania *(ATCL)*, kwa kufungiwa kufanya kazi zake pengine kisingeweza kutokea; kwani ingekuwa rahisi kubadilishana uzoefu katika uendeshaji mzuri wa Mashirika ya Ndege kwa Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa gharama za uendeshaji wa *CASSOA* zinaonekana kuwa kubwa, zinazokadiriwa kufikia Dola za Kimarekani 1,349,306, Kamati inashauri ziangaliwe njia bora ikiwezekana kupunguza matumizi hayo, pamoja na kudhibiti matumizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa chini ya *CASSOA* ndege za nchi wanachama zitakuwa zinatumia anga za nchi zao kwa kanuni za aina moja, Kamati inashauri nchi yetu kupitia Mamlaka yake ya Usafiri wa Anga (*Tanzania Civil Aviation Authority),* kuwa makini sana na matumizi hayo ili kutoruhusu matumizi yanayoweza kuleta madhara katika anga letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya *CASSOA,* Nchi Wanachama kama tulivyoona, zitakuwa na uwezo wa kuazimana wataalam na kufundisha wataalam wa fani mbalimbali pamoja. Kamati inaunga mkono jambo hili na inaishauri Serikali, kutobweteka kufundisha wataalam wake, kwani tayari Watanzania wana kumbukumbu ya kile kilichotokea mwaka 1977, pale Jumuiya ya Afrika Mashariki ya wakati huo ilipovunjika. Hivyo, tushirikiane kwa tahadhari na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kwamba, kwa kuwa Itifaki mbalimbali zinazoletwa mbele ya Kamati za Kudumu za Bunge lako Tukufu zina maslahi kwa Taifa letu, basi ni vizuri Wajumbe wazipate mapema. Hii itawapa Wabunge fursa nzuri ya kuzisoma, kuzitafakari na hatimaye kutoa ushauri ulio bora zaidi, kuliko ilivyo sasa kwani Itifaki nyingi huletwa kwenye Kamati kwa muda mfupi sana na Kamati hutakiwa zitoe ushauri na maoni yake tayari kwa kuwasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kwamba, kwa kuwa majukumu ya vyombo hivi viwili *TCAA* na *CASSOA* kimsingi yanafanana na kwamba, tofauti yake kimoja ni chombo cha kikanda *(Regional Body*) na kingine ni chombo cha nchi, basi shughuli zake ziainishwe vizuri. Hii itasaidia kuondoa migongano inayoweza kujitokeza. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kupita *TCAA, TAA, ATCL,* pamoja na wadau wengine, kuimarisha miundombinu ya usafiri wa anga, viwanja vyetu vya ndege na kukuza taaluma za wataalam wazalendo na hivyo, kuifanya nchi yetu kuwa tayari kuingia kwenye chombo hiki cha *CASSOA* kitakapoanzishwa rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara, kwa kumpata Mtanzania mwenzetu kuwa mtendaji wa kwanza wa kukiongoza Chombo hicho. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoridhika na nafasi hiyo moja. Pamoja na ukweli kwamba, nafasi nyingi za kazi zitatolewa kwa kuzingatia uwiano, bado kutahitajika maarifa zaidi kuhakikisha kwamba, nafasi zinazohusu Watanzania haziendi kwa wengine. Vilevile

kuchukua nafasi nyingine zaidi kwa kutumia kila aina ya ushawishi. Aidha, Wizara ihusike katika kuwashawishi Watanzania wenye sifa, kujiandaa kuingia kwenye ajira hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati yangu, naomba nitumie fursa hii, kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Waziri wa Miundombinu; Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Naibu Waziri wa Miundombinu; Mhandisi Omar A. Chambo, Katibu Mkuu wa Wizara; Pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo, kwa kuwasilisha vizuri Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki hiyo, mbele ya Kamati yangu, jambo ambalo limerahisisha majadiliano na kuiwezesha Kamati kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, kwa kazi waliyoifanya ya kuipitia na kuijadili Itifaki hii na kutoa maoni yatakayoisaidia Serikali katika utekelezaji wake. Naomba niwatambue Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Alhaji Mohamed Hamisi Missanga - Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Kilango Malecele – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Paschal Constantine Degera, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu, Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Joyce Martin Masunga, Mheshimiwa Mhandisi Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Balozi Dkt. Getrude I. Mongella, Mheshimiwa Alhaji Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mheshimiwa Sigifrid Seleman Ng'itu, Mheshimiwa Mwaka Abdulrahaman Ramadhani, Mheshimiwa Philemon Mikol Sarungi na Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Didimu Kashilillah, pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa huduma mbalimbali zinazoisaidia Kamati yangu katika kutekeleza wajibu wake.

Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati hii; Bwana James John Warburg na Bibi Justina Mwaja Shauri, kwa kuiwezesha Kamati ya Miundombinu kutekeleza majukumu yake ya kila siku na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii kwa ufanisi unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ya Miundombinu, imejadili Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2007 ya kuanzishwa kwa Chombo cha Kusimamia Usalama na Ulinzi wa Anga *(Protocol on the Establishment of the East African Community Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency*) na kwamba, Maoni na Ushauri wa Kamati umezingatia mahitaji ya nchi. Kwa maana hiyo, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuridhia Itifaki hiyo kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2007 ya kuanzishwa kwa Chombo cha Kusimamia Usalama na Ulinzi wa Anga (*Protocol on the Establishment of the East African Community Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nguvu na afya njema kwa kipindi chote cha mwaka uliopita na mwaka huu toka uanze. Vilevile kwa kuniwezesha kuwa mbele yenu ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Azimio la kuridhia Itifaki ya Afrika ya Mashariki juu ya Uanzishwaji wa Chombo cha Kusimamia Usalama na Ulinzi wa Anga kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana nzima ya Azimio lililo mbele ya Bunge lako Tukufu, Kambi ya Upinzani haina pingamizi nalo; isipokuwa inataka ufafanuzi kadhaa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa Kambi ya Upinzani pamoja na Watanzania wote, tunaelewa na kuamini kuwa suala la ulinzi wa mipaka ya nchi yetu lipo mikononi mwa Mamlaka ya Jeshi la Ulinzi na Usalama na tunaposema mipaka ya nchi yetu, maana yake ni ardhini, majini na angani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tayari Serikali ilikwishanunua rada ya kisasa ya ulinzi na usalama wa anga ya Tanzania, ambayo kwa kipindi hicho aliyekuwa Waziri wa Wizara hiyo, Mheshimiwa Prof. Mwandosya, alilifafanua kuwa ununuzi wa rada hiyo ya kisasa, utaongeza usalama wa anga ya Tanzania na kuongeza mapato kwa ndege ambazo zilikuwa zinaingia anga yetu bila kuwa na kibali chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, kuwahakikishia Watanzania kuhusu ushirikiano huu wa masuala ya usalama wa anga kwa nchi mwanachama wa Itifaki hii, kwani hapo nyuma kulikuwepo na kutokuaminiana kati ya nchi wanachama, ambako kulitokea baina ya Uganda na Rwanda. Kwetu sisi suala hili ni vipi kwani usalama wa nchi ni siri ambazo hata sisi wabunge hatuna ufahamu nazo na huwa hatuhoji masuala hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha takriban miaka 20 iliyopita, Serikali yetu haijafundisha watu wanaotaka kujiunga katika fani hii inayohusu masuala ya anga. Aidha, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo, haitoi mikopo kwa ajili ya kuwasomesha vijana wanaotaka kujiunga katika fani hii. Hali halisi ni kwamba, wataalam wengi tulionao katika fani hii, umri wao umeshakuwa mkubwa kiasi kwamba, miaka mitano hadi kumi ijayo, watakuwa umri wao hauwaruhusu kuendelea na kazi ya umma; na hivyo, nchi yetu itakuwa haina wataalam katika fani hii na suluhisho litakuwa ni kwa kutegemea wageni. Je, nchi yetu imejipanga vipi katika kuhakikisha haiathiriki?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, baada ya kutoa angalizo hilo hapo juu, kwa ujumla haina pingani na kuridhiwa kwa Azimio la Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Bakari Shamis Faki kwa maoni yako, nimeshangaa rada imeingiaje, Itifaki haijasema habari ya rada imeingia tu! *(Kicheko)*

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa wasaa wa kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Awali ya yote, kutokana na kile kinachoitwa *pressure* kupanda na kushuka, nilishindwa kutoa salamu za mwaka mpya kwa wapiga kura wangu wa Tunduru, kwa hiyo, nawatakia Heri ya Mwaka Mpya. Sikufanya hivyo katika mchango wangu wa awali. Vilevile natoa hongera za dhati kabisa, kutoka ndani ya moyo wangu, kwa Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuchaguliwa na Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Akinamama, kuwa Mwenyekiti wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, natoa pongezi za dhati kwa Mwenyekiti wetu wa UWT Mkoa wa Ruvuma, Dada Kuruthum Matomondo, naye kwa kuwa Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile natoa pongezi za dhati, kwa kaka yangu, Mchungaji Mwanjale, kwa ushindi mnono alioupata katika uchaguzi mdogo wa kuziba pengo. Kwa ustaarabu tulionao wana-CCM, sitasita kutoa pongezi kwa Ndugu Mponzi, Mgombea wa CUF, kwa kudhubutu kushiriki katika uchaguzi ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo na pongezi, napenda kueleza dhahiri shahiri kwamba, naunga mkono uwasilishi wa Itifaki hii. Endapo tutaunga mkono Itifaki iliyo mbele yetu ni dhahiri kabisa ni moja ya kuunga mkono mwelekeo na maagizo ya Baba yetu wa Taifa, Mwalimu Nyereye; Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema.

Ukisoma kile kitabu cha *South South Commission*, utaona namna gani Mwenyekiti Mwenza wa *Commission* ile ambaye ni Baba wa Taifa, alivyohimiza mashirikiano ya Nchi na Nchi, pamoja na mashirikiano ya Kanda. Kama sote tunavyofahamu, Afrika Mashariki ni mashirikiano ya nchi na nchi katika Kanda na Itifaki hiii inahimiza hilo. Kwa hiyo, namna sahihi ya kumuenzi Baba yetu wa Taifa ni pamoja na kuridhia Itifaki hii iweze kupita.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, *CASSOA* kama inavyosomeka kwa kifupi, uzuri wake haiondoi yale mamlaka ya chombo chetu cha Kitaifa cha *Tanzania Civil Aviation Authority (TCAA)*, sana sana *CASSOA* itakachokifanya ni kujaribu kuimarisha utendaji bora wa *TCAA.* Kwa hiyo, hiki ni chombo ambacho kitaleta manufaa makubwa sana kwa nchi yetu. Kwa hiyo, kwa ushirikiano na kwa uelewa mkubwa wa Bunge lako Tukufu, ninaamini kabisa Wabunge wote tutaunga mkono Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kuimarisha utendaji, lakini *CASSOA* vilevile ina mwelekeo wa kupunguza gharama za utendaji wa vyombo vyetu vya Kitaifa vya udhibiti wa anga zetu. Kwa mfano, gharama za kumsomesha rubani mmoja kwa sasa hivi ni takriban Dola 60,000. Gharama za kumsomesha Mhandisi wa Ndege kwa sasa hivi ni takriban dola 45,000. Sasa kwa kutumia chombo hiki cha *CASSOA*, itakuwa rahisi kabisa kwa nchi zetu hizi tano za Afrika Mashariki na Kati, kuhakikisha kwamba gharama hizi zinatumika kwa pamoja na tunasomesha wataalam wetu kwa pamoja, ambao tutawatumia kwa pamoja. Sasa Tanzania badala ya kutumia mamilioni ya fedha kama nchi peke yake, kwa Itifaki hii itatuwezesha sisi kama taifa, kutoa tu mchango katika fungu lile kubwa ambalo bila chombo hiki, nchi yetu ingelazimika kutumia fedha zile nyingi. Kwa hiyo, *CASSOA* ni mwelekeo mzuri licha ya kuleta ushirikiano wa kikanda, lakini vilevile itasaidia kupunguza gharama za kulinda anga zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Itifaki hii itatuelekeza kuhakikisha kwamba, pale itakapotokea upungufu katika nchi moja na endapo upungufu ule haupo katika nchi nyingine, basi Itifaki hii inatuwezesha kupata huduma kwa nchi jirani kwa ule upungufu ambao unayo, kwa gharama nafuu tofauti na Itifaki hii kama isingeweza kurithiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa mwisho ni kuisihi Serikali. Hivi karibuni tumejulishwa kwenye Kamati kwamba, Wahandisi na Marubani tulionao, wengi umri wao ni mkubwa na wengine ambao wamesomeshwa hivi karibuni wamekuwa wakiingia kwenye sekta nyingine na wengine hata kutoka nje ya nchi. Wanachokifuata huko ni maslahi. Sasa kwa kuwa gharama za kuwasomesha hawa watu ni kubwa na vile vile kwa kuwa mahitaji ya watu hawa nayo ni makubwa, naiomba Serikali ijaribu kuboresha maslahi ya marubani wetu, ijitahidi kuboresha maslahi ya wahandisi wa ndege, ili kile kinachoitwa *Retainment* kiwe katika *level* ya juu. Tusipofanya hivyo, nchi itakuwa inatumia fedha nyingi kuwasomesha wataalam wake, matokeo yake wataalam hao wanakimbia, wanakuwa hawana maslahi tena kwa Taifa letu ingawa ndilo lililowagharimia kuwasomesha. Kwa hiyo, naisihi sana Serikali iliangalie suala la kuboresha maslahi ya marubani, *engineers* na wale wote wanaohusika katika sekta ya usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kutoa mchango mdogo lakini vilevile lazima *ni-declare interest* mimi ni miongozi mwa wajumbe wa Kamati hii ya Miundombinu. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuzingatie Kanuni ya 151, ambayo imesema kabisa kuwa, kwa kuokoa muda, wenzetu waliopata nafasi mbalimbali walishapongezwa na Mheshimiwa Spika na kama heri ya mwaka mpya, mmeshapelekeana barua, kwa hiyo, tusipoteze muda. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Herbert Mntangi, namshukuru Mheshimiwa Arfi ameliondoa jina lake. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninaomba kusema kwamba, ninaunga mkono hoja hii ya Azimio la Kuridhia Itifaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja kubwa ambalo lazima tulifahamu ni kwamba, kuridhia na kuwa na chombo kimoja ndani ya jumuiya yenye nchi zaidi ya nchi tatu, tunategemea Rwanda na Burundi zitajiunga, ina faida moja kubwa; Kwanza, vyombo vinavyotumika katika kusimamia shughuli za usalama wa anga, kwa mfano, rada, vyombo maalum vya hali ya hewa na mambo mengine mengi, vyombo hivi kimsingi ni ghali sana. Kwa hiyo, kwa kuwa na nchi zaidi ya moja zinazokaa pamoja na kushirikiana katika mfumo huu kwa pamoja, inatoa fursa kwa nchi hizi kugawana gharama hizo kubwa na kupunguza mzigo mkubwa kwa nchi moja moja peke yake. Kwa hiyo, hii ni faida kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wanaotakiwa kuendesha na kusimamia vyombo hivi ni adimu na ni wachache sana, ndani ya Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, tutapata fursa vilevile ya kutumia wataalam hawa wachache kwa kuendesha shughuli za usalama kwa nchi zaidi ya tatu. Inawezekana tukawa na upungufu mkubwa wa wataalam katika nchi moja kama Tanzania, lakini tukamtumia mtaalam mmoja wa kutoka Uganda na akatoa huduma zinazotosheleza kwa nchi zote tano za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwagharimia elimu wataalam hao kama nilivyosema katika vyombo vingine ni gharama kubwa. Kwa msingi huo ni kwamba, wataalam hao hao tukaoanza kuwatumia katika nchi tano kwa madhumuni yale yale maana yake ni kwamba, nchi hizi tano tutakuwa tumegawana gharama ya kumpata mtaalam mmoja badala ya kupata wataalam watano kwa ajili ya kila mtaalam katika kila nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapokuwa na chombo kimoja, kwa mfano, rada inayoongoza ndege, yenye uwezo mkubwa itakayoweza kuangalia eneo lote la Jumuiya ya Afrika Mashariki na tukakubaliana kimsingi kwamba, tunaweza tukatumia chombo hicho sisi wanachama wote, maana yake vilevile itasaidia kwa kiwango kikubwa, kuondoa usiri mkubwa unaoweza kufanyika katika baadhi ya nchi kwa kupitisha vyombo vya hatari katika nchi zetu. Kwa vile tunatumia chombo kimoja ni dhahiri ndege zote zitakazokuwa zinaingia ndani ya eneo ya anga la Afrika Mashariki, zitakuwa zinafuatiliwa mwenendo wake na chombo kimoja na haitakuwa siri; Kenya wataona, Tanzania wataona, Uganda wataona, Rwanda wataona na Burundi wataona. Kimsingi usiri huo unasaidia vilevile katika kujenga usalama zaidi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida nyingine kubwa ni kwamba, vyombo hivi vinapokuwa vya nchi moja moja, hadhi yake inakuwa sio kubwa sana. Tunapokuwa na chombo kimoja kikubwa kwa ajili ya nchi zaidi ya moja na hii maana yake nchi tano za Jumuiya ya Afrika Mashariki, vyombo hivi vinapata hadhi kubwa zaidi kimataifa na ni rahisi vyombo kama hivi, kutambuliwa na kupata misaada ya kimataifa ili kuviwezesha kuviimarisha viweze kufanya kazi zao vizuri zaidi na kwa usalama zaidi kwa abiria na wale wote wanaoutumia anga. Kwa hiyo, pia ni faida moja kubwa ya kuwa na mchakato

wa kuridhia Itifaki hii, kwa ajili ya kuwa na chombo kimoja ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo kama hivi kwa Tanzania na kwa nchi nyingine zote za Afrika Mashariki, vitakuwa vinasaidia kwa sababu vinalenga kwenye usalama. Kwa hiyo, vitasaidia kutoa muongozo kwa mfano, kuhakikisha kwamba viwanja vyote vya ndege vinawekwa taa ili ndege ziweze kutua kwa usalama hata wakati wa usiku. Vipo viwanja vingine havina taa, kwa hiyo, chombo kama hiki kitaweka msukumo na kwa sababu Tanzania au Kenya ni Mwanachama wa Chombo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la kuweka taa katika viwanja vya ndege, litatekelezwa kwa sababu ni agizo la chombo tulichokiridhia. Vilevile litasaidia kuhakikisha kwamba, hata urefu wa viwanja vya ndege, kufuatana na viwango vya kimataifa vinafuatwa; hivyo, pale ambapo viwanja vya ndege havina urefu wa kutosha, ninaamini chombo kama hicho kinachosimamia usalama, kitaweza kutoa maoni na ushauri na kuongeza urefu wa viwanja vyetu vya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile vitaweza kusimamia vyombo vingine vinavyotoa huduma za usalama, kwa mfano, magari ya zima moto, wataweza kuhakikisha na kutoa ushauri kwamba, viwanja vyetu vya ndege kwa sababu ya usalama huo wa anga, basi tuwe na magari ya viwango vinavyotakiwa kimataifa, badala ya kuwa na Land Rover 109, zenye uwezo mdogo, inawezekana wakapendekeza viwango vikubwa zaidi vya kukidhi hali ya usalama na tukavitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala moja ambalo linatokana na usimamizi. Hapa Tanzania tunayo mamlaka inayosimamia shughuli za anga *(TCAA)* na inafanya kazi zake vizuri, lakini kwa sababu inatambuliwa na chombo cha kimataifa kinachosimamia shughuli za usalama wa anga duniani *(ICAO)*, basi mamlaka yetu hii pia inakaguliwa na chombo hicho cha kimataifa. Matokeo ya ukaguzi wa chombo hicho cha kimataifa kwa mamlaka yetu, ndiyo iliyopelekea Watanzania kusikia Shirika la Ndege la Tanzania *(ATCL)* limesimamishwa. Walifanya ukaguzi na hapa nataka niwaondoe wasiwasi Watanzania, ukaguzi uliofanywa na chombo hicho cha kimataifa kwa mamlaka yetu, ndiyo uliodhihirisha kwamba shirika letu la ndege ile leseni yake ya kufanyia kazi kwa shughuli za anga, ilikuwa imekwishapitwa na wakati, walitakiwa ku-*renew*. Kwa kuwa walikuwa na matatizo mengi ya kifedha, hawakuweza kufanya kazi hiyo.

Ili ku-*renew* yapo mambo muhimu lazima uyafanye ya uthibisho wa marubani wako, uthibitisho wa vyombo vyako, ndege unazotumia, uthibitisho wa vifaa vingine muhimu na kadhalika. Kwa sababu yote haya, yalikuwa yanahitaji fedha na shirika halikuwa na fedha, hawakuweza kufanya mambo hayo kwa wakati. Matokeo yake chombo kile cha kimataifa kilipofanya ukaguzi, kikaishauri mamlaka yetu ya Tanzania kwamba, mnalo shirika la ndege, lakini muda wake wa leseni za kufanya kazi umepita hawaja-*renew*. Ninyi kama wasimamizi wa nchi, mnapaswa kuchukua hatua kuhakikisha kwamba, *ATCL* ina-*renew* leseni yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, walipopewa muda na kwa sababu waliendelea kuwa hawana fedha, walishindwa kukamilisha kazi hiyo kwa wakati waliopewa na chombo kile cha Kimataifa, hivyo mamlaka yetu ikalazimika kuwasimamisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo sahihi watu wakaamini kwamba, *ATCL* ilisimamishwa kwa sababu ilikuwa na ndege mbovu hapana; ilisimamishwa kwa sababu leseni yao ilikuwa imekwisha na walishindwa kukamilisha kanuni kwa wakati na taratibu za kimataifa za kuhakikisha kwamba, leseni yao inafufuliwa. Hilo ndilo lilikuwa la msingi, kwa hiyo, suala la ndege mbovu halipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumza mabadiliko ya ndege za zamani na ndege za kisasa, ndege za *series* zilizopita si kwamba ni mbovu, unaweza ukawa na boeing 237 ya kizamani, lakini ipo kwenye hali nzuri sana na inafanya kazi vizuri. Tofauti ni kwamba, ndege hizo series za kizamani, kwa mfano, Air Tanzania walikuwa nayo hiyo boeing 237 lakini gharama zake ni kubwa sana kuiendesha. Kwa hiyo, ni lazima uende kwenye ndege za kisasa ambazo uvumbuzi umeonesha wameweza kupunguza gharama za mafuta za kuendeshea ndege hizo. Ndiyo maana utaona sasa hivi Air Tanzania, wanazo ndege hizi japokuwa ni ndogo lakini ni za kisasa na wana mpango kabambe wa kuagiza ndege nyingine kubwa zaidi ya saba za kimataifa, ambazo tunaamini kabisa zitakuwa za kisasa na zitatuhakikishia kwamba, shirika hili litafanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania waelewe kwamba, ndege za Air Tanzania zimeanza kuruka karibu wiki moja iliyopita nataarifa za juzi, jana na leo, zile ndege zilizokwenda Mwanza zenye uwezo wa kubeba abiria hamsini zimejaa zote, ndege ya jana abiria arobaini na nane, viti viwili tu vilikuwa vimekosa abiria, leo abiria 49 kiti kimoja tu kimesalia. Kwa hiyo, bado Watanzania wana imani na Shirika lao la Ndege la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona nilizungumze hilo ili kuwaondoa hofu Watanzania na tulijengee imani na heshima Shirika letu la Ndege la Tanzania. Nina imani nitaendelea kulitumia na Watanzania wengi wataendelea kulitumia. Matarajio yetu ni kwamba, litafanya vizuri kwanza kwa kuruka ndani ya nchi ya Tanzania na litaanza tena kuruka nje ya nchi ya Tanzania na wenzetu wa nje ya Tanzania wataendelea kulitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunisikiliza na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa tena nafasi, nami nitoe mchango wangu kwenye hoja hii. Kwanza, niseme naiunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono kwa kuelewa kama mtu niliyewahi kufanya kazi kwa mwaka kwenye sekta hii kwamba, sekta hii ya usalama wa anga ni muhimu mno kwa wasafiri wa ndege na kwa uchumi wa Taifa. Tatizo la biashara ya

ndege huku Afrika ya Mashariki ni kwamba, biashara hii ni ngumu sana, ndiyo maana sisi kama Taifa, biashara hii imetuyumbisha sana na hata sasa hivi tupo mahali pabaya. Ukweli ni kwamba, miundombinu ya biashara hii Afrika ya Mashariki; Tanzania, Kenya na Uganda ni michache sana inayofikia kiwango cha kimataifa. Viwango vyetu vibovu, viwanja vyetu vibovu na ni vya zamani na ndege ni za zamani hazina viwango, wataalam wanafikia umri wa kustaafu na hakuna wapya na wengine ni marubani, wahandisi wa ndege na wataalam wenyewe wa Shirika la *Civil Aviation* Afrika ya Mashariki.

Kwa hiyo, kwa lugha nyingine, unaweza ukasema kwamba, eneo hili la *Civil Aviation* la Biashara ya ndege kwa ujumla si la kuridhisha kwa ujumla wake. Kwa hiyo, kama nchi zetu zinataka kuungana ili kufanya kazi nzuri zaidi ni jambo la kuungwa mkono na kwa kweli naweza nikasema tumechelewa.

Mhehsimiwa Naibu Spika, nilibahatika kwenda Nigeria kwenye mkutano wa mambo ya *Civil Aviation* mwaka 2006; na Nigeria inasemekana ndiyo nchi yenye ajali nyingi za ndege kuliko nchi yoyote ya Afrika. Tukiwa pale wiki ile tu ilianguka ndege moja ikaua maafisa 12 wa ngazi za juu za Jeshi. Wiki moja baada ya kuondoka, ikaanguka ndege nyingine ikaua abiria karibu mia kule. Hata mimi niliona mambo ya ajabu, kwenye ndege kule saa ya kutoka, kama mmeshafika sasa mnataka kwenda zenu, mnapakuwa kwenye ndege ni kama mpo kwenye basi. Mimi nimeingia kule ndani, nikaambiwa onesha sanduku lako nikaonesha, nikaambiwa chukua sanduku lako nikachukua, ingiza kwenye ki-*van* kidogo kipo palepale unaingiza kinakupeleka kwenye *customers* unajitokea unaondoka zako. Kama una masanduku mengi ndiyo tatizo, maana sijui nani atakubebea upo ndani kabisa ya kiwanja cha ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nchi moja jina nalihifadhi, ambayo watu hupanda ndege na mbuzi na kuku. Kupanda ndege ni tofauti na unavyopanda basi, baiskeli au bajaji, lakini nchi zetu hazijafikia viwango hivyo. Kwa hiyo, kuwa na chombo kinachosema jamani tusiingie na mbuzi kwenye ndege au ni hatari kabisa kuwa na gari, gari linaloendeshwa kwa mafuta linatoa cheche pale pale kwenye ndege likisubiri masanduku yapakuliwe. Mambo namna hiyo ni lazima sisi wenyewe tusaidiane au tukemeane kwamba, tabia hiyo haifai.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo la msingi ni ukosefu wa fedha, kama unataka kutengeneza viwanja vyako viwe vizuri wape fedha, unataka ndege zako ziwe nzuri wape fedha, unataka kusomesha watalaam hao wape fedha. Kwa hiyo, tatizo la msingi ni fedha na nchi zetu zilivyo, nchi kwa nchi haifai kusema mimi ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na chombo chake hiki kama huko nyumbani hujajiandaa kuwa na fedha za kuboresha vile vitu ambavyo ni vyako na ambavyo vinasimamiwa na lile shirika lako la mambo ya usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nashauri kwamba, lazima tuangalie upya namna ya kupata fedha za kuboresha viwanja vya ndege na miundombinu mingine katika nchi yetu, pamoja na vifaa na kuangalia ndege zinavyoruka. Labda hapa si mahali pake, lakini ni lazima nikiri kwamba, bajeti inayotolewa kila mwaka hata kama tungesema ni ya kutengeneza viwanja vidogo tu kama cha Tunduru kilisemwa hapa juzi, hatuna fedha za

kutosha.  Kwa hiyo ni lazima tutumie njia nyingine za kupata fedha za kuweza kufikia viwango hivi vya Kimataifa vya miundombinu ya biashara ya ndege ili tuweze kufanikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliambiwa kwenye Mkutano huo kwamba, tatizo lingine la Afrika ni ndege za kizamani.  Ninafikiri nitasikika tu kwamba, baadhi ya ndege zinazoruka kwenye Bara la Afrika haziruhusiwi kuruka Ulaya.  Ndege hata kama inaonekana ni sawa kwenye injini na kadhalika, lakini kama ina umri Fulani, pamoja na kwamba haina kasoro zinazodhihirika, hairuhusiwi kuruka.  Baadhi ya ndege zinazoruka huku Afrika, haziwezi kuruka zaidi ya Cairo, zikiingia Ulaya zitanyimwa kibali, Amerika zitanyimwa kibali.  Kwa hiyo ni kweli kwamba, kuwa na vyombo vipya vya ndege na ndege mpya za kisasa zinazoendana na wakati ni sehemu ya kulinda usalama wa wasafiri wa ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao cha Ouagadougou kilichofanywa miaka ya 1990, Afrika tulikubaliana kwamba, tushirikiane kwa kufungua milango ya nchi zetu ili sisi kwa sisi tuwe na soko kubwa la ndege.  Badaye tuliunda kitu kinachoitwa *Kentown Convetion*, ambayo sisi Bunge letu hapa tuliridhia mwaka jana. *Convetion* hii itawezesha nchi za Kiafrika kununua ndege za kisasa kwa bei nafuu.

Ninafahamu toka turidhie, bado hatujajiandikisha kwenye makao makuu ya utaratibu huo ili watu wetu wanaotaka kununua ndege mpya kama Air Tanzania, leo tumesikia kwamba, wana mpango wa kununia ndege mpya sijui zifike tisa; waweze kutumia unafuu huo na kuleta ndege za kisasa na mashirika mengine yote ya ndege.  Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba Naibu Waziri na Wizara kwa ujumla, waharakishe *registration* ya lile Azimio tulilolitoa hapa ili wanaotaka kunua ndege za kisasa katika nchi yetu au hata kukodi tu, waweze kufaidika na utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa na ndege za kisasa ni muhimu na mimi nataka kuwaambieni, baadhi ya ndege zinazoruka hapa Tanzania zingeenda Ulaya zisingeruhusiwa.  Bahati mbaya kwenye hili, sikubaliani sana na Mheshimiwa Mntangi, kwa sababu mimi nina uelewa kidogo wa mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujitahidi kuwa wa kisasa kwa kila hali katika biashara hii.  Marubani waliofundishwa vizuri, wahandisi waliofundishwa vizuri, wataalam wa *Civil Aviation* waliofundishwa vizuri, viwanja vya ndege vya kisasa, ndege zenyewe za kisasa na nidhamu ya kuendesha vyombo hivi, kama nilivyosema ukishaingia kwenye ndege na ng'ombe na magari ya mizigo, ndiyo haitakiwi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ningependa kusisitiza kwamba, kwa sababu kwa muda mrefu hatufundishi wataalamu hawa, Afrika ya Mashariki kwa ujumla ni lazima tujitahidi kwa sababu hata wale wachache tulionao, wengi wanaibwa na nchi nyingine; kwa mfano, Marubani wa Tanzania wapo Kenya, wapo mpaka India, Asia na nchi nyingine za Afrika.  Kwa kuwa wana uzoefu, wanajua leo wanatafutwa kila mahali na bei yao ni kubwa sana.  Marubani wanaozunguka humu ndani, hatuwalipi kimataifa na ndiyo maana wanakuja kuwaiba watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumalizia kwa kusema tena naunga mkono hoja, lakini mambo haya tuyafanye inavyotakiwa ili tuweze kufaidika. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, kwa kuleta Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo sina mengi ya kuchangia ila kukumbusha mchango wangu niliochangia siku ya bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, juu ya umuhimu wa kuwawezesha wanafunzi marubani wa Tanzania, nao kuweza kulipiwa kama wenzao ili Tanzania pia iwe na marubani. Bila kufanya hivyo, usalama wa anga huu unaozungumziwa leo ukiacha mambo mengine, utakuwa mikononi mwa wageni tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza *precision air* kwa kuwa na marubani wanawake, sijui kama nao ni Watanzania. Pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa hatua alizochukua kuinusuru *ATC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani pia bado kuna tatizo la *management*, japo sina taarifa za kina; ni vyema tufuatilie ili tujiridhishe kuwa tatizo lilikuwa la mtaji tu. Mungu awabariki.

**MHE. DR. LUKA J. B. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uungaji mkono hoja hii, napata tatizo juu ya maudhui halisi ya neno 'chombo' katika Itifaki hii kama ilivyotafsiriwa kutoka neno la kiingereza *Agency*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashindwa kuelewa kama kitu hiki kinachoridhiwa ni 'Wakala' kwa maana ya *Agency* au ni Mamlaka kwa maana ya '*Authority*'?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya kuridhia Itifaki hii, kwa kuwa usimamizi wa usalama na ulinzi wa anga wa kikanda, kwa maana wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, unahakikisha usalama wa eneo zima la ukanda huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakupongeza kwa kuleta Azimio hili muhimu. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, napenda kuchangia maneno yafuatayo:-

Marubani wote wanaoendesha ndege, lazima wawe na sifa zinazotakiwa. Ndege zote zinazoruka ni lazima ziwe nzima, kwa ajili ya usalama wa abiria. Ndege mbovu zipigwe marufuku kuruka zitahatarisha usalama wa abiria. Vilevile ihakikishwe kwamba, huduma inaboreshwa ndani ya ndege na kwenye viwanja vya ndege na vifaa muhimu vya kuongozea ndege ni lazima viwepo na viwe vya kutosha kama rada na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii tena, kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha maelezo niliyoyatoa wakati nawasilisha Itifaki ya Chombo cha Usalama wa Anga.

Nachukua nafasi hii, kuwashukuru sana Wabunge wote waliopata fursa ya kuchangia katika hoja hii, ambayo kwa ujumla wake wote wameunga mkono. Ninawashukuru sana kwa kuunga mkono hoja hii. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu wetu, ningependa niwatambue waliochangia kwa kusema hapa Bungeni na wale ambao wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimwa Wabunge waliochangia kwa kusema kwanza ni Mheshimiwa Godrey Zambi, ambaye alikuja hapa kuzungumza kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu, Mheshimwa Bakari Shamis Faki, alizungumza kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimwa Herbert James Mntangi na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa George Malima Lubeleje, ambaye mchango wake ulikuwa umeelekezwa kwenye Wizara nyingine, Mheshimiwa Lucas Siyame na Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoanza kusema, nawashukuru Waheshimwa Wabunge wote, kwa sababu wameunga mkono. Maelezo mengi waliyotupa hapa ni ya kutupa moyo tu kwamba, tutakaporidhia Itifaki hii, basi tuweze kuwa waangalifu na kutoa ushauri ambao tunatakiwa tuutekeleze katika kuisimamia Itifaki ambayo tutairidhia muda si mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na Kamati yetu ya Miundombinu, kama nilivyosema mwanzo, ukiachilia mbali ushauri waliotupa kwenye Kamati kule kwa kuzungumza na kutupa maelekezo mbalimbali, lakini kwenye taarifa yao iliyowasilishwa hapa, wametufafanulia mambo mengi ambayo nisingependa kuyapitia yote, lakini nakubali angalizo walilotupa kwamba, tuhakikishe tunasimamia uboreshaji wa wataalam, pamoja na kutoa mafunzo kwa watalaam wetu, ili chombo hiki kitakapoanza kutumika,

wataalam wetu ama wananchi wetu, wasiwe wasindikizaji badala yake washiriki kikamilifu.

Mheshimwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba, tumelizingatia na kwa taarifa tu ni kwamba, sasa hivi tupo katika harakati za kuanzisha Mfuko kwa ajili ya mafunzo, kama vile ambavyo Waheshimwa Wabunge wengine walivyokwisha kusema hapa kwamba, wanafunzi wetu katika eneo hili la marubani, pamoja na mafundi, wamekuwa hawalipiwi gharama za mafunzo. Ninafikiri baada ya kutambua hilo, hapa Tanzania kupitia Chombo chetu cha Mamlaka ya Udhibiti wa Hali ya Usafiri wa Anga kwa kushirikiana na vyombo vingine vya sekta ya usafiri wa anga, tumeanzisha huo Mfuko ambao utasaidia kuhakikisha tunafundisha wanafunzi, pamoja na wataalam mbalimbali ili tutakapokuwa tunakitumia chombo hiki, tusionekane kwamba ni wasindikizaji. Niseme tu kwamba ni bahati nzuri hivi sasa chombo hiki kilivyoanzishwa, kama ambavyo wenzetu wa Kamati ya Miundombinu walivyojata hapa, sasa hivi kinaendeshwa na Mtanzania, ambalo ni jambo la kujivunia, kwa hiyo, tutaendeleza kasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, kwa taarifa hata katika mchakato ule wa kupata watendaji wengine katika chombo hiki, kwa sasa inaonekena kwamba, Watanzania ndio walikuwa na nafasi kubwa zaidi, kwa sababu katika wale wanne waliokuwa wanatakiwa, walioko sasa hivi ingelikuwa kama ni kuchukua tu waliokuwa wamestahili zaidi walikuwa ni Watanzania wote, lakini kwa sababu ya kupeana ile *share* ya Kinchi ndio maana nafasi nyingine ikabidi wenzetu wengine wapate. Kwa hiyo, katika hili, hatupo nyuma sana, lakini haimaanishi kwamba, tutalala usingizi. Tutaendelea kuhakikisha kwamba, tunafundisha watu wetu na tunakuwa sambamba nao. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Upinzani alizungumizia suala la *CASSOA*; Chombo cha Kuoanisha na Kusimamia Sheria na Kanuni na alitaka kujua matumizi ya rada ili kuongoza ndege na mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili tunasema kwamba, *CASSOA* ni Chombo cha Kuoanisha Sheria na Kanuni kwa usalama wa usafiri wa anga linaloziunganisha. Linalozungumzwa hapa ni anga za ndege na sio la *Civil Aviation*, halihusiani na usalama ule ambao tunaujua kwa maana ya *defence.* Kwa hiyo, usalama tunaozungumzia hapa ni ule wa kiraia, ndio maana inajulikana kama *Civil Aviation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata hapa ushauri kutoka kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutakapokuwa tunatekeleza Itifaki hii, lazima tuwe waangalifu wa kuona kwamba, vifaa mbalimbali vinavyotumika viwe katika ubora unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa ambayo inatufanya turidhie Itifaki hii ni kuunganisha nguvu zetu pamoja katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hii itatufanya tuweze tukachangia nguvu na hata katika upatikanaji wa vyombo, pamoja na wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji waliochangia kwa njia ya maandishi, tukianza na Mheshimiwa Siyame, aliaka kupata ufafanuzi ama kuelewa kwa nini tunakiita hiki chombo na kule kwenye kiingereza tunakiita *agency?* Kusema kweli hapa nadhani labda ni kujumuisha maneno, lakini chombo hiki kwa kiswahili tunaweza tukakiita ni wakala. Kwa hiyo, tukiita chombo ama tukiita walaka ni jambo hilo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya, alisititiza suala hili la kwamba, wanafunzi wetu hawapati fedha za mafunzo; nimekwisha kulijibu. Tutakapoanzisha Mfuko, kwa vyovyote vile fedha hizo zitaweza kusaidia kuhudumia kwenye masomo kule na kulipia gharama zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lubeleje amesisitiza suala la Marubani wa Ndege lazima wawe na sifa zinazotakiwa. Haya ndio madhumuni yenyewe ya kuanzisha chombo hiki, kwa sababu kinakuwa kinawadhibiti na kuangalia kama kweli wanastahili na kuna suala vilevile la kutumia wataalam hao kwa pamoja, badala ya kuwa unajitegemea mwenyewe katika *full recources.* Kwa hiyo, kama utakuwa huna wataalam ambao unaweza kuwatumia mwenyewe, ukapitia chombo hiki kuweza kuelewesha wataalam hawa na wengine wapo wapi ili kuweza kuwatumia kwa utaratibu huo, tutakuwa tunapunguza gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazungumzaji wengine waliozungumza hapa ni Mheshimwa Mtutura, ambaye amejaribu kuonyesha faida za chombo hiki. Kusema kweli ndio tulizozieleza hata sisi katika uwasilishaji, lakini msisitizo wa kwamba katika kuunga mkono lazima tuonyeshe chombo hiki kinaunga mkono mashirikiano ya South South; tunadhani kwamba ni jambo zuri na itakuwa ni mahali pazuri pa kuanzia. Hata wenzetu ambao hawajaridhia hasa katika jambo lile la kusema tuwasukume wengine ambao hawajaridhia, Kenya peke yake sasa hivi ndiyo itakuwa bado haijaridhia, kwa sababu Uganda tayari walikuwa wamesharidhia.

Kenya wataridhia muda si mrefu, kwa sababu utaratibu wa Kenya ni tofauti na wa kwetu; wenzetu wanapitisha Itifaki hizi kupitia ngazi ya Baraza la Mawaziri. Kwa hiyo, nadhani baada ya sisi kuwa tumeridhia, utakuwepo msukumo mkubwa zaidi wa kuhakikisha na wao wanaridhia ili kutoa nafasi kwa wenzetu waliojiunga baadaye na Jumuiya; nchi za Rwanda na Burundi, nazo zinajiunga ili tuanze kukitumia chombo hiki ipasavyo.

Mamshukuru sana Mheshimiwa Herbert Mtangi, kwa maelezo yake aliyoyaeleza hapa ya kuonesha jinsi ambavyo chombo hiki kitakuwa ni kiungo, lakini vilevile kwa kutoa ufafanuzi. Napenda nitumie nafasi hii kuelezea hapa kwamba, tunapozungumzia ndege za zamani, haimaanishi kwamba ndege hizo ni mbovu, inaweza kuwa ni ndege za zamani lakini bado zinatembea kwenye anga. Niseme tu kwamba, ndege hata ikiwa ya zamani, haiwezi kupewa nafasi ya kuruka mpaka iwe imethibitishwa kwamba, ina uwezo wa kuruka angani. Kwa hiyo, suala la kusema kwamba, ukishakuwa na ndege za zamani huwezi kuzirusha angani, kama zina uwezo wa kuruka angani zinaweza zikaruka tu. Kwa hiyo, nakushukuru sana kwa ufafanuzi huo na mimi nimeona nitumie nafasi hii

kulisemea hilo. Naomba tusiwe na hofu yoyote, kama ndege itakuwa ni ya zamani lakini bado ina uwezo wa kuruka inaweza kuruka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba, Mheshimiwa Basil Mramba mwishoni alitahadharisha kwamba, ndege zetu hizi tulizonazo nchi nyingine zinaweza zisiruke. Inawezekana, kwa sababu ya kutofautina katika hatua za kimaendeleo, sisi hapa ndiyo tunaanza, kwa hiyo, zile tulizonazo tunaendelea kuzitumia na wakati huo tunaendelea kukusanya nguvu zetu. Namshukuru sana Mheshimiwa Basil Mramba, kwa ushauri wake, pamoja na uzoefu aliotuonesha wa matatizo yanayojitokeza katika nchi nyingine ambazo hazina chombo kinachofanana na hiki ambacho tunakianzisha hapa. Kama kweli inafika mahali watu wanaingia na mbuzi kwenye ndege, inakuwa ni kitu cha hatari, kwa hiyo, anachosisitiza ni kwamba, chombo hiki kina umuhimu wake kwa sababu ndiyo kitatuweka kwenye ulimwengu wa kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mramba, amegusia vilevile suala la kufundisha wataalam wetu; hili nilikwishaligusia. Suala la kufundisha wataalam wetu, lina kipaumbele cha kipekee kabisa, hasa tunapoanzisha chombo hiki. Ninadhani tutakapokuwa tumekamilisha mipango yote baada ya kuridhia, tutakuwa na nafasi ya kusimamia wataalam wetu, kuboresha maslahi yao kama Wabunge wengine walivyosema na hasa ukizingatia kuwa, wataalam wetu wengine wameshazeeka. Mafunzo haya yatakuwa ndiyo *replacement* ya hao watakaokuwa wanazeeka na maslahi yakiboreshwa, hili suala la kukimbia kutoka nje litafutika, tutakuwa tunawavuta wanarudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia hapa, wametupa ushauri wa jinsi ambavyo tunatakiwa kuwa waangalifu, tunapoingia katika kutekeleza Itifaki hii. Naomba tu niishie hapa kwa kusema kwamba, tutayazingatia haya yote ambayo wametushauri na sisi kwa upande wetu tutaendelea kupata uzoefu hata wa nchi nyingine, kuona ni namna gani utekelezaji wa suala hili la usalama wa anga linatekelezwa ili tuende katika ulimwengu wa kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la kuanzisha Chombo cha Kusimamia Usalama na Ulinzi wa Anga liliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ningependa kutoa taarifa ifuatayo: Kwanza kabisa, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, wanatakiwa kwenye kikao mara baada ya kuahirishwa kwa shughuli za Bunge katika Ukumbi wa Msekwa. Pili, kesho ni Siku ya Alhamisi, ndiyo siku ya maswali kwa Waziri Mkuu. Taarifa tulizonazo ni

kwamba, watu wanakwenda kujiandikisha saa kumi na moja asubuhi; mkienda saa kumi na moja asubuhi ofisi itakuwa imefungwa, kwa hiyo, mfike pale saa moja na nusu, mkifika saa kumi na moja askari atawazuia mlangoni. Naomba mzingatie hilo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kusema sina tangazo lingine isipokuwa naomba niwashukuru kwa kazi ya siku ya leo. Tumeendesha kazi vizuri, niwatakie jioni njema na niaahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.29 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 5 Februari, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*